JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI,SANAA NA MICHEZO



# HOTUBA YA MHESHIMIWA PAUL CHRISTIAN MAKONDA (MB.), WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

MEI, 2026

DODOMA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba akifurahia burudani ya ngoma wakati alipowasili kufungua Mkutano wa 110 wa Watayarishaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma (WASHITIRI), unaoratibiwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC uliofanyika jijini Arusha, tarehe 25 Machi, 2026.

# VIONGOZI WA WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



Mhe. Paul C. Makonda (Mb.)
WAZIRI



Mhe. Hamis M. Mwinjuma (Mb.)
NAIBU WAZIRI



Bw. Gerson P. Msigwa
KATIBU MKUU



Bw. Methusela S. Ntonda
NAIBU KATIBU MKUU

## YALIYOMO


ORODHA YA VIFUPISHO ............................................ iii

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1

2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA ........................ 10

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2025/26 ............................ 13

4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO ........... 149

5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27 ........................................................ 151

5.1 SEKTA YA HABARI ............................................ 151

5.1.1 IDARA YA HABARI - MAELEZO ................. 151

5.1.2 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC) 152

5.1.3 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN) 153

5.1.4 BODI YA ITHIBATI YA WAANDISHI WA HABARI ................................................... 154

5.1.5 KAMATI YA MAUDHUI ............................. 155

5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI .......... 156

5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI . 156

5.2.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA) 157

5.2.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA ........................................ 158

5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA ................... 158

5.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA .......... 158

5.3.2 BODI YA FILAMU TANZANIA .................... 159

5.3.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA) .... 159
5.3.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA) 160
5.3.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa) ................................ 161
5.3.6 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA ................................................ 162
5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO ............... 162
5.4.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO ...... 162
5.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT) ..... 164
5.4.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA ...................................................... 165
5.4.4 UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU ...................................................... 166
5.5 MIRADI YA MAENDELEO .................................. 166

6.0 SHUKURANI .................................................... 174

7.0 HITIMISHO ...................................................... 178

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AAFCON | The African Amputee Football Cup of Nations |
| AFCON | Africa Cup of Nations |
| AICC | Arusha International Conference Center |
| AMIS | Artist Management Information System |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BASATA | Baraza la Sanaa la Taifa |
| BET | Black Entertainment Televison |
| BMT | Baraza la Michezo la Taifa |
| BRELA | Business Regulations and Licensing Agency |
| CAC | Chamwino Arts Center |
| CAF | Confederation of African Football |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CDEA | Culture and Development East Africa |
| CHAN | Championship of African Nations |
| CMOs | Collective Management Organizations |
| COSOTA | Copyright Office of Tanzania (Ofisi ya Hakimiliki Tanzania) |
| CRDB | Benki ya CRDB |
| CRJE | China Railway Jianchang Engineering |
| DEV | Development |
| EDCF | Economic Development Cooperation Fund |
| eGA | e - Government Authority |
| FEASSSA | Federation of East Africa Secondary School Sports Associations |
| GOYN | Global Opportunity Youth Network |
| HAPAWARDS | Hollywood and African Prestigious Awards |
| KOICA | Shirika la Ushirikiano Kimataifa la Korea |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |

| | |
|---|---|
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| JNICC | Julius Nyerere International Conference Center |
| JNHPP | Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere |
| KAKAMA | Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki |
| KOICA | Korean International Cooperation Agency |
| MASIKIDU | Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani |
| MTV | Music Television |
| MUM | Muslim University of Morogoro |
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Eduction and Training |
| NEST | National e-Procurement System of Tanzania |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NBS | National Bureau of Statistics |
| NCAA | Ngorongoro Conservation Area Authority |
| NEEC | National Economic Empowerment Council |
| NMB | National Microfinance Bank |
| OAU | Organisation of African Union (Umoja wa Nchi Huru za Afrika) |
| OBFT | Open Boxing Federation of Tanzania |
| OC | Other Charges (Matumizi Mengineyo) |
| OWM – TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PE | Personal Emoluments |
| RTD | Redio Tanzania |
| SADC | Southern African Development Community |
| SARS | System ya Usajili wa Vyama vya Michezo |
| SAUT | Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino |
| SHIMISEMITA | Shirikisho la Michezo la Serikali za Mitaa Tanzania |

| | |
|---|---|
| SHIMIWI | Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali |
| SHIMMUTA | Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Kampuni Binafsi Tanzania |
| SIMA | Sports Infrastracture Management Agency |
| SJMC | The School of Journalism and Mass Communication |
| SGR | Standard Gauge Railway |
| TAMRISO | Tanzania Music Rights Society |
| TANAPA | Tanzania National Park |
| TaSUBa | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| TAPSEA | Tanzania Personal Secretaries Association |
| TAUSI | Tax Administration Universal System Interface |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TBC | Tanzania Broadcasting Corporation |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TCRA | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| TCTA | Tanzania Correction Training Academy |
| TFB | Tanzania Film Board |
| TFF | Tanzania Football Federation |
| NIC | Shirika la Bima la Taifa |
| TIN | Taxpayer Identification Number |
| TMA | Tanzania Music Award |
| TOA | Tanzania Olympians Association |
| ToT | Training of Trainers |
| TPA | Tanzania Port Authority |
| TPBRC | Tanzania Professional Boxing Regulatory Commission |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |

| | |
|---|---|
| TSC | Tanzania Safari Channel |
| TSN | Tanzania Standard Newspapers |
| TWFA | Tanzania Women Football Association |
| UAE | United Arab Emirates |
| UCSAF | Universal Communication Service Access Fund |
| UDSM | University of Dar es Salaam |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| UMISSETA | Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania |
| UMITASHUMTA | Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania |
| UNESCO | United Nations, Educational, Scientific and Cultural |
| VIP | Very Important Person |
| VON | Voice of Nigeria |
| WAFCON | Women's Cup of Nation |
| WAWAMAKI | Kikundi cha Wanawake Wajasiriamali wa Sanaa za Ufundi cha Kijiji cha |
| WWO | Waandishi Waendesha Ofisi |

**HOTUBA YA MHESHIMIWA PAUL CHRISTIAN MAKONDA (MB.), WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO, AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo katika Bunge lako Tukufu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fungu 96) kwa mwaka wa Fedha 2026/27.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupatia uhai, afya njema na kutuwezesha kukutana tena siku ya leo kujadili ustawi wa sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu atuongoze katika kujadili hotuba hii ya bajeti kwa dhamira ya kuhakikisha Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo zinakuwa na mchango mkubwa katika maendeleo na ustawi wa Taifa letu.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kwanza, kuwa Naibu Waziri na baadaye Waziri kamili wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Hii ni heshima kubwa sana kwangu na kwa familia yangu na naichukulia kama chachu ya kuendelea kulitumikia Taifa hili kwa bidii, weledi na uadilifu mkubwa. Ninamwahidi utumishi uliotukuka katika kuzisimamia sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Sekta hizi ni za kimageuzi, zikisimamiwa vizuri zitazalisha ajira kwa vijana. Hili litakuwa lengo langu katika kipindi chote nikiwa katika nafasi hii. Kama alivyosema Mheshimiwa Rais wakati ananiapisha, VIJANA TUNAELEWANA NA TUTAKWENDA PAMOJA.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri na maono mapana yanayolenga kuleta maendeleo kwa mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa Taifa kwa ujumla. Pia, nimpongeze kwa kuendelea kuliongoza Taifa vyema katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na changamoto mbalimbali, hususan migogoro ya vita ya Mashariki ya Kati na vita ya Urusi na Ukraine ambayo imeathiri kwa kiasi kikubwa uchumi wa dunia, ikiwemo kupanda kwa bei za mafuta na bidhaa mbalimbali. Pamoja na changamoto hizo, Mheshimiwa Rais ameendelea kutuongoza kama Taifa kubaki katika umoja, mshikamano na amani.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue fursa hii ya kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John

Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kwake kwa awamu nyingine ya pili, na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa kwake kushika nafasi hiyo. Aidha, nawapongeza viongozi hawa wote kwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais. Viongozi hawa wamekuwa chachu na msaada kwa Mheshimiwa Rais kwa kutupatia maelekezo pamoja na ushauri unaosaidia kuboresha sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo. Ninawashukuru na kuwapongeza sana.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** nizidi kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyotoa utekelezaji wa malengo ya Serikali katika mwaka 2025/26 na mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2026/27. Pamoja na masuala mengine hotuba hiyo imetoa maelezo kuhusu Sekta zilizo chini ya Wizara. Wizara yangu imezingatia na itatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuliongoza kwa busara na weledi mkubwa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maelekezo na miongozo yako imekuwa msingi wa ufanisi mkubwa wa

Bunge katika kuisimamia Serikali kutekeleza vema majukumu yake. Vilevile, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.), Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukusaidia na kukushauri vema katika majukumu yako ya kuliongoza Bunge. Nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.), Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso (Mb.) na Mheshimiwa Najima Murtaza Giga (Mb.) kwa kusimamia vema na kwa ustadi mkubwa mijadala katika Bunge lako Tukufu.

**8. *Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb.), na Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe (Mb.), Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa maelekezo, ushauri na maoni yao kwa Wizara yangu ambayo yametusaidia sana katika kuboresha utendaji kazi. Maelekezo yao yamesaidia kwa kiwango kikubwa katika uwasilishaji wa hotuba hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Kamati hii imekuwa nguzo muhimu katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa bajeti na ukaguzi wa miradi, ambapo imefanikisha kuhakikisha rasilimali za umma zinatumiwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya umma. Kama misingi ya nyumba imara, ndivyo uongozi wa Kamati hii ulivyojenga msingi madhubuti wa maendeleo, unaoleta mafanikio endelevu na mabadiliko chanya katika jamii yetu.

**9. *Mheshimiwa Spika***, pia, nitumie fursa hii kuwashukuru waheshimiwa wabunge wote kwa maoni, ushauri na maelekezo ambayo yamekuwa yakiisaidia Wizara kuboresha vipaumbele, mikakati na pia kuweka msingi imara wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi zaidi.

**10. *Mheshimiwa Spika,*** ni masikitiko yangu kwamba katika kipindi cha mwaka 2025/26 Bunge lako Tukufu lilipatwa na misiba mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge. Misiba hiyo ni pamoja na msiba wa Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Mbunge wa Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Peramiho, na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu akiwawakilisha Wafanyakazi. Kwa niaba ya Wizara na wadau wetu, tunatoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, familia za marehemu, ndugu, jamaa na marafiki na watanzania wote kwa ujumla. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

**11. *Mheshimiwa Spika,*** mafanikio yaliyopatikana katika kipindi chote hiki ni kutokana na ushirikiano mzuri miongoni mwa wadau wa Wizara wakiwamo viongozi, watumishi na washirika wa maendeleo. Natambua mchango wao mkubwa wanaoutoa kwa Wizara ambao umeleta matunda ninayojivunia mbele ya Bunge lako Tukufu leo hii.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** niruhusu kwa dhati ya moyo wangu nimshukuru Mheshimiwa Hamis M. Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nimshukuru Bw. Gerson P. Msigwa, Katibu Mkuu; Bw. Methusela S. Ntonda, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na watumishi wote wanaofanya kazi kwa bidii na wanaohakikisha mipango ya Wizara inatekelezwa kama ilivyopangwa. Rai yangu ni kuwa tuendeleze ushirikiano huu.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia, niwashukuru Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ikiwa ni pamoja na mashirika ya kimataifa, mashirikisho, vyama, vilabu na kila mdau kwa nafasi yake katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa kuhakikisha Sekta hizi zinakua na kufanikisha malengo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa sera.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru wapiga kura wangu wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini kwa kuniamini na kunipigia kura nyingi. Pia, kwa kunipatia ushirikiano mkubwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu; na wakati wa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokabili jimbo letu la Arusha. Ushirikiano wenu kwangu, moyo wa uzalendo, na utayari wenu ni nguzo kuu katika kulipatia maendeleo jimbo letu la Arusha Mjini. Naomba wananchi wa Arusha waendelee kuniamini kwani nitaendelea kuwa mtumishi wao ambaye nitawatumikia

kwa uadilifu mkubwa.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara hii ni mhimili kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ambayo kwa maneno mengine naweza kusema ni Wizara yenye nguvu shawishi (***soft power***) ya nchi inayobeba Taifa letu na kulitambulisha kwa Mataifa. Sekta ya habari imekuwa na mchango mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa muhimu zinazowawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha, utamaduni wetu ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Hivyo, kupitia sekta ya utamaduni Serikali imeendelea kujenga uzalendo, kuhifadhi mila na desturi pamoja na maadili ya Mtanzania.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo zimeendelea kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi hususan kwenye ukuaji na mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la Taifa. Mathalani kwa mwaka 2024 sekta za sanaa na burudani ziliongoza kwa kukua kwa asilimia 17.1. Kwa upande wa mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la Taifa, sekta hizi, zilichangia kwa wastani wa asilimia 0.4. Hii inadhihirisha wazi kuwa sekta hizi ni vichocheo vya uchumi hususan kwenye sekta nyingine za kiuchumi kama vile utalii, huduma za malazi na fedha.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2024, shughuli za habari na mawasiliano zilikua kwa asilimia 14.3 ikilinganishwa na

ukuaji wa asilimia 7.6 mwaka 2023. Aidha, mchango wa shughuli za Habari na mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.6 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 1.5 mwaka 2023.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa sekta ya sanaa, imekuwa na nafasi kubwa katika uzalishaji wa ajira hususan kwa vijana. Aidha, wasanii wetu wameendelea kuwa mabalozi wa nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu. Michezo nayo ni kiungo muhimu katika kujenga fahari ya maendeleo ya Taifa letu. Michezo siyo burudani tu, bali pia ni nyenzo ya kuimarisha afya, umoja na mshikamano wa taifa na ni chanzo cha ajira kwa vijana wetu.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa muktadha huo Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa sekta hizi hususan ni michezo inafanya uwekezaji mkubwa unaolenga kuibadili kabisa Tanzania katika ramani ya michezo. Mheshimiwa Rais amewekeza zaidi ya shlingi trilioni 1.2 katika michezo ikiwa ni sehemu ya kuifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa AFCON 2027. Uwekezaji huo upo katika timu za Taifa, uendeshaji wa michezo pamoja na miundombinu ya michezo ikiwemo ujenzi wa viwanja vya mpira wa miguu katika Jiji la Arusha na Dodoma, ujenzi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, ujenzi wa vituo vya michezo na kupumzikia wananchi jijini Dar es Salaam na Dodoma, na ujenzi wa viwanja vidogo (vya mazoezi) kumi na moja (11) ikiwa vitano (5) Arusha na sita (6) Dar es Salaam.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii imezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2025/26 na Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2026/27 aliyoiwasilisha hapa Bungeni tarehe 01 Aprili, 2026; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025 - 2030); Mpango Mkakati wa Wizara (2026/27 - 2030/31); na sera, sheria na miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na maelekezo mbalimbali ya viongozi wakuu wa Serikali.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba yangu imegawanyika katika sehemu saba (7): Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Dira, Dhima, Majukumu, Misingi ya Mwelekeo, na Vipaumbele vya Wizara na taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Sehemu ya Tatu inaelezea Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Kipindi cha Mwaka 2025/26 na Sehemu ya Nne inabainisha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa ili kuzipatia ufumbuzi. Aidha, Sehemu ya Tano ni Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2026/27; Sehemu ya Sita Shukrani; na Sehemu ya Saba ni Hitimisho.

## 2.0 DIRA, DHIMA, MAJUKUMU, MISINGI YA MWELEKEO NA VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Dira ya Wizara ni *"Kuwa na Taifa linalohabarishwa kikamilifu, linaloshamirika kiutamaduni, lenye kazi bora za sanaa na lenye umahiri katika michezo"* na dhima ni ***"****Kuendeleza utambulisho wa Taifa kwa kuwezesha upatikanaji stahiki wa habari, kukuza utamaduni, sanaa na michezo kwa lengo la kuleta maendeleo ya jamii kiuchumi.****"***

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia Dira ya Wizara, majukumu ya msingi ya Wizara ni pamoja na: kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mipango, Miradi na Programu mbalimbali katika Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuendeleza shughuli za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na kusimamia shughuli za filamu na michezo ya kuigiza. Majukumu mengine ni kuimarisha utendaji na Rasilimaliwatu wizarani na kusimamia utendaji wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ambazo ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), na Baraza la Michezo la Taifa (BMT). Vilevile, Wizara inaratibu na kusimamia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika, Bodi ya Ithibati Tanzania na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

Aidha, Wizara inaratibu Kamati ya Maudhui ambayo Kimuundo ipo chini ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza na kuimarisha utendaji kazi, Wizara inaongozwa na misingi mitano (5) ya kimkakati na kimageuzi ambayo ni Kuwafikia Wadau *(Outreach Programmes)*; Mageuzi ya Taasisi *(Institutional Reforms)*; Utawala Bora *(Good Governance)*; Ujenzi wa Miundombinu *(Infrastructure Development)*; na Utafutaji wa Rasilimali *(Resources Mobilization).*

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** chini ya misingi hiyo, katika mwaka 2026/27, Wizara imejipanga kutekeleza maeneo mbalimbali ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na:

(i) Kukamilisha kukarabati, kuboresha, kujenga na kuendelea kutunza miundombinu katika sekta za habari, utamaduni, sanaa na michezo;
(ii) Kukamilisha maandalizi ya Tanzania kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON 2027 yatakayofanyika Juni hadi Julai 2027;
(iii) Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya 74 ya Urembo ya Dunia (Miss World);
(iv) Kukamilisha kutunga na kuhuisha Sera, Sheria, mikakati, miongozo na kanuni mbalimbali katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji katika sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
(v) Kuimarisha na kustawisha kiswahili kikanda na kimataifa;
(vi) Kuimarisha, kuziwezesha na kufanikisha ushiriki

wa timu za Taifa katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa;

(vii) Kuboresha elimu na mafunzo katika tasnia za utamaduni, sanaa na michezo;

(viii) Kuweka na kuboresha mazingira wezeshi na kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

(ix) Kuratibu, kuendesha na kusimamia matamasha, shughuli na matukio makubwa ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** maeneo mengine ni kuziimarisha na kuziongezea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziweze kusimamia na kutekeleza majukumu ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; kuimarisha ushirikiano na Wizara nyingine katika utendaji kazi hususan zile zinazohusika na masuala ya Kazi na Ajira, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Elimu, Afya, Maliasili na Utalii, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwamo Sekta Binafsi katika maendeleo kwa kufadhili na kusukuma mbele gurudumu la Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2025/26

## 3.1 MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA

### 3.1.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi Bilioni Moja na Milioni Thelathini na Sita Elfu (shilingi 1,036,000,000) kutoka kwenye vyanzo sita (6) ambavyo ni mapato yatokanayo na viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru; ada za mafunzo na mitihani kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; vitambulisho vya waandishi wa habari; machapisho ya picha, mabango na majarida; usajili wa magazeti; na ada ya mwaka ya magazeti.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufika mwezi Aprili 2026 shilingi Milioni mia sita tisini na tisa, laki saba na sita elfu, tisini na tatu (shilingi 699,706,093), sawa na asilimia 67.5 ya lengo la mwaka zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu za kutofikia kwa lengo ni pamoja na kupungua kwa matukio katika viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru kutokana na kufungwa kulikotokana na ukarabati unaoendelea katika viwanja hivyo.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza makusanyo ya maduhuli ikiwamo kufanya ukarabati mkubwa wa miundombinu ya viwanja, ili kuwezesha

kuvutia mashabiki wengi zaidi; kuongeza hamasa katika michezo ikiwemo zawadi mbalimbali kwa washindi ili kuhamasisha matokeo mazuri yatakayochochea ushabiki na hatimaye mapato.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Wizara, kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ni shilingi Bilioni Arobaini, Milioni Mia Mbili Tisini na Tano, Mia Moja Tisini na Mbili Elfu (shilingi 40,295,192,000), ambapo hadi mwezi Aprili 2026, shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Ishirini, Sitini na Tatu Elfu na Mia Sita Themanini na Nne (shilingi 17,020,063,684), sawa na asilimia 42 ya lengo zilikuwa zimekusanywa. Miongoni mwa sababu zilizochangia kutofikiwa kwa malengo ni pamoja na baadhi ya taasisi kushindwa kulipa kwa wakati huduma za matangazo zilizotolewa na taasisi zilizo chini ya Wizara ikiwemo TSN na TBC. Kwa upande wa vyuo, moja ya sababu ni wanavyuo kutokulipa ada kwa wakati kutokana na changamoto mbalimbali.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi inaendelea kutoa elimu kwa wadau na kufanya kampeni mbalimbali ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo. Kampeni hizo ni pamoja na kuhamasisha usajili na kufuata taratibu za uzalishaji na usambazaji wa kazi za sanaa; kuongeza kasi ya kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa taasisi; utekelezaji wa mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218 na kuhamasisha wanavyuo kulipa ada kwa wakati.

### 3.1.2 Bajeti ya Matumizi ya Wizara na Mtiririko wa Fedha

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara iliidhinishiwa bajeti yenye jumla ya shilingi Bilioni Mia Tano Kumi na Tisa, Milioni Mia Sita Sitini, na Sabini na Tatu Elfu (shilingi 519,660,073,000). Kati ya fedha hizo, Mishahara ni shilingi Bilioni Thelathini na Tatu, Milioni Mia Nne na Tatu, Mia Nane Kumi na Tatu Elfu (shilingi 33,403,813,000), Matumizi Mengineyo ni shilingi Bilioni Ishirini na Nane, na Milioni Sitini na Tano, Mia Nne Sabini na Mbili Elfu (shilingi 28,065,472,000) na Miradi ya Maendeleo ni shilingi Bilioni Mia Nne Hamsini na Nane, Milioni Mia Moja Tisini, Mia Saba Themanini na Nane Elfu (Shilingi 458,190,788,000).

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Aprili 2026, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi Bilioni Mia Tatu Hamsini na Mbili, Milioni Mia Tisa Arobaini na Mbili, Mia Nne Hamsini na Nne Elfu, Mia Nne Sabini na Mbili na Senti Tisini na Saba (shilingi 352,942,454,472.97) sawa na asilimia 67.9 ya bajeti yote. Kati ya fedha zilizopokelewa, Mishahara ilikuwa shilingi Bilioni Ishirini na Saba, Milioni Mia Sita Themanini na Nne, Mia Tano Arobaini na Nne Elfu, Mia Moja Hamsini na Nane na Senti Tisini (shilingi 27,684,544,158.90) sawa na asilimia 82.9 ya bajeti ya Mishahara; Matumizi Mengineyo ni shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tisa Ishirini na Tano, Mia Tano Sitini na Sita Elfu, Mia Mbili Thelathini na Tatu na Senti Themanini na Moja (shilingi 20,925,566,233.81) sawa

na asilimia 74.6 ya bajeti ya Matumizi Mengineyo; na Miradi ya Maendeleo ni shilingi Bilioni Mia Tatu na Nne, Milioni Mia Tatu Thelathini na Mbili, Mia Tatu Arobaini na Nne Elfu, Themanini na Senti Ishirini na Sita (shilingi 304,332,344,080.26) sawa na asilimia 66.4 ya bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26

### 3.2.1 SEKTA YA HABARI

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu ya Sekta ya Habari ni pamoja na kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Wizara kupitia sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

#### 3.2.1.1 IDARA YA HABARI

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003; Sheria ya Huduma za Habari Sura ya 229 na kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa sera, mikakati, programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali ya kuwaletea wananchi maendeleo. Wizara kupitia sekta hii imetekeleza majukumu yafuatayo:

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya habari imeendelea kuwa kichocheo muhimu cha ukuaji wa uchumi nchini

kwa kuibua, kukuza vipaji, ajira na kuhakikisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati. Kwa kutambua umuhimu huo, Wizara kupitia Idara ya Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali imeendelea kuisemea Serikali kwa kutoa taarifa mbalimbali kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Hatua hii imelenga kuwapatia wananchi taarifa sahihi na za uhakika kuhusu mafanikio yanayopatikana, pamoja na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha huduma za kijamii na kukuza uchumi wa Taifa.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia jitihada hizi, wananchi wameendelea kufahamishwa kuhusu juhudi za Serikali katika kukuza uchumi na kuimarisha uwekezaji, hususan katika miundombinu ya usafiri ikiwemo reli, barabara, maji na anga. Maboresho haya yameiweka Tanzania katika nafasi nzuri ya ushindani, kikanda na kimataifa. Baadhi ya miradi ambayo imekuwa ikitolewa taarifa kwa umma ni pamoja na maendeleo ya ujenzi na uendeshaji wa huduma za treni ya kisasa ya SGR; ukarabati mkubwa wa reli ya TAZARA; pamoja na miradi ya kuboresha na kuongeza uwezo wa viwanja vya ndege ili kuhudumia abiria na mizigo kwa ufanisi zaidi. Aidha, Serikali imeendelea kuwekeza katika upanuzi na uboreshaji wa bandari za Dar es Salaam, Mwanza, Tanga, Mtwara, Bukoba na Kigoma, hatua inayochochea biashara na kukuza uchumi wa Taifa.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara imeisemea Serikali kuhusu kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa daraja la JP Magufuli (Kigongo – Busisi) mkoani Mwanza

ambalo limekua mkombozi kwa wananchi na wafanyabiashara wa mikoa ya kanda ya ziwa na nchi jirani. Aidha, imeisemea Serikali kuhusu kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza; miradi ya ukarabati wa vivuko na uimarishaji wa huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika Ziwa Viktoria, Tanganyika, Nyasa na Bahari ya Hindi; mradi wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia dawa ya Bohari ya Dawa (MSD) Kanda ya Kati Dodoma; juhudi za Serikali kukuza sekta ya utalii; na taarifa kuhusu kuimarika kwa uzalishaji wa umeme kulikochangiwa na ufanisi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere (JNHPP).

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** mbali na Msemaji Mkuu wa Serikali kuwaeleza wananchi mafanikio ya utekelezaji wa miradi hiyo, ameendelea kutoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayoendelea nchini. Miongoni mwa masuala hayo yanahusu maandalizi ya Tanzania kwa kushirikiana na Kenya na Uganda kuwa mwenyeji wa Mashindano ya AFCON 2027 ambapo Serikali chini ya uongozi imara wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo katika jiji la Dar es salaam na Arusha. Aidha, Wizara kupitia Msemaji Mkuu wa Serikali kwa nyakati tofauti imekuwa ikiwaeleza wananchi kuhusu mpango wa Serikali wa kuendelea kuimarisha sekta ya anga kwa kununua ndege mpya kupitia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL); na manufaa ya mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda kwenda Tanga.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mengine ni ujenzi wa soko kuu Mwanza ambalo sasa linatumiwa na wafanyabiashara; Wizara kuhamia na kuanza kutumia majengo mapya katika Mji wa Serikali Mtumba; kuanza kwa mradi wa ujenzi wa matanki matano yatakayosambaza maji kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza; kukamilika kwa Mradi wa Shule ya Wasichana Shelukindo mkoani Tanga na mradi wa ujenzi wa daraja jipya la Pangani mkoani Tanga. Vilevile taarifa zimetolewa kuhusu uboreshaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi nchini katika ngazi ya Hospitali za Rufaa na Kanda zikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamin Mkapa, na Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI).

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile Wizara imehabarisha umma kuhusu uwekezaji maalumu wenye kulenga kukuza na kutoa ajira kwa vijana kupitia mfumo wa vijana na kukuza viwanda kupitia kongani maalumu za uwekezaji (TISEZA) ambao umerahisisha taratibu, kupunguza urasimu, na kuvutia miradi itakayoongeza ajira na ujuzi kwa vijana. Mwelekeo huu unaenda sambamba na hatua za Serikali za kuendeleza programu za uwekezaji zinazoweka vijana katikati, ikiwemo uanzishaji wa mikakati ya vijana kumiliki na kuendesha miradi ya uzalishaji.

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, hatua hizi zimeendelea kusaidia kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu utekelezaji wa miradi ya kimkakati, sambamba na kuimarisha uwazi na mawasiliano kati ya Serikali na

umma. Wizara imeendelea kuratibu ziara za waandishi wa habari kwenda kutembelea na kujionea miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita. Kupitia ziara hizo, waandishi wa habari wamepata fursa ya kuona kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo, hivyo kupata uelewa wa kutosha unaowawezesha kutoa taarifa sahihi na uhakika kwa ajili ya kujenga uelewa kwa umma, kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kujenga uaminifu kwa umma na kuzuia kusambaa kwa taarifa zisizo sahihi ambazo zimekua na athari hasi kwenye jamii yetu, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO imeendelea kuratibu na kuandaa mikutano ya Msemaji Mkuu wa Serikali na vyombo vya habari kwa lengo la kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali ya Awamu ya Sita. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imefanikiwa kuandaa mikutano 22. Kupitia mikutano hii, wizara kupitia Idara ya Habari na Msemaji Mkuu imetoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yenye maslahi kwa umma, sambamba na kuwakumbusha waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi kuzingatia maadili ya taaluma ya uandishi wa habari na utangazaji kwa kuhakikisha wanathibitisha taarifa kabla ya kuzichapisha au kuzitangaza kupitia vyombo vyao vya habari na mitandao ya kijamii ili kuepuka kutoa taarifa zisizo rasmi zinazoweza kuchochea taharuki na kuvuruga amani katika jamii.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, habari za uzushi zisipodhibitiwa zinaweza kuleta madhara makubwa kwenye jamii ikiwemo kuharibu heshima ya watu kwenye jamii, kupotosha ufanyaji maamuzi, kuharibu uchumi na biashara na kuchochea unyanyasaji mtandaoni. Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari kwa nyakati tofauti imekua ikihimiza wananchi na wadau wa sekta ya habari kuepuka kusambaza habari ambazo hazijathibitishwa. Pia, imekua ikishirikiana na taasisi nyingine za Serikali likiwemo Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kutoa elimu kwa wadau wa tasnia ya habari na wananchi kwa ujumla namna ya kujilinda dhidi ya taarifa potofu, uzushi, uhalifu na ulaghai mitandaoni na kuwahimiza wananchi kuongeza umakini katika matumizi ya mitandao, kuepuka kusambaza taarifa hizo, na kuzifuta pindi wanapozipokea kupitia mitandao ya kijamii.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kukabiliana na wimbi la taarifa za upotoshaji na ongezeko la mitandao isiyo rasmi na matumizi mabaya ya akili unde, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO na Msemaji Mkuu wa Serikali imeratibu na kuendesha zoezi la urasimishaji na uthibitisho wa akaunti za mitandao ya kijamii za Wizara, mikoa, taasisi, wakala, Halmashauri na mashirika ya Serikali. Lengo la zoezi hili ni kulinda usalama wa taarifa na kuimarisha utambulisho rasmi wa taasisi za Serikali ambapo kupitia zoezi hilo, jumla ya akaunti 412 za mtandao wa Instagram; 200 za mtandao wa Facebook; na zaidi ya 300 za mtandao wa X zamani Twitter zimethibitishwa.

Hatua hii imesaidia kulinda taswira na kuongeza uaminifu wa taarifa zinazotolewa na Serikali kupitia majukwaa hayo. Kwa ujumla, juhudi hizi zinaonesha dhamira thabiti ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kutoka vyanzo sahihi na kwa wakati, huku ikiendelea kulinda maslahi ya Taifa.

**46.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata taarifa sahihi kuhusu mambo mbalimbali yanayofanywa na Serikali, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO, imeratibu mikutano ya taasisi za Serikali kuzungumza na waandishi wa habari ambapo katika kipindi cha Julai hadi Aprili, 2026, Wizara imeratibu na kufanikisha mikutano 30. Aidha, Wizara iliratibu mikutano 15 ya Waheshimiwa Mawaziri kuelezea utekelezaji wa majukumu na utekelezaji wa ahadi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha siku 100 za muhula wa pili wa Serikali ya Awamu ya Sita. Wizara zilizoshiriki katika mikutano hiyo ni pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalumu; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana; Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; pamoja na Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji. Wizara nyingine ni Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Maji; Wizara ya Madini; Wizara ya Uchukuzi; na Wizara ya Afya. Hatua hizi zimeendelea kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na wananchi, pamoja na kuhakikisha umma unapata taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa sera, programu na

miradi ya maendeleo ya Taifa.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu na kufanya tathmini ya utoaji wa taarifa za Serikali kwa umma ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Kutokana na tathmini hiyo, Wizara iliitisha Kikao Kazi cha Wakuu wa Idara na Vitengo vya Mawasiliano Serikalini wa Wizara kilichofanyika tarehe 11 Desemba, 2025. Katika kikao kazi hicho, jumla ya Wakuu wa Idara na Vitengo vya Mawasiliano Serikalini 520 walipatiwa mafunzo kuhusu mikakati mbalimbali ya kuimarisha utoaji wa taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu vyombo na waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na ziara za viongozi, kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu shughuli muhimu za Serikali na Taifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026, waandishi wa habari waliratibiwa kushiriki katika matukio mbalimbali ikiwemo Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba 2025; uzinduzi wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa; pamoja na uzinduzi wa Kituo cha Biashara na Usafirishaji Ubungo. Aidha, waandishi hao waliratibiwa katika ziara za Mheshimiwa Rais katika mikoa ya Simiyu, Mara na Mwanza, ambapo alizungumza na wananchi na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Daraja la JP Magufuli (Kigongo – Busisi). Vilevile, Wizara iliratibu vyombo vya

habari katika matukio mengine muhimu ya kitaifa, yakiwemo Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani wa mwaka 2025, mikutano na shughuli mbalimbali za Serikali.

**49.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuratibu waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, ili kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi na za uhakika na kwa wakati kuhusu shughuli za maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, waandishi wa habari waliratibiwa kushiriki katika matukio makubwa mbalimbali ikiwemo; Mkutano Mkuu wa Mahakimu na Majaji; vikao vya Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mkutano wa 16 wa Wataalamu wa Bodi ya Ununuzi na Ugavi (PSTPB); Kongamano la Anwani za Makazi na Maonesho ya Kiteknolojia ya Huduma za Posta; Maadhimisho ya Siku ya Sheria Nchini; Hafla ya kufungua Soko la Kimataifa la Kariakoo; na Mashindano ya CHAN 2024. Matukio haya yameongeza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa kikamilifu kuhusu Serikali yao, Wizara imechapisha nakala 20,000 za Jarida la NCHI YETU linalohusu mafanikio ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Sita. Jarida hili lina taarifa mbalimbali za miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa na Serikali. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Habari-MAELEZO inaendelea kutoa kila siku jarida hili mtandaoni.

#### 3.2.1.2 Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

**51.** ***Mheshimiwa Spika***, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) linasimamiwa kupitia Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania, Sura 239. Majukumu ya TBC ni kutoa huduma ya utangazaji kwa kuhabarisha, kuelimisha, kuburudisha na kutafakarisha. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, Shirika limetekeleza majukumu mbalimbali ambayo yanafafanuliwa ifuatavyo:

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TBC imeendelea na utekelezaji wa mradi wa Upanuzi wa Usikivu kwa kujenga vituo vya kurusha matangazo ya redio, masafa ya FM katika Wilaya 18 nchini. Mradi huu uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Ujenzi unaendelea katika Wilaya za Kalambo (Rukwa), Liwale (Lindi), Rufiji (Pwani), Biharamulo (Kagera), Urambo na Igunga (Tabora), Karatu (Manyara), Kilolo (Iringa), Ulanga (Morogoro), Iramba (Singida) na Ngara (Kagera). Kazi zilizokamilika ni: ujenzi wa minara, ununuzi na ufungaji wa mitambo ya umeme, ujenzi wa vyumba vya kuhifadhi mitambo na ununuzi wa mitambo ya kurusha matangazo ya redio (transmitter). Wakati huo huo, TBC imepokea mitambo ya masafa ya FM kwa ajili ya Wilaya za Tanganyika (Katavi), Gairo (Morogoro), Hanang (Manyara), Siha (Kilimanjaro) na Mpwapwa (Dodoma) ambapo tayari hatua za awali za maandalizi ya ufungaji wa mitambo zinaendelea.

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC inashirikiana na wadua wengine wa maendeleo ya mawasiliano na teknolojia ya habari ikiwemo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambapo mradi wa upanuzi wa usikivu unatekelezwa katika Wilaya kumi (10) za Kyerwa (Kagera), Chunya (Mbeya), Kiteto (Manyara), Chemba (Dodoma) na Mkinga (Tanga). Kazi ya ujenzi wa majengo ya kuhifadhi mitambo inaendelea na imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji. Maeneo mengine ambayo mradi unatekelezwa ni katika maeneo ya: Bukombe (Geita), Usangi (Kilimanjaro), Rombo (Kilimanjaro), Buhigwe (Kigoma) na Tunduru (Ruvuma) ambapo kazi ya ununuzi wa mitambo ya kurusha matangazo inaendelea.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatekeleza mradi wa upanuzi wa usikivu katika Wilaya 15 na kazi ya ufungaji wa mitambo ya kurushia matangazo imekamilika kwenye vituo vya Arumeru (Arusha), Meatu (Simiyu), Sengerema (Mwanza), Kilosa (Morogoro), Mpwapwa (Dodoma) na Momba (Songwe). Aidha, ujenzi wa majengo ya kuhifadhi mitambo inaendelea kwenye halmashauri za Iringa Vijijini (Iringa), Lushoto (Tanga), Simanjiro (Manyara), Mpimbwe (Rukwa), Nyang'hwale (Geita), Kilombero (Morogoro), Nkasi Kusini (Rukwa), Itigi (Singida) na Mkalama (Singida).

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hii ni hatua muhimu ya kupeleka mawasiliano ya redio kwa wananchi wote hususan waishio maeneo ya mipakani na yale yenye

usikivu hafifu. Hadi Aprili 2026, usikivu wa redio za TBC umefikia Wilaya zote 139 na kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivi kutaongeza usikivu hadi asilimia 98 na hivyo kuondoa changamoto ya usikivu kwenye maeneo yenye usikivu hafifu na yasiyokuwa na usikivu kabisa. Mkakati wa Serikali ni kufikisha Usikivu wa redio za TBC kwenye Halmashauri zote 184 nchi nzima baada ya lengo la usikivu katika Wilaya zote nchini kufikiwa.

**56.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TBC imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha umma wa Watanzania kwa weledi. Serikali imewezesha upatikanaji wa huduma ya utangazaji muda wote kwa kulipia masafa ya Satelaiti, simu na intaneti kwa ajili ya kurusha matangazo mbashara ya redio na televisheni. Aidha, Serikali imewezesha upatikanaji wa huduma ya utangazaji kwa kuboresha masafa ya satelaiti kutoka uwezo wa 3MHZ hadi 7MHZ ili kukidhi mahitaji yanayotokana na ongezeko la chaneli za televisheni (TBC1, $TBC_2$ na Tanzania Safari Chaneli), idhaa za redio (TBC taifa, BONGO FM, TBC International na redio za Kanda, redio jamii Arusha na Dodoma) na TBC Mtandaoni. Uwezeshaji huu umekuwa na tija kubwa kwa kuongeza uwezo wa TBC kurusha matangazo mbashara yenye manufaa kwa umma ambapo Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 TBC ilirusha jumla ya matangazo mbashara 403 yenye thamani ya Shilingi 5,565,590,825 yaliyohusu ziara na matukio yanayohusu viongozi wa kitaifa.

**57.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TBC imeboresha na kuimarisha chaneli zake za kimkakati ili kukidhi mahitaji ya wakati na kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya habari na Utangazaji. Serikali imewekeza jumla ya shilingi 1,317,523,580 kwa ajili ya studio za TBC kwa kufunga mifumo mipya ya kisasa ya kidijiti, kununua mitambo na vifaa vipya vya utangazaji na hivyo kuongeza ubora wa picha na sauti. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, TBC ilinunua kamera za kisasa 15, *wireless microphone* 38, vifaa kwa ajili ya urushaji wa matangazo mbashara ya televisheni (LiveU-6), vifaa vya kurushia matangazo ya mbashara ya redio (Quantum- 1), vifaa vya kuchanganya sauti na picha za video (video mixer – 3) na gari moja (1) aina ya Coaster na gari moja la kurusha matangazo mbashara ya Televisheni (OB-Van) lenye kamera sita lililogharimu Shilingi 3,800,000,000 kwa ajili ya shughuli za utangazaji. Aidha, TBC imefanya maboresho katika studio za BONGOFM kwa kuzihamishia TBC1 - Mikocheni kutoka barabara ya Nyerere. Maboresho mengine yaliyofanyika ni katika studio za TBC Zanzibar, Dodoma na TBC Mtandao. Fauka ya hayo, TBC imefunga mfumo wa kuchambua na kuchakata takwimu za uchumi na biashara - TBC Arc na kufunga mfumo maalumu wa AR/VR kwa ajili ya kuboresha muonekano wa graphics maalum katika muundo wa 3D.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa TBC inawafikiwa vijana kwenye majukwaa ya mtandaoni hasa wanafuatilia kwenye majukwaa ya mtandaoni maboresho makubwa ya kimaudhui na

mifumo yamefanyika kupitia BongoFM, TBC2 na TBC Mtandao. Chaneli hizi za kimkakati zimekuwa chachu kwa kuongeza watazamaji, wafuatiliaji na wasikilizaji hivyo kukidhi malengo ya kuanzishwa kwake. Hadi mwezi Aprili 2026 BongoFM ina wafuatiliaji *475,000* kwenye mtandao wa *Instagram*, watazamaji wa machapisho kwenye kurasa ya *YouTube* wamefika *19,239,386.* Kwa upande wa TBCDigita inawafuatiliaji *2,200,000* katika ukurasa wa *Instagram na* watazamaji wa machapisho *61,055,545* kwenye ukurasa wa *YouTube.* Serikali kupitia TBC itaendelea kuwekeza katika uandaaji wa maudhui hasa ya mtandaoni kwenye chaneli zake za vijana.

**59. *Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TBC imeendelea kuboresha uandaaji wa vipindi vya redio, televisheni na TBC Mtandaoni vinavyoelimisha na kuhabarisha umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali pamoja na utekelezaji wa shughuli za viongozi wakuu wa Serikali. Katika kipindi cha 2025/26, TBC imeandaa vipindi vya redio na televisheni vyenye maudhui mbalimbali yenye lengo la kuelimisha umma wa watanzania: Uzalendo vipindi 1,920 (baadhi ya vipindi vyenye maudhui haya ni pamoja na *Mada Kuu*, *Mizani*, *Focus on this Week na Tanzania Today)*, Afya 415, uchumi na Biashara 601, Elimu 132, utunzaji wa mazingira 112, malezi ya watoto 130, mchango wa vijana katika kukuza uchumi 982 na sheria 34. Vipindi vingine vinahusu haki na umuhimu wa amani vipindi 617 (kipindi cha *Sisi ni Tanzania*) pamoja na masuala yahusuyo upatikanaji wa fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa makundi ya watu wenye ulemavu na

wanawake vipindi 77 (Kipindi cha *Wape nafasi*). Aidha, kupitia idhaa ya Bongo FM vipindi vikivyoandaliwa ni pamoja na: *Flyover, Bao la Asubuhi, Kijora na Power Bank.* Kwa upande wa TBC2 vipindi vilivyoandaliwa ni *2DJ Night, Kibajaji on Point, JABA na Binti bora.* Fauka ya hayo, TBC imeendelea kutekeleza mikakati ya kukuza lugha adhimu ya Kiswahili kwa kuwa Balozi mzuri Duniani kote kupitia kipindi cha *Lulu za Kiswahili.* Mkakati wa TBC ni kuhakikisha inaandaa vipindi vya redio, televisheni na mitandao ya kijamii vitakavyowawezesha Watanzania kuifahamu vizuri Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutangaza Utalii wa nchi yetu na kuhakikisha Sekta ya Utalii inakua kwa kasi kuelekea Utekelezaji wa Dira 2050, TBC kupitia chaneli yake ya Tanzania Safari ambayo ni mahsusi kwa ajili ya kutangaza fursa za utalii na utajiri wa maliasili za nchi yetu imewezesha kuandaa maudhui na kutafsiri na kurusha jumla ya vipindi 1,125 katika lugha tano (5) za kimataifa ambazo ni Kireno, Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa na Kichina. Matumizi ya lugha za Kimataifa yamewezesha kuongezeka kwa mawanda ya watazamaji na wafuatiliaji duniani kote na hivyo kufikia malengo ya kitaifa katika kuongeza idadi ya watalii nchini. Aidha, maudhui ya chaneli hii yanapatikana mtandaoni kupitia tovuti ya *www.safarichannel.go.tz* na katika mtandao wa *Youtube* ambapo machapisho yametazamwa na watu 729,471 na wafuatiliaji 85,100 kwenye ukurasa wa mtandao wa Instagram.

**61.** ***Mheshimiwa Spika***, tarehe 2 Septemba 2022, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa mjini Bagamoyo wakati wa maandalizi ya filamu ya Tanzania '*The Royal Tour*", alielekeza Tanzania National Parks Authority (TANAPA) kuitangaza njia ya utumwa kama kivutio cha utalii. Kufuatia agizo hilo, wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na TANAPA walifanya utafiti na kuwasilisha ripoti iliyobainisha vivutio mbalimbali pamoja na kupendekeza mikakati ya kuitangaza njia hiyo kupitia vyombo vya habari. Katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Wizara kupitia TBC inashiriki zoezi la utambuzi wa njia ya misafara ya utumwa na wapagazi na kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko katika njia hii kupitia Kampeni ya *Slave Caravan*.

**62.** ***Mheshimiwa Spika***, kampeni ya *Slave Caravan* inahusisha utangazaji wa njia hii na vivutio ambavyo, isivyo bahati, havijulikani kwa Watanzania na wageni wanaotembelea Tanzania licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa historia. Aidha, utangazaji wa njia hii unakwenda sambamba na kuhifadhi kumbukumbu za wazee na kuandaa makala mbalimbali za kumbukumbu hizo katika jamii ambazo njia hii imepita kutoka Zanzibar hadi Bara (Ujiji – Kigoma) ambapo tayari kampeni imebaini vituo 14 vitakavyotumika kama sehemu ya kuhifadhi kumbukumbu. Kuhifadhi kumbukumbu za wazee wanaofahamu maeneo mbalimbali ya njia hii kutasaidia kuhifadhi urithi huu

muhimu katika historia ya Tanzania kwa kuhifadhi maelezo kuhusu watumwa, utumwa, masulia na maisha baada ya kukomeshwa kwa utumwa. Hatua hii inalenga kukuza utalii wa kiutamaduni na kihistoria, kuongeza idadi ya watalii wa ndani na nje ya nchi, na kuchochea ukuaji wa uchumi. Njia hii, inayotarajiwa kuvutia wageni kuanzia Zanzibar, Bagamoyo hadi Ujiji, pia itasaidia kuhifadhi na kutangaza urithi wa taifa kwa vizazi vijavyo.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC imeanzisha kampeni maalumu zenye lengo la kuhakikisha kunakuwepo na uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kupunguza madhara yanayotokana na uvunaji wa miti kwa ajili ya kutumika kama nishati ya kupikia pamoja na athari za afya zinazotokana na moshi. Jukumu hili linatekelezwa kupitia kampeni ya "Pika Kijanja". TBC kupitia idhaa yake ya redio ya BongoFM imeendesha matamasha manne (4) na makongamano (2) kwa lengo la kuelimisha na kuhamasisha matumizi ya nishati safi katika maeneo mbalimbali nchini. Baadhi ya maeneo yaliyofikiwa na kampeni hii kwa kupitia matamasha na makongamano ni mikoa ya Dar es Salaam, Lindi (Ruangwa) na Zanzibar (Kizimkazi). Katika nyakati zote makundi ya watu mbalimbali wakiwemo *mamalishe* na *babalishe* wameshiriki na kugawiwa mitungi ya gesi kwa ajili ya kutumika kama nishati mbadala. Hadi Aprili 2026, zaidi ya mamalishe na babalishe 9,000 walishiriki makongamano na matamasha na zaidi ya mitungi ya gesi 5,000 ilitolewa bure.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za uhifadhi wa mazingira na ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, Wizara kupitia TBC kwenye kipindi cha JAMBO TANZANIA imeendelea kuendesha na kusimamia kampeni ya upandaji miti nchi nzima inayofahamika kwa jina la **"27 ya Kijani"** inayofanyika kila **tarehe 27** ya kila mwezi. Kampeni hii ilizinduliwa mwezi Januari mwaka 2023. Tarehe 27 Januari, 2026 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliiongoza timu ya TBC na wana mazingira wengine nchini kote kwa kupanda miti katika kumbukizi ya siku yake ya kuzaliwa hafla iliyofanyika Kizimkazi, Wilaya ya Kusini Unguja ambapo jumla ya miti 169,310 ilipandwa siku hiyo katika mikoa yote nchini. Hadi Aprili, 2026, zaidi ya miti 10,000,000 imepandwa maeneo mbalimbali nchini tangu kuasisiwa kwa kampeni hiyo.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TBC inaendesha kampeni mahususi kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu utunzaji wa mazingira inayojulikana kwa **Jicho la Mpita Njia.** Kampeni hii inarushwa kupitia kipindi cha ARIDHIO, ambapo wanahabari wa TBC hupita katika maeneo yaliyokithiri kwa uchafu na hatimaye kutafuta suluhisho la kutatua changamoto hiyo. Kipindi hiki kimekuwa na matokeo chanya kwa maeneo yote ambayo waandishi wa TBC wamefanikiwa kufika. Hadi Aprili, 2026 TBC imefanikiwa kufika Zanzibar na maeneo 18 ya mikoa ya Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Tanga, Njombe, Simiyu, Songwe, Manyara, Mtwara, Mara, Singida, Geita na Morogoro na kufanikiwa kuandaa makala zaidi ya 200 zinazochochea usafi na

utunzaji wa mazingira.

**66.** ***Mheshnimiwa Spika,*** katika kutekeleza azma ya Serikali kuhamia Makao Makuu ya nchi jijini Dodoma, Wizara kupitia TBC imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya TBC jijini Dodoma eneo la Vikonje. Awamu ya Kwanza ya Ujenzi inatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi 54,204,499,116.46 ambapo hadi mwezi Aprili 2026, kiasi cha shilingi 19,592,179,456.58 kimepokelewa kwa ajili ya malipo ya Mkandarasi na Mshauri elekezi wa ujenzi wa jengo la utawala, studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Ujenzi umefikia asilimia 52 ambapo kazi zilizotekelezwa ni kuanza ufungaji wa mifumo ya muhimu ya utangazaji kwenye studio za redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Kukamilika kwa mradi huu mkubwa ni hatua ya wazi katika kuipa heshima tasnia ya habari nchini na historia ya Tanzania katika kuhabarisha umma toka enzi za Redio Tanzania Dar es Salaam - RTD kwa uwepo wa majengo, studio na vifaa vya kisasa vya utangazaji. Mradi huu awamu ya kwanza unatarajiwa kukamilika Juni, 2026 kulingana na mkataba.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** TBC kikiwa ni chombo cha utangazaji cha umma kimeendelea kuwa na jukumu la kuimarisha mahusiano na vyombo vingine vya kimataifa kwa kuingia makubaliano (MoU) ya kubadilishana maudhui na vipindi, mafunzo kwa watumishi na kuitangaza lugha adhimu ya Kiswahili kupitia vyombo vya habari vya mataifa hayo. Vyombo vya habari ambavyo ni washirika na TBC ni pamoja na Voice of

Nigeria (VoN), RT ya Russia, Southern Africa Broadcasting Association (SABA), NHK ya Japan na African Union of Broadcasting (AUB). Washirika hawa wamekuwa ni chachu katika kuitangaza Tanzania kimataifa ikiwa ni pamoja na kuongeza ushawishi wa Tanzania kupitia maudhui mbalimbali yaliyotafsiriwa kwa Lugha adhimu ya Kiswahili. Kwa upande mwingine TBC imekuwa ni mlezi wa vyombo vya habari ambavyo vinamilikiwa na Halmashauri mbalimbali nchini kwa kutoa mafunzo kwa watendaji katika kuwajengea uwezo kutokana na ukuaji wa haraka wa tasnia ya habari na utangazaji. TBC imeimarisha chaneli ya matangazo yake ya taarifa ya habari kwa lugha ya kiingereza (English News) ili kuitangaza nchi kimataifa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika***, TBC inajivunia mafanikio katika nyanja zote za kihabari, mifumo, miundombinu ya utangazaji na maslahi ya watumishi yaliyoboreshwa. Matokeo ya maboresho haya ni kuongezeka kwa ubunifu kihabari hivyo kuwezesha TBC kupata tuzo mbalimbali za kihabari kitaifa na Kimataifa. Katika kipindi cha mwaka 2025/26 TBC kama taasisi, wanahabari, watozi na watumishi wake wameweza kupata tuzo mbalimbali wakiwemo Bw. D'jaro Deus Arungu kupitia kipindi chake cha Papaso (*ZIKOMO AFRICA AND CARIBBEAN AWARDS 2025*) kipengele cha *Media Legend of the Year*, 2025 Bw. Sam Clinton na Bi.Caroline Malewo walipata Tuzo ya *AFRICA MEDIA AWARD*, 2025 kwenye Kipengele cha *Best Outstanding Interview of the Year* kupitia kipindi cha *Focus on this week* kinachotangazwa na chaneli ya TBC1. Fauka ya hayo, TBC ilipata tuzo za CHOMBO BORA CHA

MAWASILIANO KWA UMMA NA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI, 2025. Tuzo hiyo ilitolewa na Taasisi ya Tuzo za Ubunifu wa Sekta ya Umma; KIPINDI BORA CHA ELIMU KWA WAJASILIAMALI WADOGO kupitia kipindi cha *Ngazi* kinachorushwa na Chaneli ya TBC1, tuzo iliyotolewa na Umoja wa Wanawake Wajasiliamali Tanzania. Kupatikana kwa tuzo hizi kunadhihirisha wazi kuwa TBC imekuwa na mchango mkubwa katika kutekeleza dhima yake ya kuelimisha, kuhabarisha, kuburudisha na kutafakarisha kwa kuzingatia ubunifu na misingi ya weledi kwenye taaluma ya uandishi wa habari.

**69. *Mheshimiwa Spika,*** Chaneli za TBC1, TBC2 na Tanzania Safari Chaneli kwa kupitia mtandao wa televisheni wa *Canal+International* zimeweza kufikia nchi 46 zinazoongea *Kingereza, Kifaransa na Kireno*. Nchi hizo ni pamoja na Angola, Benin, Burkina Faso, Botswana, Burundi, Kameruni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Kongo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Djibouti, Equatorial Guinea, Ethiopia, Eritrea, Eswatini, Gabon, Gambia, Ghana, Green Cape, Guinea Conakry, Guinea Bissau, Ivory Coast, Kenya, Liberia, Lesotho, Mali, Malawi, Mauritania, Mozambique, Namibia, Niger, Nigeria, Rwanda, Sao Tome, Senegal, Sierra Leone, Somalia, Sudani, Afrika Kusini, Sudani Kusini, Uganda, Tanzania, Togo, Zambia, Zimbabwe. Aidha, kupitia AZAM nchi saba (7) zimefikiwa ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Malawi na Zimbambwe.

### 3.2.1.3 Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN)

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ilianzishwa kwa tamko la Rais la mwaka 1970. Aidha, TSN inatekeleza majukumu chini ya sheria ya Makampuni Sura ya 212 ikiwa na jukumu la kuhabarisha na kuelimisha umma kwa kuchapa na kusambaza magazeti ya Serikali ambayo ni *Daily News*, *Sunday News*, HabariLEO na SpotiLEO. Vilevile, TSN huchapisha habari kupitia nyanja za kidigiti; tovuti na mitandao ya kijamii kwa lugha za Kiswahili na Kiingereza ikiwamo *Facebook, Instagram na Youtube*. Katika kipindi cha mwaka 2025/26, Wizara kupitia TSN imetekeleza majukumu yafuatayo:

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TSN imeendelea kutekeleza mradi wa ufungaji mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji kwa kujenga jengo la kiwanda cha uchapaji na kununua mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji. Hatua ya ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji imefikia asilimia 83.1 ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na uwekaji wa vigae, uwekaji wa milango na madirisha, ufungaji wa mifumo ya maji, umeme, TEHAMA, utambuzi na udhibiti wa moto na kupaka rangi jengo. Ununuzi wa mitambo mipya ya kisasa ya uchapaji umefikia asilimia 85. Mitambo iliyonunuliwa ni pamoja na *Hybrid Web Offset Press, Computer to Plate (CTP) Machine, Compressor (Large Size) 38kw, Guillotine/Cutting Machine, Six Color Fed Machine, Gatherer, Stitcher na Knife Trimmer* yenye thamani ya Shilingi 17,821,368,600.



*Pichani ni wajumbe wa Kamati ya ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo wakiwa wameambatana na Waziri Mheshimiwa Paul Chistian Makonda (Mb.), wakipokea maelezo kutoka kwa mshauri elekezi juu ya ujenzi wa jengo la Kiwanda cha uchapaji mnamo tarehe 15 Machi, 2026 jijini Dar es Salaam.*




*Picha ya jengo la Kiwanda cha uchapaji litakavyokuwa likionekana kwa nje baada ya kukamilika kujengwa*

**72. *Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TSN imeendelea kuboresha uandaaji na uchapaji wa maudhui kupitia Magazeti, Chaneli ya mtandaoni na majukwaa ya mitandao ya kijamii. TSN imeimarisha uandaaji wa maudhui ya kimkakati yaliyolenga kujenga na kuendeleza taswira chanya ya nchi na Serikali, ndani na nje ya mipaka ya Taifa. Maudhui hayo yalijikita katika kuhabarisha mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hadi Aprili 2026, TSN imeandaa na kuchapisha jumla ya makala 2,973 za kimkakati, ambapo makala 178 za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, makala 140 za Bunge la Wawakilishi Zanzibar, makala 144 za utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo, makala 656 za elimu ya mpiga kura na uraia, makala 180 za maboresho ya huduma za kijamii, makala 288 za ukuaji wa uchumi, na makala 1,387 za elimu juu ya sera, mikakati na miongozo na nafasi ya Tanzania katika diplomasia ya kikanda na kimataifa. Aidha, TSN imeendelea kusambaza jumla ya nakala za magazeti 1,909,752, wasomaji wa gazeti tepe wameongezeka kwa asilimia 24 na ufuatiliaji wa majukwaa ya kidigitali umeongezeka kwa asimilia 19.

**73. *Mheshimiwa Spika,*** TSN imeanzisha maktaba maalum ya historia kwa kuweka matoleo ya zamani ya magazeti na picha kwenye mfumo wa kidijiti. Jumla ya matoleo 12,600 ya *Daily News* na *HabariLeo*, picha 2,499 na makala maalumu 2,100 zimepatiwa alama ya utambuzi *(indexing)*. Mfumu huu umehifadhi nyaraka zote muhimu zinazohusu historia ya nchi, historia

kuhusu viongozi wakiwemo waasisi wa Taifa, historia ya harakati za ukombozi wa Uhuru kwa nchi za Kusini mwa Afrika na historia kuhusu masuala ya kidiplomasia. Kutokana na maktaba ya TSN kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu za kihistoria Kampuni imefanikiwa kuwa chanzo kikuu cha taarifa kwa ajili ya Kitabu cha Rais wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa; Rais wa Awamu ya Pili, Hayati Ally Hassan Mwinyi; Kitabu cha Muungano; na picha zote zilizopamba Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere. Katika hatua ya uimarishaji wa mfumo wa kidigiti, kampuni imeunda mfumo wa *TSN Intergreted Management Information System (TIMIS)* unaounganisha *Digital Archive* na tovuti ya Kampuni ili kuwezesha kutoa huduma na kupata taarifa zote popote duniani.

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutangaza utalii, kipekee TSN imeendelea kuandaa na kuchapa makala maalumu zenye maudhui kuhusu sekta ya utalii. Jumla ya makala 172 ziliandaliwa ikiwa yanalenga kuibua na kuonesha vivutio vya utalii, mafanikio ya sekta ya utalii, fursa za ajira na uwekezaji, pamoja na mchango wa sekta ya utalii katika kukuza pato la Taifa na ustawi wa wananchi. Makala maalumu zilikuwa na lengo kimkakati la kuitangaza Tanzania kimataifa kama kivutio bora cha utalii na uwekezaji.

**75.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TSN imeimarisha maktaba maalumu ya kidigiti kwa ajili ya

kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za magazeti na picha zilizotumika katika habari zilizochapishwa. Hadi Aprili 2026, magazeti ya Daily News yenye zaidi ya miaka 90 na HabariLEO yenye miaka 20 yaliyobeba taarifa muhimu kuhusu historia ya Tanzania, historia ya viongozi mashuhuri nchini na nje ya nchi, habari za uhusiano wa kidiplomasia, habari za harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika na historia ya masuala ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kimichezo yameihifadhiwa kwenye maktaba, ambapo huduma ya upatikanaji wa taarifa za Maktaba ya kidigiti zinapatikana kupitia anuani ya ePaper.tsn.go.tz.

**76.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TSN imefanya utafiti wa masoko ili kuboresha ubora wa bidhaa na huduma zinazotolewa na TSN. Februari 2026, TSN ilikamilisha na kuwasilisha taarifa ya utafiti wa masoko katika Bodi ya Wakurugenzi ambapo utafiti ulijikita katika maeneo ya mahitaji ya soko, aina ya wateja, biashara pamoja na ubora wa bidhaa. Matokeo ya utafiti yamewezesha kuboresha usambazaji wa magazeti kwa njia ya nakala ngumu, matumizi ya teknolojia katika usambazaji wa magazeti kwa njia ya mfumo. Sambamba na hayo, maboresho ya *ePaper App* yamelenga kuendana na mabadiliko ya teknolojia kwa kuongeza jitihada katika uuzaji wa gazeti tepe ili kuongeza mapato.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhimiza jitihada za matumizi bora ya mifumo kwa ajili ya kurahisisha utoaji huduma, Wizara kupitia TSN imeendelea na maboresho ya mifumo ya utoaji wa huduma ikiwa na lengo la

kuongeza ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za Kampuni, ambapo hadi Aprili 2026, TSN imeboresha mifumo miwili (2) ambayo ni mfumo wa ankara *(TSN billing system)* kwa ajili ya kumrahisisishia mteja kufikia huduma kwa urahisi na kukamilisha malipo ya huduma husika na kuboresha upatikanaji wa gazeti mtandao *(TSN ePaper)* kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa gazeti tepe kwa njia ya mtandao kwa ubora na wakati sahihi.

### 3.2.1.4 Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229, kwa lengo la kusimamia, kuimarisha na kuhakikisha taaluma ya uandishi wa habari nchini inazingatia misingi ya weledi, maadili na uwajibikaji, pamoja na kuratibu utoaji wa mafunzo kwa Waandishi wa Habari. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Bodi ya Ithibati imetekeleza majukumu yafuatayo:

**79.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Ithibati imepokea maombi na kusajili waandishi wa habari 4,139 kupitia mfumo wa Tai Habari ambapo Waandishi wa Habari 3,357 wenye vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa sheria wamepatiwa ithibati.

**80.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuhakikisha kuwa Maadili ya Taaluma ya Waandishi wa Habari yanazingatiwa, Wizara kupitia Bodi ya Ithibati imeshughulikia malalamiko 14 ya uvunjifu wa maadili ya taaluma ya

habari katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026. Malalamiko hayo yameshughulikiwa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwaita wahusika kuzungumza nao na kuwaonya na wale ambao hawakuwa na vigezo kuwashauri kuacha kufanya kazi za kihabari na kutafuta sifa za taaluma kwa mujibu wa Sheria.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Ithibati imeandaa mwongozo maalumu wa kisheria utakaowezesha wanahabari wakongwe walioathiriwa na mfumo wa ithibati kurejea katika mfumo rasmi, kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 ambayo ilitungwa kwa ajili ya kukuza taaluma ya uandishi wa habari kwa kuweka mfumo wa kitaasisi utakaosimamia sekta ya habari. Mwongozo huu umeandaliwa kwa kutambua kwamba kumekuwepo na kundi la waandishi wa habari waliopata ujuzi na uzoefu wa muda mrefu kazini bila kuwa na sifa rasmi za kitaaluma kama zinavyotambuliwa kisheria na wamechangia kwa kiwango kikubwa katika maendeleo ya taaluma ya habari. Mwongozo huu unaweka utaratibu wa kisheria wa kutambua na kuthibitisha umahiri wao kupitia tathmini maalumu ya uzoefu, weledi na maadili ya taaluma, na kuwawezesha kupata ithibati kwa mujibu wa sheria. Utekelezaji wa mwongozo huo unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2026/27.

**82.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuhakikisha kuwa Waandishi wa Habari wanakuwa na weledi katika taaluma yao Bodi iliratibu mafunzo ya muda mfupi ya Waandishi wa Habari. Bodi ya Ithibati kwa kushirikiana

na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Shule Kuu ya Uandishi wa Habari) ilifanikiwa kutoa mafunzo katika Kanda tano (5) ambazo ni Kanda ya Mashariki tarehe 11 Agosti, 2025; Kaskazini tarehe16 Agosti, 2025; Kanda ya Kati, tarehe 14 Agosti, 2025, Nyanda za Juu Kusini tarehe19 Agosti, 2025 na Kanda ya Ziwa, tarehe 07 Agosti, 2025 ambapo Waandishi wa Habari 1,071 walipewa mafunzo kuhusu uzingatiaji wa maadili ya uandishi wa Habari katika utekelezaji wa majukumu yao.

**83.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwa na kumbukumbu sahihi za Waandishi wa Habari, Serikali imeendelea kuimarisha utunzaji wa kanzidata ya Ithibati ya Waandishi wa Habari. Wizara kupitia Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao na Idara ya Habari-MAELEZO ilifanikiwa kutengeneza Mfumo wa Ithibati wa kidijiti kwa ajili ya usajili na kutunza Kanzidata ya Waandishi wa Habari unaojulikana kwa jina la **TAI – HABARI**. Mfumo huu umeleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Habari ambapo Waandishi wa Habari wanajisajili mahali walipo na kupata vitambulisho vya kidijiti (Digital Press Card). Aidha, Mfumo umerahisisha upatikanajii wa taarifa na takwimu sahihi za Waandishi wa Habari wanaofanya kazi za kihabari nchini ambapo hadi Aprili 2026, jumla ya Waandishi wa Habari 4,139 wamejisajili.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia ushirikiano kati ya Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari na Mfuko wa

Utamaduni na Sanaa Tanzania, Serikali inaendelea kuchukua hatua za kuwawezesha vijana wanaojiajiri katika sekta ya habari kwa kuwawezesha mitaji ya kukuza, kuendeleza na kuzalisha kazi zao katika ubora unaokidhi mahitaji ya soko kupitia mikopo yenye masharti nafuu. Katika kutekeleza hayo, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** anatoa shilingi 20,000,000,000 kwa ajili ya Mfuko wa Utamaduni na tayari 2,000,000,000 kwa ajili ya mikopo kwa Watengeneza Maudhui Mtandaoni *(content creators)* zimetoka kwa lengo la kuwasaidia kupata vitendea kazi na kuongeza uzalishaji wa kazi zao.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Utamaduni na Sanaa umetoa mafunzo kwa watengeneza Maudhui Mtandaoni yenye lengo la kuwawezesha kutengeneza kazi zenye ubora kwa soko shindani la ndani na nje ya nchi. Mafunzo kwa awamu ya kwanza yametolewa kwa watengeneza Maudhui Mtandaoni 931 ambao kati yao wanawake ni 574 sawa na asilimia 62 na wanaume ni 357 sawa na asilimia 38 kutoka mikoa mitatu (3) ya Dar es Salaam (347), Mwanza (250) na Arusha (334). Aidha, mada zilizofundishwa ni pamoja na umuhimu na aina za urasimishaji, kubiasharisha maudhui, maadili na miongozo ya utoaji huduma mtandaoni, elimu ya fedha, masoko, uwekezaji pamoja na usimamizi na uandishi wa miradi.

### 3.2.1.5 Kamati ya Maudhui (TCRA)

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania huundwa na Waziri

mwenye dhamana na sekta ya Habari na Utangazaji kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2023. Kwa mujibu wa Kifungu hicho, Mjumbe mmojawapo wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndiye huwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui ambayo ina wajumbe wasiozidi watano (5). Muda wa wajumbe hao utakuwa miaka mitatu (3) kuanzia tarehe ya kuteuliwa. Wajumbe hao wanaweza kuteuliwa tena kwa muhula mwingine mmoja.

**87.** ***Mheshimiwa Spika***, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania hutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 28 cha Sheria hiyo na kuyatolea taarifa kwa Waziri mwenye dhamana ya Habari na Utangazaji. Majukumu ya Kamati hii ni kusimamia maudhui yanayotolewa katika vyombo vya habari na kuchukua hatua pale kunapotokea ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na maadili. Kabla ya kuchukua hatua za kisheria, Serikali hutanguliza mazungumzo, ushauri na utoaji wa maelekezo kwa vyombo husika ikilenga kutoa fursa ya kujirekebisha. Hatua hizi huchukuliwa pale tu ambapo ukiukaji unaendelea, unajirudia au unasababisha madhara makubwa kwa umma. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano imetekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kufanya vikao tisa (9) vya Kamati vya kushughulikia mashauri dhidi ya watoa huduma 14 ambao walikiuka Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni zao;

(ii) Kufanya mapitio ya taarifa ya ukiukaji wa kanuni za utangazaji dhidi ya watoa huduma11 wa maudhui ya utangazaji waliobainika kuwa na ukiukaji wa mara kwa mara wa Sheria, Kanuni na Masharti ya Leseni; na
(iii) Kushiriki kwenye vikao vitatu (3) vya mashauriano na watoa huduma wa utangazaji wa maudhui kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Masharti ya Leseni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

### 3.2.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**88.** ***Mheshimwa Spika***, utamaduni ndio mtima wa Taifa, hakuna Taifa linaloweza kujitambulisha kwa utamaduni wa nchi nyingine. Aidha, Tanzania ni taifa pekee katika Afrika Mashariki na Kati lililofanikiwa kwa kiasi kikubwa kuhimili misukosuko inayotokana na tamaduni za kigeni kwa kudumisha utamaduni wake. Tanzania imefanikiwa kudumisha misingi ya umoja, mshikamano, upendo, amani na utangamano wa kitaifa bila kujali wingi wa jamii tulizonazo.

#### 3.2.2.1 Idara ya Maendeleo ya Utamaduni

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya utamaduni imekasimiwa majukumu ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa utamaduni wa Taifa ikijumuisha lugha, mila, desturi, historia na maadili ya Taifa. Aidha, sekta hii ina jukumu la kudumisha na kuendeleza utambulisho wa Taifa letu; kuhamasisha na kukuza thamani ya utamaduni wa Taifa kwa wananchi hususan

watoto na vijana ambao ndio hazina ya Taifa la sasa na baadaye; kuratibu na kusimamia maendeleo ya lugha adhimu na aushi ya Kiswahili ndani na nje ya nchi pamoja na kuratibu na kufanya tafiti za urithi wa utamaduni usioshikika hususani lugha za kijamii ambazo ni kibebeo kikuu cha urithi wa utamaduni wa Taifa letu. Vilevile, sekta hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili, 2026, sekta ya utamaduni imetekeleza majukumu mbalimbali yafuatayo:

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imejaliwa kuwa na utajiri mkubwa wa uanuai wa urithi wa utamaduni. Katika kuhakikisha kuwa urithi huu unalindwa, unahifadhiwa na kuendelezwa, Serikali imefanya utafiti wa kutambua, kuorodhesha na kulinda urithi wa utamaduni usioshikika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Utafiti huo uliofanyika kwa kushirikisha wadau wa utamaduni ulijikita katika kutambua na kuorodhesha Vazi la Kanga kama moja ya alama muhimu ya utambulisho wa Mtanzania na urithi wa Utamaduni. Kufuatia utafiti huo, andiko la Vazi la Kanga liliwasilishwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) tarehe 31 Machi, 2026 kwa lengo la kuingizwa kwenye orodha ya Urithi wa Dunia wa Utamaduni Usioshikika inayosimamiwa na Shirika hilo. Manufaa ya kutambuliwa kwa urithi wa utamaduni wa Tanzania katika Orodha ya Urithi wa Dunia ni pamoja na kuongeza hadhi ya utambuzi wa kimataifa; kupata fursa

za ufadhili wa uendelezaji na uhifadhi wa urithi huo kutoka kwenye mifuko ya kimataifa inayoratibiwa na UNESCO; kutangaza urithi wa utamaduni wa Tanzania pamoja na utalii wa kiutamaduni duniani.

**91.** ***Mheshimiwa Spika***, jitihada nyingine zilizofanywa na Serikali ni kukamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa miaka mitano (5) 2026/27 - 2030/31 wa Kulinda Urithi wa Utamaduni Usioshikika *(National Framework for Safeguarding Intangible Cultural Heritage)* ili kuhakikisha urithi wetu wa utamaduni unaendelea kulindwa na kudumishwa. Vilevile, katika kupanua wigo wa uelewa kwa wadau wa masuala ya urithi wa utamaduni, Serikali kupitia Wizara iliratibu warsha ya wadau wa utamaduni iliyofanyika tarehe 11 Novemba, 2025 jijini Dar es Salaam ambapo takribani washiriki 150 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walihudhuria.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na suala la mmomonyoko wa maadili nchini, Serikali kupitia Wizara imeandaa Mkakati wa Taifa wa miaka 10 yaani 2026/27 hadi 2036/37 wa kukabiliana na Mmomonyoko wa Maadili nchini. Maandalizi ya mkakati huo yameshirikisha wadau mbalimbali wakiwamo; Wizara, taasisi za umma, asasi za kiraia, sekta binafsi, viongozi wa dini na vyombo vya ulinzi na usalama.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** mbali na mkakati huo, Serikali kupitia televisheni ya Taifa TBC imeanzisha kipindi maalumu cha Maadili, Uzalendo na Utaifa kinachojulikana kwa jina la ***"Sisi ni Tanzania"***. Kipindi hiki ni mahususi kwa ajili ya kuukumbusha

umma wa Watanzania kuhusu umuhimu wa kurejea kwenye misingi ya maadili, mila, desturi, miiko, uzalendo na uadilifu.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na mmomonyoko wa maadili nchini, ulinzi wa maadili na utamaduni wetu ni jukumu mtambuka na linamgusa kila mtu katika jamii kwani Serikali pekee haiwezi. Familia, Taasisi za dini, mashirika na watu binafsi wanapaswa kushiriki kikamilifu katika kulinda na kurithisha maadili kwa jamii hususan watoto na vijana. Wazazi na Walezi wanahimizwa kusimamia malezi bora, ikiwamo kudhibiti maudhui wanayoyapata watoto kupitia vyombo vya habari. Ushirikiano wa wadau wote ni msingi wa kulinda utamaduni na maadili ya Taifa. Hivyo, nitoe wito kwa jamii nzima, kila mtu katika nafasi yake kulinda maadili ya Taifa na Utamaduni wetu kwa wivu mkubwa kwani hatuwezi kuwa Taifa lenye maendeleo kama tusipotengeneza kizazi chenye maadili.

**95.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa watanzania wanaendelea kujivunia, kusherehekea, kuenzi, kuthamini na kunufaika na urithi wa utamaduni wao, Serikali iliratibu matamasha manne (4) ya utamaduni yaliyoandaliwa na wadau. Matamasha hayo ni Tamasha la 16 la Muziki wa Cigogo lililofanyika katika viwanja vya Mshikamano vilivyopo Wilaya ya Chamwino, Dodoma tarehe 25 - 27 Julai, 2025; Tamasha la Utalii na Utamaduni la Serengeti (Serengeti Cultural Festival) lililofanyika tarehe 22 - 25 Julai, 2025 Mgumu wilayani Serengeti, mkoani Mara; Tamasha la

Utamaduni wa Wamaasai (Orkwaak le Maa Festival Week) lililofanyika tarehe 23 - 24 Agosti, 2025 Siha mkoani Kilimanjaro na Tamasha la Utamaduni la Jamii ya Wahaya (Ijuuka Omuka) lilifanyika tarehe 18 - 22 Desemba, 2025 mkoani Kagera.

Aidha, Wizara ilishiriki katika matukio mawili (2) ya kimila na kihistoria ambayo ni uzinduzi wa sherehe ya Kimila ya ubadilishanaji rika wa jamii ya Kimaasai ya Enkipaata iliyofanyika tarehe 18 - 21 Oktoba, 2025 mkoani Arusha; pamoja na Kumbukizi ya Mashujaa wa Vita vya Majimaji na Tamasha la Utalii wa Utamaduni lililofanyika tarehe 19 - 27 Februari, 2026 Songea mkoani Ruvuma. Kufanyika kwa matamasha ya utamaduni na matukio ya kimila na kihistoria ni muhimu sana kwani kunaimarisha mshikamano wa kitaifa, kurithisha tamaduni na kukuza utalii wa kiutamaduni.

**96.** ***Mheshimiwa Spika***, Utamaduni ni msingi wa utambulisho wa Taifa. Katika Taifa letu utamaduni umejengwa kwenye misingi ya utu, upendo, mshikamano, udugu na utaifa. Moja ya nyenzo muhimu ya kufanya utamaduni uwe hai ni kufanya matamasha ya utamaduni. Hivyo, ni wajibu wetu kuuenzi, kuuhifadhi na kuuendeleza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Kwa msingi huo, Serikali inasisitiza kuendelea kufanyika kwa matamasha ya utamaduni na matukio ya kihistoria katika jamii mbalimbali nchini kwa sababu yanaufanya utamaduni wetu kuendelea kuishi. Tukishindwa kuuenzi utamaduni wetu tutapoteza sifa ya kuwa taifa. Hivyo, tujivunie, tuuenzi

na kuuendeleza urithi wa utamaduni wetu.

**97.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 kwa lengo la kubainisha mafanikio, changamoto na mapungufu ya utekelezaji wa Sera hiyo. Hatua inayofuata ni kukamilisha uhuishaji wa sera hiyo.

**98.** ***Mhesimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa tunaimarisha utendaji kazi wa wataalamu na kuongeza tija na ufanisi kwenye utoaji wa huduma kwa wananchi, Serikali kupitia Wizara iliratibu Kikao Kazi cha kumi na sita (16) cha Maafisa Utamaduni nchini kilichofanyika tarehe 28 - 31 Machi, 2026 katika ukumbi wa AICC jijini Arusha. Kikao kazi hicho kiliwakutanisha Maafisa Utamaduni zaidi ya 250 kutoka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kwa ajili ya kujadili hali ya utekelezaji wa majukumu; kubainisha changamoto zinazokabili utendajikazi; na kupendekeza namna bora ya kuzitatua ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kufanyika kwa vikao vya kisekta ni jukwaa muhimu la kuwakutanisha watunga sera (Wizara) na watekelezaji wa Sera (Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa) kubadilishana uzoefu na kunoa ujuzi. Miongoni mwa matokeo ya vikao hivi ni kuongezeka kwa ufanisi na utendajikazi wa Maofisa Utamaduni katika maeneo yao; kupanuka kwa wigo wa ushirikiano miongoni mwao; na kuimarishwa kwa ari ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

#### 3.2.2.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliundwa kwa Sheria ya Baraza la Kiswahili la Taifa Sura ya 52. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Baraza ni chombo cha Serikali chenye dhamana ya kusimamia matumizi na maendeleo ya lugha ya Kiswahili na kufuatilia maendeleo yake ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo la msingi, BAKITA inatekeleza Mkakati wa Taifa wa Kupeleka Kiswahili kimataifa, inasimamia matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili na kuzuia upotoshaji wake. Pia, inatoa ithibati ya matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu na fasaha katika vitabu vinavyoandikwa kwa Kiswahili pamoja na kutoa tafsiri rasmi ya lugha ya Kiswahili. Majukumu mengine ni pamoja na kuratibu vyama, asasi na wadau wote wanaojishughulisha na ukuzaji na uendelezaji wa lugha ya Kiswahili na kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na umma na kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika katika kuanzisha tafsiri sanifu ya istilahi za Kiswahili katika nyanja mbalimbali. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, BAKITA imetekeleza majukumu mbalimbali yafuatayo:

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha Kiswahili kinaendana na mabadiliko ya teknolojia, BAKITA imeandaa Kongoo ya Kiswahili ya Taifa (KOKITA), shughuli hii ya pekee kwa lugha ya Kiswahili inayolenga kusheheneza Kiswahili katika teknolojia ya kikopyuta na kuhifadhi pamoja na kuonyesha muktadha wa matumizi ya maneno ya Kiswahili katika nyanja

mbalimbali na kuwa na nyenzo za kuwasaidia wanafunzi wa Kiswahili kama lugha ya kigeni, wanaleksikografia, waandishi wa vitabu na watafiti wa lugha mbalimbali. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, BAKITA imekusanya, imehariri na kuingiza maneno milioni 22 katika Kongoo ya Kiswahili ya Taifa (KOKITA), ambapo hadi Aprili 2026, kongoo hiyo ina jumla ya maneno milioni 61 na lengo ni kufikisha maneno milioni 100. Kongoo hii itakuwa daraja la kuongeza nafasi ya Kiswahili katika teknolojia ya kikompyuta hususani katika matumizi ya Akili Unde (AI). Pia, Baraza linaendelea kukuza ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwamo Taasisi ya Mozilla ili kuwezesha kuimarisha Kiswahili katika Teknolojia.

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia BAKITA imeongoza umma wa wazungumzaji wa Kiswahili, wadau na wapenzi wa Kiswahili Afrika na Duniani kote kushughudia hatua kubwa ya Kiswahili kukubalika kuwa lugha rasmi ya Mkutano Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Kiswahili ni lugha ya kwanza ya Afrika kupata hadhi hiyo na hayo yalijiri katika Mkutano Mkuu wa 43 wa Shirika hilo uliofanyika Samarkand - Uzbekstani tarehe 30 Oktoba hadi 13 Novemba, 2025. Kwa muktadha huo, Kiswahili sasa ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendekleo kwa Nchi za Kusini mwa Afrika, Umoja wa Afrika, Umoja wa Wazalishaji Almasi Afrika na UNESCO. Vilevile, Kiswahili ni lugha pekee ya Afrika iliyotengewa siku ya kuadhimishwa ambayo ni tarehe 7 Julai kila mwaka. Katika hatua nyingine, Wizara kupitia BAKITA

imefanya kikao na UNESCO pamoja na wadau wa maudhui ya mtandaoni kuhusu nafasi ya Kiswahili katika mitandao mikubwa ya kijamii ya META, TikTok na Google ili wapanue nafasi ya Kiswahili katika mitandao hiyo na hivyo kuongeza ajira na kipato kwa waandaaji wa maudhui kupitia mitandao ya kijamii.

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, nyota ya Kiswahili imeendelea kuangaza Kimataifa baada ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kuridhia Lugha hiyo kuwa mojawapo ya Lugha rasmi zitakazotumika katika Mikutano Mikuu ya Shirika hilo. Hatua hii inaifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza yenye asili ya Afrika kupewa hadhi hiyo. Jitihada hizi ni hatua za makusudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha Kiswahili kinapata hadhi katika majukwaa ya kimataifa, ambapo kwa sasa Kiswahili ni Lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Wazalishaji Almasi Afrika (ADPA) na Umoja wa Afrika (AU).

**103.** ***Mheshimiwa Spika***, pia, Lugha ya Kiswahili imetengewa Siku Maalumu ya Kuadhimishwa Duniani na Shirika la UNESCO ambapo hufanyika kila ifikapo tarehe 7 Julai kila mwaka. Kwa kuenzi siku hiyo, Serikali kupitia BAKITA kwa kushirikiana na BAKIZA iliungana na balozi mbalimbali ndani na nje ya Tanzania pamoja na mashirika mbalimbali ya kimataifa ikiwamo

UNESCO kufanya maadhimisho ya Nne ya siku ya Kiswahili Duniani ambayo kitaifa yalifanyika Zanzibar kuanzia tarehe 05 - 07 Julai, 2025. Maadhimisho hayo yalitanguliwa na Mbio za Masafa za Kimataifa za Kiswahili zilizofanyika tarehe 28 Juni 2025 jijini Arusha chini ya Kaulimbiu "Kiswahili Fahari ya Afrika, tukienzi na kukiendeleza". Aidha, maadhimisho yaliendelea tarehe 5 Julai, 2025 kwa tukio la Usiku wa Mwanamke Hazina lililokuwa na mada ya "Nafasi ya mwanamke katika Utawala na Uongozi" kwa mtazamo wa Fasihi ya Afrika. Tukio hilo lilikwenda sambamba na usiku wa Mswahili uliofanyika katika Ukumbi wa New Amani Hotel, Zanzibar.

**104.** ***Mheshimiwa Spika***, matembezi ya wanafunzi na wadau wa Kiswahili yaliendelea tarehe 6 Julai, 2025 ambayo yalianzia Skuli ya Sekondari ya Tumekuja na kuishia katika Viwanja vya Polisi Ziwani Zanzibar. Matembezi hayo yalilenga kuhimiza matumizi ya Lugha ya Kiswahili miongoni mwa Wanafunzi na wadau wa Kiswahili. Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU) kilifanyika katika Ukumbi wa Polisi Ziwani Zanzibar mnamo tarehe 7 Julai 2025, ambapo Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar aliyemwakilisha Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufunga maadhimisho hayo. Maadhimisho hayo yalikuwa na kaulimbiu: "Kiswahili kwa Amani na Mshikamano."

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, BAKITA iliratibu ushiriki wa Tanzania katika maadhimisho ya Nne ya kikanda ya siku ya Kiswahili Duniani kwa nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki, yaliyoratibiwa na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA) yaliyofanyika Kikanda Kigali, Rwanda. Pia maadhimisho hayo yalifanyika kwenye Maonyesho ya Dunia ya Biashara, Osaka Expo 2025 nchini Japani. Halikadhalika, balozi mbalimbali za Tanzania ziliadhimisha siku hiyo ya Kiswahili na kuonyesha masuala mbalimbali ya utamaduni wa Mswahili ikiwa ni pamoja na vyakula na mavazi.

**106.** ***Mheshimiwa Spika***, BAKITA ilipata nafasi ya kushiriki katika Kongamano la Kiswahili na Tuzo za Wasta lililofanyika tarehe 10 - 11 Oktoba, 2025 jijini Nairobi, Kenya na kongamano la Kiswahili lililoandaliwa Uganda tarehe 13 - 17 Aprili, 2025. Aidha, BAKITA ilishiriki Kongamano la Chama cha Kiswahili Duniani (CHAUKIDU) liliofanyika tarehe 14 - 16, Desemba, 2025 nchini Kenya. Makongamano haya yote yalikuwa na lengo la kuwaleta pamoja walumbi, wataalamu na wadau wa Kiswahili kujadili mambo mbalimbali ya kukienzi na kukiendeleza Kiswahili.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Kiswahili kinasheheni msamiati mpya na unaokidhi mahitaji katika nyanja mbalimbali, BAKITA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali vikiwamo vyuo vikuu, Wizara, pamoja na wataalamu wa lugha katika uga wa istilahi, isimu na lahaja waliunda jopo la pamoja na kuandaa Mwongozo wa Usanifishaji Mkubwa wa Pili

(II). Usanifishaji huu unafanyika baada ya ule wa mwaka 1,930, ambao unalenga kuboresha na kukusanya maneno mengi zaidi kutoka katika lugha za Afrika ili kujenga umiliki wa pamoja wa lugha ya Kiswahili barani Afrika. Halikadhalika, BAKITA inaendelea kufanya utafiti wa maneno, ambapo maneno 1,371 yamekusanywa kutoka lugha mbalimbali za Kibantu kama Luganda, Kinyarwanda, Kilingala, Kioshiwambo, na Kizulu, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mradi wa usanifishaji mkubwa. Kazi hii ni hatua muhimu baada ya Kiswahili kupata hadhi maalumu katika jumuiya za kikanda na kimataifa.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo katika kuelekea mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) 2027, Serikali kupitia BAKITA inaendelea na shughuli ya usanifishaji wa Istilahi za michezo, ambapo hadi sasa jumla ya istilahi 420 za michezo zimesanifishwa.

**109.** ***Mheshimiwa Spika***, Wahenga wanasema, "Asiyefahamu lugha, hafahamu mila". BAKITA imeendelea kuuelimisha umma kuhusu kuzingatia matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu pamoja na utamaduni wake. Shughuli hii imehusisha kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 1,057 kupitia vituo vya TBC Taifa, Radio One, UFM, Times FM, Clouds FM, Kiss FM, Wapo Redio, Channel Ten TV, Shine FM, Redio Maria, Idea FM na Radio Umoja wa Mataifa. Aidha, Baraza liliandaa maudhui 758 ya mtandaoni na kutoa elimu ya matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia mitandao ya kijamii ambayo ni *facebook*, *youtube*, na

*instagram*, pamoja na kuandaa Makala 42 zilizochapishwa katika gazeti la HabariLEO toleo la kila siku ya Ijumaa. Jitihada hizi ni hatua muhimu za kuhakikisha wananchi wote wanatumia Kiswahili fasaha na sanifu katika shughuli za kila siku.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwezesha Watanzania kunufaika na fursa za Kiswahili duniani, BAKITA imeendelea kuwanoa walimu wenye stadi za kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kwa kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni. Baraza liliendesha kozi hiyo ya muda mfupi kwa walimu 83 jijini Dar es Salaam. Aidha, lilitoa Mafunzo hayo kwa walimu saba (7) katika Chuo Kikuu cha St. Johns jijini Dodoma, ambapo yalikuwa ni mafunzo ya kimkakati kwani walimu watano (5) walipata nafasi ya kufundisha Kiswahili kwa wenyeji nchini Afrika Kusini. Pia, Baraza lilitoa mafunzo ya aina hiyo kwa waongoza watalii 17. Mafunzo hayo yalifanyika jijini Arusha katika Shule ya Msingi Meru, ikiwa ni sehemu ya kukuza lugha ya Kiswahili kupitia utalii. Mafunzo haya yameongeza chachu kwani Watanzania wameendelea kunufaika na fursa za kujiajiri kupitia taaluma za Kiswahili na stadi nyingine husianifu, mathalani hadi Aprili 2026 jumla ya watanzania 507 wanafanya kazi ya ufundishaji wa Kiswahili nje ya nchi.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Kiswahili kutumika kikamilifu katika utoaji wa huduma za umma, BAKITA imeendelea kutoa mafunzo ya msasa ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu pamoja na

utamaduni wake kwa makundi maalumu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Baraza kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi Waendesha Ofisi Tanzania (TAPSEA), lilitoa mafunzo ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu na utamaduni wake kwa Waandishi Waendesha Ofisi (WWO) 844. Halikadhalika, mafunzo hayo yameendelea kwa Makatibu wa kamati za Halmashauri 12 pamoja na Wahudumu wa Mapokezi na Huduma kwa Wateja 52. Kwa ujumla washiriki 2,094 waliopatiwa mafunzo hayo. Natoa rai kwa kada zote kushiriki mafunzo haya, ili kujengewa uwezo wa kuwasiliana na kuandika nyaraka kwa Kiswahili fasaha na sanifu katika mazingira rasmi.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha vyombo vya habari vinaongeza wigo wa matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili. Serikali imeendelea kutoa elimu na semina kwa wanahabari kwa nia ya kutilia mkazo matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza limeandaa na kufanya Kongamano la tano (5) la Idhaa zinazotangaza kwa Kiswahili Duniani likiwa na kaulimbiu “Tasnia ya Habari, Msingi wa Maendeleo ya Kiswahili Duniani”. Lengo kuu la Kongamano la Idhaa ni kuimarisha uhusiano wa taasisi za Kiswahili na vyombo vya habari ambavyo vinatekeleza jukumu kubwa la kukikuza na kukieneza Kiswahili ndani na nje ya nchi. Kongamano hili lilihusisha wamiliki wa vyombo vya habari, wahariri, watangazaji na waandishi katika redio, televisheni, magazeti na blogu za Kiswahili duniani. Aidha, washiriki wengine ni pamoja na maafisa habari wa Wizara, Idara, Taasisi, Kampuni na Mashirika

yaliyomo nchini na watozi wa studio za muziki, filamu na matangazo. Pia, makundi mengine yaliyoshiriki ni pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa, wataalamu wa lugha ya Kiswahili walio katika taasisi za Kiswahili, wawakilishi wa vyama vya Kiswahili, wachapishaji, wahadhiri na wanafunzi wa vyuo vikuu na walimu wa Kiswahili wa shule za sekondari za jijini Arusha. Kongamano lilifanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) jijini Arusha tarehe 24 hadi 27 Machi, 2026.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikikikisha umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wageni wanaojifunza Kiswahili, BAKITA imeendesha mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wageni. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Baraza iliandaa na kusimamia mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wageni 29 kutoka nchi za Kenya (7), Ghana (5), Zimbabwe (3), Malawi (2), Somalia (1), Uingereza (1), Sudani (2), India (1), Nigeria (4), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (3) na Jamhuri ya Cheki (1). Aidha, miongoni mwao ni madaktari 21 waliokuja nchini kufanya mafunzo ya vitendo chini ya Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT). Aidha, upimaji wa Umahiri wa lugha ulifanyika kwa wanafunzi 25 wa shule ya kimataifa ya Breaburn ya jijini Arusha. Hatua hii ya msingi inaunga mkono jitihada za Serikali katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi hasa zile zinazotolewa na wageni.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukuza na kueneza

matumizi ya Kiswahili katika majukwaa ya kimataifa. Hatua hizo ni pamoja na kushirikiana na mashirika ya kimataifa na nchi rafiki katika kufundisha Kiswahili pamoja na kuandaa programu za mafunzo ya lugha hiyo kwa wageni. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia BAKITA ilitoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni 57 kwa njia ya mkondoni, wakiwemo Wanafunzi 53 wa Chuo cha Triumphant na Wanadiplomasia wanne (4) kutoka nchini Namibia. Aidha, wageni 20 walipata mafunzo hayo kwa njia ya ana kwa ana yaliyotolewa katika ofisi za BAKITA jijini Dar es Salaam. Wageni hao walitoka nchi za Uingereza (2), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (3), Jamhuri ya Cheki (Czech) (1), Uturuki (1), Zimbabwe (4), Uganda (3), Sudani Kusini (1), Ghana (2), Botswana (2) na China (1). Vilevile, zaidi ya wageni 607 wamepatiwa mafunzo hayo kupitia vituo vinavyofundisha Kiswahili kwa wageni, vinavyosimamiwa na BAKITA ndani na nje ya nchi.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** BAKITA imefanya Tafiti kwa lengo la kuongeza maneno kwenye Kongoo ya Kiswahili ya Taifa (KOKITA). Tafiti tisa (9) zimefanywa katika nyuga za siasa, mazingira, elimu, sayansi na teknolojia, afya, uchumi, sanaa, michezo na kilimo. Utafiti huu umefanywa kwa kushirikiana na vyuo vikuu, wataalamu wa istilahi, wataalamu katika sekta husika pamoja na wadau mbalimbali wa lugha ya Kiswahili ambapo umewezesha kuongeza takribani maneno milioni 22 katika kongoo ya Taifa (KOKITA).

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma ya ukalimani inaimarika pamoja na

kuchangamkia fursa zinazotokana na mikutano ya kitaifa na kimataifa inayofanyika ndani na nje ya nchi, BAKITA ilitoa mafunzo ya msasa ya kuwajengea uwezo wakalimani 18. Mafunzo hayo yalifanyika kwa wiki mbili kuanzia tarehe 17 hadi 28 Novemba, 2025 katika darasa maalumu la Ukalimani lililopo ofisi za BAKITA jijini Dar es Salaam. Idadi hii inafanya nchi kuwa na jumla ya wakalimani 183 waliotambuliwa na BAKITA. Aidha, Baraza liliratibu na kutoa huduma za ukalimani katika mikutano 19 ya kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa mikutano hiyo ni: Pan Africa ILGA Conference in Johannesburg, South Afrika – Mistry Hills Hotel; The forth International Conference on Business Management and Economic Develpment (ICBMED): *Creativity, Innovation and Business for Economic Development* – Gold Crest Hotel Mwanza; *Regional Training and Certification Program for Biosafety and Biosecurity Professionals* – NPHL Dar es Salaam; Haki za Wanawake katika Majiji – Zanzibar; Kusikiliza shauri la kesi ya madai – Mahakama Kuu pamoja na Shauri la kukutwa na nyara za Serikali (Kasa na Kobe wa majini) – Kituo cha Polisi Sitakishari, Ukonga - Dar es Salaam.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** ufunguaji wa vituo vya kufundishia Kiswahli kwa wageni ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kufanya Kiswahili kuwa bidhaa ya miaka kumi (10) kutoka 2022 – 2032. Katika kuhakikisha dhamira ya Serikari ya awamu ya sita katika kukuza na kuendeleza Kiswahili duniani, BAKITA imetambua na kusajili jumla ya vituo vitano (5). Vituo hivyo ni pamoja na *Kiswahili Centre of Excellence in South Afrika* (KCESA), *Tanzania Kiswahili Cultural*

*Centre* vyote vya nchini Afrika ya Kusini na vinamilikiwa na Watanzania waishio Afrika Kusini. Aidha, kituo kimoja (1) cha Imani Languages Academy kinachomilikiwa na Mtanzania kimesajiliwa nchini Japani. Vituo viwili (2) vimefunguliwa ndani ya nchi, ambapo ni pamoja na St. Constantine's International school jijini Arusha na Laoshi Institute of Languages cha jijini Dar es Salam. Hatua hii inafanya kuwe na jumla ya vituo 55 vya kufundisha Kiswahili kwa wageni, ambapo vituo 20 vipo nje ya nchi na 35 vipo nchini. Ufunguaji wa vituo hivi umeongeza chachu ya ujifunzaji wa Kiswahili kwa wageni.

**118.** ***Mheshimiwa Spika***, Fauka ya hayo, nafasi ya Kiswahili Kimataifa inategemewa kuimarisha ajira na fursa kwa wataalamu wa Kiswahili katika Ufundishaji, Tafsiri, Ukalimani, Uandishi wa Vitabu na Utangazaji. Ni azma ya Nchi yetu kukuza diplomasia, shughuli za kiuchumi, uwekezaji, kilimo, utalii, madini, viwanda na biashara kupitia lugha ya Kiswahili. Pamoja na kazi kubwa iliyofanywa katika eneo hili la lugha adhimu na aushi ya Kiswahili, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi sasa Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa saba (7) duniani zilizotambuliwa na kupangiwa siku yake ya kuadhimishwa. Kiswahili ni lugha pekee ya Afrika katika lugha hizo. Kwa msingi huo tuna kila sababu ya kujivunia mafanikio makubwa tuliyoyapata ya lugha ya Kiswahili, moja ya Tunu muhimu na urithi wa Taifa letu.

### 3.2.2.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika (ALHC) kinaratibiwa na Wizara kwa mujibu wa Azimio la Umoja wa Afrika la mwaka 2011 (Assembly/AU/Dec.357 (XIV)), lililoridhia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa kitovu cha uhifadhi wa kumbukumbu za harakati za ukombozi wa Afrika kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Uamuzi huu haukuwa wa bahati mbaya, bali ni matokeo ya mchango mkubwa na wa kihistoria wa Tanzania katika mapambano ya ukombozi wa nchi nyingi za Afrika.

**120.** ***Mheshimiwa Spika***, kituo hiki kina jukumu pana na la kimkakati la kutambua, kukusanya, kuhifadhi na kuendeleza urithi wa ukombozi unaojumuisha nyaraka, picha, filamu, hotuba za viongozi, ramani, nyimbo, sare, pamoja na maeneo muhimu ya kihistoria kama vile makaburi ya mashujaa, kambi za wapigania uhuru na miundombinu ya ukombozi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Wizara kupitia Kituo hiki imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa kama ifuatavyo:

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kudumisha hadhi ya Tanzania kama "Mama wa Ukombozi wa Afrika" kwa vitendo, kwa kuhakikisha kuwa mchango wetu wa kihistoria unatambulika, unahifadhiwa na kuendelezwa kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Katika kuonesha dhamira hiyo,

tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uamuzi wake wa kimkakati wa kuutekeleza mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Afrika. Hatua hii inaakisi uongozi thabiti na dira ya kulinda historia ya Taifa letu huku tukiiweka katika nafasi ya kimataifa kama kitovu cha kumbukumbu za ukombozi wa Bara la Afrika.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya utekelezaji, Wizara kupitia Kituo imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 424.6 katika Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uhifadhi wa Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika kitakachokuwa Taasisi ya Umoja wa Afrika. Eneo hilo tayari limeshamilikishwa rasmi kwa Wizara, hatua inayoweka msingi imara wa utekelezaji wa mradi huu wa kimkakati wa kitaifa na kibara. Aidha, maandalizi yanaendelea ikiwa ni pamoja na taratibu za kumpata Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa ujenzi. Hakika, Kituo hiki hakitakuwa tu alama ya kihistoria ya urithi wa ukombozi, bali pia kitakuwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi kupitia utalii wa kihistoria, kitaongeza ajira kwa vijana, na kuleta manufaa kwa Wilaya ya Kongwa na Taifa kwa ujumla, sambamba na kuimarisha mshikamano wa kitaifa na nafasi ya Tanzania kama kielelezo cha uongozi na mshikamano wa Bara la Afrika katika kuendeleza urithi na uchumi wa utamaduni.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuonesha dhamira ya dhati na isiyotetereka katika kulinda na kuhifadhi urithi wa ukombozi ambao ni msingi wa historia, heshima na utambulisho wa Taifa letu. Ni dhahiri kuwa bila historia imara Taifa hupoteza dira, na bila kuilinda tunahatarisha mustakabali wa vizazi vijavyo. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia Kituo ilipanda miche 700 ya mianzi kandokando ya Mto Ngerengere katika eneo la Mazimbu, Mkoa wa Morogoro kwa lengo la kudhibiti mmomonyoko wa udongo uliokuwa unatishia makaburi ya mashujaa wa ukombozi. Hatua hii imeimarisha ulinzi wa mazingira ya maeneo ya kumbukumbu za kihistoria na kuhakikisha makaburi hayo yanaendelea kuhifadhiwa kwa usalama, hivyo kuthibitisha kuwa Serikali ni sikivu, inachukua hatua na inaweka msingi imara wa kizazi kijacho kujivunia chimbuko lake.

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Serikali imechukua hatua madhubuti za kuimarisha utambuzi na heshima kwa mashujaa wa harakati za ukombozi. Wizara kupitia Kituo imeweka vibao 35 vya utambulisho katika makaburi ya wapigania uhuru wa Afrika Kusini yaliyopo Mazimbu na Dakawa, hatua iliyoongeza upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wageni, wanafunzi na watafiti, pamoja na kuinua hadhi ya maeneo hayo kuwa vituo hai vya elimu ya historia ya ukombozi. Aidha, mabango nane ya utambulisho wa kihistoria yamesimikwa katika maeneo ya Kaole (Pwani), Mazimbu na Dakawa (Morogoro), pamoja na Kongwa (Dodoma) ili kuboresha utoaji wa taarifa kwa umma. Vilevile, maboresho ya mfumo wa maji katika eneo la

makaburi ya Dakawa yamefanyika ili kuwezesha umwagiliaji wa maua na kuboresha mandhari ya eneo hilo, hatua inayochangia kuhifadhi heshima na hadhi ya maeneo ya kumbukumbu za mashujaa wetu.

**125.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kubaki mstari wa mbele katika kuimarisha uhifadhi wa rasilimali za kumbukumbu ambazo ni mhimili muhimu wa historia ya Taifa na Bara kwa ujumla. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara kupitia Kituo ilifanya kazi ya kitaalamu ya kuchambua, kupanga na kuhifadhi nyaraka za kihistoria zilizopo katika Ofisi za Kituo cha Maendeleo Dakawa. Nyaraka hizo zinajumuisha vitabu na machapisho yaliyotumiwa na wanafunzi wa chama cha African National Congress (ANC) waliokuwa wakisoma nchini Tanzania wakati wa harakati za ukombozi. Zoezi hili lilifanyika kwa kuzingatia viwango vya kitaalamu vya uhifadhi wa kumbukumbu, ikiwemo matumizi ya maboksi maalumu yanayolinda nyaraka dhidi ya uharibifu wa kimazingira, na hivyo kuongeza usalama na uendelevu wa nyenzo hizi muhimu kwa matumizi ya tafiti, elimu na rejea za kihistoria.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na juhudi hizo, Kituo kilifanya mahojiano na mashuhuda 40 wa harakati za ukombozi wa Afrika kwa lengo la kuhifadhi simulizi na ushuhuda binafsi wa matukio ya kihistoria. Hatua hii imewezesha kuhifadhi historia hai ya ukombozi ambayo ni rasilimali adimu na yenye thamani kubwa kwa tafiti za kitaaluma, elimu ya kizazi kipya na uendelezaji wa utambulisho wa Bara la Afrika. Miongoni

mwa mashuhuda hao ni Bi. Sophia Halfani Namananda, aliyewahi kufundisha watoto wa wapigania uhuru wa FRELIMO katika Shule ya Msingi Lusewa, Songea mkoani Ruvuma, ushuhuda wake ukiwa kielelezo hai cha mchango wa Tanzania katika kuandaa na kulea kizazi cha wapigania uhuru barani Afrika.

**127.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa lengo la kuandaa na kusambaza maarifa ya kihistoria kwa vizazi vya sasa na vijavyo, Serikali imejipambanua kwa vitendo zaidi. Kituo imekamilisha uandaaji wa rasimu tatu (3) za vitabu ambavyo ni *Maeneo ya Urithi wa Ukombozi*; *Mchango wa Wanawake katika Harakati za Ukombozi wa Afrika*; pamoja na *Hotuba za Viongozi wa Afrika*. Machapisho hayo yataongeza upatikanaji wa taarifa sahihi kuhusu historia ya ukombozi wa Afrika na mchango wa Tanzania katika harakati hizo. Aidha, vitabu hivi vitatumika kama nyenzo muhimu katika taasisi za elimu, tafiti za kihistoria na katika kuhamasisha vijana kuelewa na kuthamini historia ya Bara la Afrika. Katika kipindi cha hadi mwezi Aprili 2026, Kituo kinaendelea na hatua za kitaalamu za uhakiki wa maudhui, uhariri pamoja na maandalizi ya uchapishaji ili kuhakikisha ubora na usahihi wa machapisho hayo kabla ya kusambazwa kwa umma.

**128.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa msukumo wa dhati, Serikali imejipanga kuimarisha utalii wa kihistoria na kuongeza uelewa kuhusu mchango wa Tanzania katika ukombozi wa Afrika kupitia uratibu wa ziara 16 zilizofanyika katika maeneo muhimu ya kihistoria yaliyopo katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Ruvuma,

Dar es Salaam, Dodoma na Iringa. Ziara hizi zilihusisha wadau mbalimbali wakiwemo maafisa wa Serikali, wanafunzi, watafiti, pamoja na wageni kutoka nje ya nchi. Ziara hizi zimechangia kwa kiasi kikubwa kuongeza uelewa wa historia ya ukombozi, kukuza utalii wa urithi na kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kidiplomasia. Vilevile, ziara za viongozi wa ngazi za juu, akiwemo Makamu wa Rais wa Zimbabwe Mheshimiwa Kembo Campbell Mohadi aliyetembelea Kaole, Bagamoyo tarehe 31 Agosti, 2025, zimeendelea kuimarisha uhusiano wa kihistoria na kuthibitisha nafasi ya Tanzania kama kitovu cha urithi na historia ya ukombozi wa Bara la Afrika.

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha uelewa wa historia ya ukombozi wa Afrika kwa kizazi cha sasa na kijacho kupitia kampeni za elimu, uhamasishaji na ushirikiano wa kimkakati, zikiwemo ziara 10 za elimu katika shule za Dar es Salaam, matumizi ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, pamoja na ushiriki katika majukwaa ya maonesho ya kitaifa ikiwemo Sabasaba, kumbukizi ya Vita vya Maji Maji na mikutano ya kitaifa ya Sekta mbalimbali hatua zilizowezesha kuwafikia maelfu ya wananchi na vijana. Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Shirika la Utangazaji Tanzania na Taasisi ya Elimu Tanzania, Kituo kimeendesha vipindi maalum vya elimu na kutoa mafunzo kwa wadau wa sekta ya elimu, hatua zinazodhihirisha dhamira thabiti ya Serikali ya kuendeleza urithi wa ukombozi kama chachu ya uzalendo, utambulisho wa Taifa na mshikamano wa kijamii.

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uelewa wa vijana na umma kuhusu harakati za ukombozi wa Afrika, Kituo iliratibu Maadhimisho ya Siku ya Ukombozi wa Nchi za Kusini mwa Afrika tarehe 23 Machi 2026 jijini Dar es Salaam, yaliyobebwa na kaulimbiu inayohamasisha ukuaji wa viwanda, mabadiliko ya kilimo na mpito wa nishati kwa SADC imara. Maadhimisho hayo yamekumbusha na kuimarisha mshikamano wa kihistoria wa ukombozi, huku yakisisitiza kuwa urithi huo ni chachu ya ushirikiano wa kikanda na maendeleo ya pamoja, na hivyo kuendeleza dhamira ya nchi wanachama kushirikiana kwa karibu zaidi kwa ustawi wa wananchi wa ukanda wa Kusini mwa Afrika.

**131.** ***Mheshimiwa Spika***, chini ya maelekezo na msukumo wa Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kimkakati kuhakikisha urithi wa kihistoria wa Taifa unalindwa na kudumu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo. Kituo imeendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya uhifadhi wa maeneo muhimu ya kihistoria ikiwamo Kongwa - Dodoma, Kaole – Pwani, na Kinondoni – Dar es Salaam, kwani maeneo ya urithi wa ukombozi yamekuwa yakikumbwa na changamoto ya kuharibika kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi na mazingira, shinikizo la kibiashara, maendeleo ya miji, pamoja na ukosefu wa uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa maeneo hayo.

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imechukua hatua kadhaa za kuzuia hali hiyo isiendelee kwa kuongeza juhudi za ukarabati na matengenezo katika baadhi ya maeneo hayo. Pamoja na changamoto hizo, Serikali imeongeza kasi ya ukarabati na matengenezo ya maeneo hayo, huku ikiimarisha ushirikiano na taasisi za kikanda na kimataifa kama Umoja wa Afrika kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujenga mikakati madhubuti ya pamoja ya kuhifadhi urithi wa ukombozi, hatua ambazo zinaendelea kudhihirisha nia ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha maeneo haya yanabaki salama na kuendelea kuwa sehemu ya fahari ya Taifa.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Awamu ya Sita inaendelea kuimarisha utambulisho wa Taifa kupitia uhifadhi na utangazaji wa urithi wa kihistoria kama kichocheo cha maendeleo na utalii. Kituo kimefanikisha kutangaza maeneo saba (7) ya historia ya ukombozi wa Bara la Afrika na Hifadhi ya Malikale kuwa urithi wa Taifa ili yatambuliwe, yahifadhiwe na kulindwa kisheria kupitia Tangazo la Serikali na 582 la tarehe 26 Septemba, 2025 ambapo maeneo yaliyotangazwa ni Kambi ya Wapigania uhuru wa Chama cha ANC iliyopo Mazimbu - Morogoro, Kambi ya Wapigania Uhuru wa chama cha FRELIMO iliyopo katika Shule ya Sekondari Samora Machel - Ruvuma, Kambi ya Wapigania Uhuru ya Kihesa Mgagao - Iringa, Makazi ya Mtemi Fundikira - Tabora na Mtemi Isike - Singida na maeneo mengine ya kihistoria hivyo kufikisha idadi 15 ya maeneo ya historia yaliyotangazwa. Hatua ya kutangazwa kwa maeneo hayo inalenga kuyatambua, kuyahifadhi na kuyalinda kupitia

sheria ya Malikale na kutangazwa kuwa maeneo ya kichocheo cha vivutio vya utalii wa kihistoria nchini.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu kwa mafanikio mchakato wa kukifanya Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kuwa miongoni mwa taasisi rasmi zilizo chini ya Umoja wa Afrika; ambapo katika kikao cha Baraza la Mawaziri la Umoja wa Afrika kilichofanyika mwezi Februari, 2026, azimio la kukitambua na kukiridhia Kituo hicho lilipitishwa rasmi, sambamba na kutoa wito kwa nchi zote wanachama wa Bara la Afrika, Jumuiya za Kikanda pamoja na Mashirika ya Kimataifa kushirikiana na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utekelezaji wake. Uamuzi huu una manufaa makubwa kwa nchi yetu, ikiwa ni pamoja na kuimarisha hadhi ya Tanzania kimataifa kama kitovu cha historia ya ukombozi wa Afrika, kuvutia rasilimali na uwekezaji katika uhifadhi na utalii wa urithi, kukuza ajira na utafiti wa kitaaluma, pamoja na kuimarisha elimu ya uzalendo na mshikamano wa Kiafrika kupitia ujumuishaji wa urithi wa ukombozi katika mitaala ya elimu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

### 3.2.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Maendeleo ya Sanaa nchini ina jukumu la kuratibu na kusimamia maendeleo ya Sanaa. Sekta hii ni moja ya maeneo muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu kutokana na mchango wake katika kutoa ajira hususan kwa vijana, kukuza utalii na kuitangaza nchi kimataifa.

Sekta ya Sanaa inahusisha Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania, Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA), Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

#### 3.2.3.1 Idara ya Maendeleo ya Sanaa

**136.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu makuu ni kuandaa, kushauri na kusimamia sera, sheria, mipango na mikakati mbalimbali inayolenga kuleta mageuzi katika ukuaji wa Sekta ya Sanaa hapa nchini. Vipaumbele vya sasa ni kuimarisha miundombinu ya Sanaa, kuimarisha zaidi ulinzi wa hakimiliki, kupambana na uharamia, kulinda maadili katika kazi za Sanaa na kuhakikisha sekta inachangia kikamilifu uchumi wa mhusika mmoja mmoja na katika pato la Taifa. Katika kipindi cha Julai, 2025 na Aprili, 2026 Serikali imeandaa Katiba ya Mfano itakayotumiwa na Mashirikisho na Vyama vya Sanaa nchini kikiwa ni chombo cha kimkakati kinachounganisha mageuzi ya sanaa na maono mapana ya Taifa. Katiba hii itakapoanza kutumika mwaka 2026/2027 inatarajiwa kuwa mwarobaini wa migogoro isiyoisha na kuvifanya vyama na mashirikisho kuwa taasisi imara zinazojitegemea, zinazojisimamia, zenye hadhi sawa na zinazozalisha ajira na mapato. Katiba hizi zilizoandaliwa kwa ushirikiano mkubwa na wadau wenyewe zinatoa usawa katika maeneo muhimu ya uzingatiwaji wa sheria za kitaifa na kimataifa, maadili ya Taifa, elimu, mafunzo na uzoefu kwa viongozi, vipindi vya uongozi, hatma ya mali za Chama na Shirikisho pale uhai wake

utakapokoma, uwazi kwenye mapato na matumizi, mifumo ya mawasiliano pamoja na uzingativu wa hirakia na taasisi nyingine. Taasisi hizi sasa zinakwenda kuwa kiungo muhimu kati ya Serikali na wadau wa kisekta na hivyo kurahisisha mawasiliano na mipango ya maendeleo.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali ilifanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi za BASATA, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, TaSUBa, COSOTA, pamoja na Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania kwa lengo la kuhakikisha mipango ya muda mfupi na muda mrefu inazingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 inayoitambua sekta ya Sanaa na Burudani kama moja ya maeneo ya mageuzi ya kimkakati ya kulifikisha Taifa katika Uchumi wa Dola Trilioni Moja ifikapo mwaka 2050. Miongoni mwa matokeo ya tathmini hii ni kuongezeka kwa ushiriki wa vijana na watoto katika fani mbalimbali za Sanaa; kuimarika kwa mifumo ya kidijiti, kuongezeka kwa ulinzi wa hakimiliki na mapato ya wasanii, pamoja na maboresho ya miundombinu na upatikanaji wa mikopo na ruzuku kwa wadau. Aidha, maadili ya kazi za Sanaa yameendelea kuimarika, huku ukusanyaji wa takwimu ukisaidia kupanga maendeleo ya sekta kwa ufanisi zaidi. Mikakati iliyoafikiwa kujumuishwa katika mipango ya Taasisi ni uimarishaji wa miundombinu ya Sanaa, usimamizi wa hakimiliki, uimarishaji wa mifumo ya utoaji wa huduma kidijiti na uboreshaji wa huduma za kifedha miongoni mwa wadau wetu.

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia utajiri wa asili wa nchi yetu, utamaduni, ukarimu amani, mshikamano na uzoefu uliopatikana kupitia mashindano ya *Miss and Mister Deaf International* yaliyosimamiwa na Serikali hapa nchini mwaka 202I, 2022 na 2023; waandaaji wa mashindano makongwe na makubwa zaidi ya ulimbwende duniani ya Miss World wameshawishika na kukubali Tanzania iwe mwenyeji mwaka 2027. Kati ya Julai 2025 hadi Aprili 2026 waandaaji hao wamefika hapa nchini mara tatu kwa lengo la kuiona nchi, kutembelea vivutio vyake na kujiridhisha na miundombinu yake. Katika ziara hizo, Tanzania imekuwa mwenyeji wa Miss World, Opal Suchata kutoka Thailand, Miss World Africa, Hasset Dereje kutoka Ethiopia na Bi. Julia Evelyn Morley, Mwenyekiti na Mkurugenzi Mkuu wa Miss World Limited. Kutokana na mashindano haya, Tanzania itanufaika kiuchumi kupitia viingilio, huduma kwa wageni, udhamini na mauzoo ya bidhaa kwa wageni; wabunifu wetu kupata kazi na uzoefu; nchi kutangazwa kupitia televisheni na mitandao duniani kote katika nyanja za utalii wa asili na utamaduni; kuimarisha diplomasia na zaidi ya yote kuifanya dunia iamini tena kuwa Tanzania ni mahala salama kwa watu wote. Aidha, kufuatia kuhitimishwa kwa mashindano ya Miss World Tanzania tarehe 19 Aprili, 2026 mlimbwende Bi. Latricia Ian Sawe ameshinda na ataiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Miss World nchini Vietnam mwezi Septemba 2026.



*Bi. Bernice Fernandes ambaye ni mmoja wa Jaji wa Shindano la Miss World Tanzania akimvalisha sashi mshindi wa shindano hilo Bi. Latricia Ian Sawe katika fainali iliyofanyika tarehe 19 Aprili, 2026 Jijini Dar es Salaam.*



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali Bw. Gerson Msigwa akimkabidhi zawadi mshindi wa Shindano la Ulimbwende wa Dunia kwa Tanzania (Miss World Tanzania) Bi. Latricia Ian Sawe katika fainali iliyofanyika Aprili 19, 2026 Jijini Dar es Salaam.*




*Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mheshimiwa Paul Christian Makonda (Mb.) aliposhuhudia utiaji saini Mkataba wa Tanzania kuwa mwenyeji wa Mashindano ya 74 ya Ulimbwende wa Dunia mwaka 2027 (Miss World 2027), tarehe 20 Aprili, 2026 jijini Dar es Salaam.*

**139.** ***Mheshimiwa Spika***, Mashindano ya Miss World 2027 yatatumika kama kichocheo cha hamasa kuelekea AFCON 2027 na kuongeza mwamko wa kitaifa pamoja na ushiriki wa wananchi katika maandalizi ya tukio hilo kubwa la kihistoria barani Afrika.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuratibu Tamasha la Serengeti Music Festival ambalo limekuwa likifanyika kila mwaka tangu 2020 kama jukwaa muhimu la kukuza na kuendeleza vipaji vya wasanii wa Kitanzania kupitia Sanaa ya Muziki kwa ujumla, pamoja na kuwaunganisha Wasanii na masoko ya kitaifa na kimataifa. Kila mwaka, pamoja na malengo yake ya

jumla, tamasha hili huwa na malengo mahsusi ambapo kwa mwaka huu, tamasha hili linalotarajiwa kufanyika tarehe 30 Mei, 2026 linalenga kutumika kama jukwaa la kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika mashindano ya AFCON 2027. Tangu kuanzishwa kwake, tamasha hili lilifikia kilele cha mafanikio mwaka 2025 ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa wakati huo. Kutokana na mchanganyiko mzuri wa waandaaji unaojumuisha Serikali na sekta binafsi hasa kutoka Vyombo vya Habari na Shirikisho la Muziki Tanzania, tamasha hili limekuwa jukwaa la wasanii wote wa Tanzania bara na Zanzibar bila kujali ushindani wao wa kimuziki.

**141.** ***Mheshimiwa Spika**,* katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, Serikali imeendelea kuratibu kwa ufanisi shughuli za uhamasishaji kupitia Sanaa sambamba na michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa ligi za Ndani (African Nations Championship 2024) na maandalizi ya Africa Cup of Nations (AFCON 2027) kwa lengo la kuhamasisha ushiriki wa wananchi, kukuza uzalendo, na kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia Sanaa na burudani. Katika utekelezaji huo, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Sanaa la Taifa na Baraza la Michezo la Taifa iliratibu Tamasha la CHAN-SINGELI lililofanyika tarehe 2 Agosti 2025 katika eneo la nje la Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni sehemu ya sherehe za uzinduzi wa mashindano hayo. Tamasha hili lilikuwa na mafanikio makubwa ambapo zaidi ya wasanii 30 wa muziki wa singeli walipata fursa ya kutumbuiza, wakihamasisha maelfu

ya mashabiki wa soka kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki sherehe hizo. Kupitia jukwaa hilo, Muziki wa singeli uliweza kutangazwa kimataifa kama sehemu ya utambulisho wa utamaduni wa Tanzania.

**142.** ***Mheshimiwa Spika***, katika muktadha huo huo, Serikali iliratibu Tamasha la Muziki Mchanganyiko lililofanyika tarehe 22 Agosti, 2025 katika eneo la nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, jijini Dar es Salaam. Tamasha hili lilikuwa na lengo mahsusi la kuhamasisha wananchi kushiriki kikamilifu katika mashindano hayo, sambamba na kuishangilia Timu ya Taifa wakati wa mchezo wa Robo Fainali dhidi ya Timu ya Taifa ya Morocco.

### 3.2.3.2 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa Sura 204. Majukumu ya BASATA ni pamoja na kufufua na kukuza maendeleo ya sanaa nchini; kufanya tafiti za masuala mbalimbali kuhusu sanaa; kutoa ushauri na misaada ya kitaalamu kwa wasanii na wadau wa sanaa; kusajili wasanii na miundombinu ya sanaa nchini; na kutengeneza kanuni na miongozo ya kusimamia ubora wa kazi za sanaa.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine, ni kuishauri Serikali kuhusu maendeleo ya sanaa nchini; kutunza kanzidata za wasanii na wadau wanaojishughulisha na kazi za sanaa; kuhimiza uzingatiaji wa maadili na tamaduni za Kitanzania katika

kazi za sanaa miongoni mwa wasanii na wadau wa sanaa; kuhamamsisha maendeleo ya sanaa kwa njia ya maonesho, mashindano, matamasha, warsha na semina; kutoa na kuimarisha mipango ya mafunzo kwa wadau wa sanaa; kuhimiza uanzishwaji wa vyama au mashirikisho ya sanaa kwa lengo la kuongeza idadi ya vikundi vinavyojishughulisha na kazi za sanaa; na kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watu, vikundi, taasisi, vyama, au wamiliki wa miundombinu wanaojishughulisha na kazi za sanaa kwa kukiuka Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuonesha dhamira thabiti ya kuendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa njia ya kidigiti. BASATA imeendelea kutekeleza jukumu la kuboresha mfumo wa AMIS (Artist Management Information System) na kuunganisha na mifumo mingine ya Serikali kama vile TRA Portal, NIDA, BRELA, GePG, TAUSI, NaPA, Mfumo wa Hakimiliki (CRIMIS) pamoja na NeST ili kurahisisha upatikanaji na ubadilishanaji wa taarifa mbalimbali. Aidha, ili kufanikisha azma hiyo, BASATA imeingia mkataba na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) kwa ajili ya kuboresha mfumo wa AMIS pamoja na kutengeneza programu tumizi ya simu (BASATA Mobile App) ambayo itarahisisha zaidi upatikanaji wa huduma za BASATA kwa njia ya kidigiti. Pia, Baraza limefanya mapitio ya kina ya mfumo wa biashara wa BASATA (Business Process System Review) yaliyolenga kuboresha taratibu za utoaji huduma, kuongeza uwazi, kupunguza urasimu na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa haraka na kwa

ufanisi zaidi kwa wasanii na wadau wa sanaa.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuhakikisha inawafikia wasanii wote nchini, BASATA imeendelea kukusanya na kuhifadhi takwimu za usajili wa wasanii, vikundi na taasisi za sanaa nchini ambapo hadi Aprili 2026 jumla ya wasanii 21,875 wamesajiliwa ikilinganishwa na wasanii 1,935 waliosajiliwa mwaka wa fedha 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 91. Takwimu hizi hutumika kama msingi muhimu katika kufanya tafiti, kuandaa mipango na kusaidia Serikali katika kufanya maamuzi ya kisera yanayolenga kuendeleza sekta ya sanaa na ubunifu nchini.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kupongeza Serikali kwa kuweka mazingira wezeshi ya kufanya shughuli za sanaa. Aidha, BASATA imeendelea kuratibu na kusimamia matamasha pamoja na utoaji wa Tuzo za Muziki kwa lengo la kutambua na kuthamini mafanikio ya wasanii nchini. Hatua hii inalenga kuhamasisha ubunifu, kuongeza ushindani chanya miongoni mwa wasanii na kukuza maendeleo ya sekta ya sanaa nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 Wizara kupitia BASATA imefanikiwa kuratibu na kusimamia jumla ya matukio 25 kati ya matukio 27 yaliyokuwa yamepangwa kufanyika, ambayo ni sawa na asilimia 93 ya utekelezaji. Baadhi ya matukio hayo ni Bongo Flava Honors lililofanyika tarehe 02 Agosti, 2025 jijini Dar es salaam), Matukio ya Ubunifu na Mitindo (Swahili Fashion Week and awards lililofanyika tarehe 5 hadi 7, Desemba 2025 jijini Dar es Salaam; Shindano la Miss Grand International

lililofanyika tarehe 18 Octoba, 2025 jijini Dar es Salaam; Shindano la Miss Universe lililofanyika tarehe 23 Agosti, 2025 jijini Dar es Salaam; na AFA Fashion Night lililofanyika tarehe 5 Disemba 2025 jijini Dar es Salaam), CIGOGO Music Festival lililofanyika tarehe 27 Julai, 2025 Chamwino, Dodoma. Aidha, BASATA imeendelea kuwawezesha wasanii chipukizi hasa vijana kwa kuanzisha programu mbalimbali za sanaa ikiwemo *BASATA Rising Star Award* iliyozinduliwa tarehe 27 Februari 2026. Lengo la Programu hii ni kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wasanii chipukizi ambapo kila mwezi tuzo ya nyimbo bora ya mwezi ya msanii chipukizi hutolewa.

**148.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya sanaa ni mhimili muhimu katika kukuza uchumi wa ubunifu na ajira kwa vijana wetu. BASATA imeandaa miongozo 7 kwa ajili ya usimamizi wa Shughuli za Sanaa ambayo ni Mwongozo wa Usuluhishi wa Migogoro ya Wasanii na Wadau wa Sanaa; Mwongozo wa Ulinzi wa Mtoto Msanii katika Sanaa; Mwongozo wa Uendeshaji wa Matukio ya Sanaa; Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashindano ya Uchoraji; Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashauri ya Kimaadili; Mwongozo wa Kamati za Sanaa za Mikoa na Kamati za Sanaa za Wilaya; na Mwongozo wa Uendeshaji wa Mashindano wa Ngoma za Asili. Miongozo hii imesaidia kurahisisha usimamizi wa shughuli za sanaa, kupunguza migogoro katika sekta ya sanaa, kuimarisha ubora wa kazi za sanaa, kuimarisha hadhi ya sanaa ya Tanzania kimataifa, kuongeza tija na kulinda maslai ya wasanii na kufungua fursa mpya za kiuchumi.

**149.** ***Mheshimiwa Spika***, BASATA imekuwa ikipokea migogoro ya wasanii kupitia dawati la usuluishi linalosimamiwa na Kitengo cha Huduma za Sheria katika kushauri na kutoa msaada wa kisheria kulingana na changamoto mbalimbali zinazowakumba wasanii. Hadi Aprili 2026 jumla ya migogoro 20 imepokelewa, migogoro 10 imetatuliwa na migogoro 10 inaendelea na taratibu za utatuzi.

**150.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulikumbusha Bunge lako tukufu kuwa sanaa ni kioo cha maadili ya jamii yetu. Pale ambapo sanaa inapoteza mwelekeo Taifa nalo hupoteza dira**.** Hivyo kamwe hatutokubali sanaa iwe chanzo cha kuporomoka kwa maadili ya Taifa letu. Kutokana na hali hiyo, BASATA imefanya maboresho ya Kanuni za BASATA za mwaka 2018 ili ziendane na mabadiliko ya sheria ya BASATA ya mwaka 2019 na taratibu za mwisho za kukamilisha Kanuni hizo zinaendelea na zinatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2026. Kanuni hizi zimeboreshwa ili kuweka misingi imara ya maadili, kupunguza au kufuta kabisa tozo na ada, kuimarisha uwajibikaji wa wasanii na kuhakikisha kazi za sanaa zinachangia kujenga jamii yenye maadili mema. Aidha, maboresho hayo ya Kanuni yanaimarisha zaidi dhana ya sasa ya Serikali ya uwezeshaji sekta badala ya udhibiti.

**151.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na uwezeshaji huo, BASATA limekuwa likichukua hatua mbalimbali kwa wasanii wanaokiuka maadili. Aidha, wakati

mwingine BASATA imekuwa ikijielekeza zaidi kwenye kutoa elimu kama mbadala wa hatua za kinidhamu kwa wasanii wasiozingatia maadili na katika kipindi hicho, BASATA imewafikia zaidi ya wasanii 1,437 kwa lengo la kuwapa elimu ya uzingatiaji wa maadili katika kazi za Sanaa na kutoa adhabu kwa wasanii 10 kutokana na kutozingatia maadili katika kazi zao kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 25 ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa.

#### 3.2.3.3 BODI YA FILAMU TANZANIA (TFB)

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza Tanzania ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura 230, ikiwa na jukumu la kusimamia, kuendeleza na kukuza tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini. Kupitia Taasisi hii, Serikali imeendelea kuweka mazingira bora ya ukuaji wa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza ambayo imeendelea kuwa moja ya sekta muhimu katika kukuza uchumi na ubunifu, kuongeza ajira kwa vijana na kuitangaza Tanzania kimataifa.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuipa kipaumbele tasnia ya sanaa na ubunifu kwa kutambua mchango wake katika maendeleo ya uchumi wa Taifa. Katika muktadha huo, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ya kukuza sekta za ubunifu ili ziwe chanzo kikubwa cha ajira na kipato kwa Watanzania.

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuweka majukwaa muhimu ya kutambua, kukuza na kuendeleza wasanii hususan wa filamu na michezo ya kuigiza nchini, Wizara kupitia Bodi ya Filamu imeratibu Tamasha na Tuzo za Filamu (TAFFA) linalofanyika kila mwaka ambalo hadi sasa ni msimu wa nne tangu kuanzishwa kwake. Malengo makuu ya tamasha hili ni kuanzisha na kuratibu program za kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya utamaduni na sanaa ikiwemo filamu na michezo ya kuigiza ili kuongeza hamasa kwa wanatasnia kuzalisha kazi zenye ubora na kusisimua masoko na fursa ya uwekezaji katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza.

**155.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha hili la kipekee nchini lenye dhima ya 'Filamu ni Biashara' lililohusisha matukio kama midahalo, warsha na mafunzo kwa wadau wa filamu na michezo ya kuigiza lilifanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 03 Julai, hadi 16 Agosti, 2025 ambapo jumla ya wadau 1,600 walishiriki zikiwemo nchi za Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Somalia, Uganda, Rwanda na Nchi kutoka nje ya Afrika ambazo ni Uswizi na Marekani. Ushiriki huu umeendelea kufungua milango ya ushirikiano wa kimataifa na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza duniani.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha hilo lilihitimishwa kupitia kilele cha usiku wa Tuzo za Filamu kilichofanyika tarehe 14 Februari, 2026 Jijini

Dar es Salaam ambapo jumla ya wadau 1,226 walishiriki. Jumla ya tuzo 28 zilitolewa katika tamasha hilo. Kati ya tuzo hizo, 26 zilikuwa za ushindani (Categorical Awards) zenye kuleta chachu ya ubunifu katika vipengele tofauti na mbili (2) zilikuwa za heshima (Lifetime Achievement Awards) zilizotolewa kwa wadau walioweka alama na kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini kwa kipindi cha muda mrefu.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Bodi ya Filamu imeendelea kuratibu na kushiriki katika matamasha na maonesho mbalimbali kwa lengo la kuitangaza tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza kitaifa na kimataifa. Matamasha hayo ni pamoja na *Kigamboni Festival* lililofanyika tarehe 06 Julai, 2025 katika Wilaya ya Kigamboni jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau 600. Katika tamasha hilo, jumla ya Tuzo 25 zilitowela ambapo Tuzo 12 zilikuwa za ushindani na Tuzo 13 zilikuwa za heshima *(Lifetime Achievement Awards)*.

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, tamasha la *Sauti Zetu Film Festival* ambalo lilikuwa na kauli mbiu ya "kupeleka sinema kwa watu" lilifanyika tarehe 05 hadi 13 Septemba, 2025 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Morogoro na Pwani. Tamasha hili lilikuwa na lengo la kutoa mafunzo ambapo jumla ya wadau 20 walishiriki kuhusu namna ya kuomba fedha za miradi katika utayarishaji wa filamu pamoja na kuonesha filamu zenye jumbe za kuelimisha jamii kwa kutumia nguvu ya sinema katika kuhamasisha mabadiliko

chanya na kutetea haki za binadamu. Kilele cha tamasha hilo kilifanyika tarehe 15 Oktoba, 2025 jijini Arusha. Vilevile, tamasha *la Iringa Film Festival* lililofanyika tarehe 13 Disemba, 2025 katika Mkoa wa Iringa ambapo mgeni rasmi alikua Mhe. Benjamin Sita, Mkuu wa Wilaya ya Iringa na kuhudhuriwa na wadau 850 na kauli mbiu ya "Uwekezaji katika Sanaa ni kukuza Utalii". Katika tamasha hilo, jumla ya tuzo 20 zilitolewa ambapo tuzo 16 zilikuwa za ushindani (Categorical Awards) na nne (4) zilikuwa za heshima *(Lifetime Achievement Awards)*.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwajengea uwezo wasanii wa filamu na michezo ya kuigiza kupitia programu mbalimbali za mafunzo. Programu hizo ni pamoja na *Mtaa kwa Mtaa*, *Tailor Made Training* pamoja na *Film Screening Sessions* ambazo zimeendelea kuwajengea uwezo wasanii katika maeneo mbalimbali ya kitaalamu. Fauka ya hayo, kupitia programu hizo, jumla ya wasanii 906 walipata mafunzo katika fani mbalimbali ikiwemo uongozaji wa filamu, uigizaji, uandishi wa miswada, uhariri wa picha pamoja na upigaji picha. Mafunzo haya yameendelea kuchangia kuimarika kwa ubora wa kazi za filamu zinazozalishwa nchini.

**160.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza iliratibu na ilishiriki katika mafunzo ya kuwajengewa uwezo watumishi na wadau wa filamu ambayo yalifanyika kuanzia tarehe 07 hadi 20 Septemba, 2025 nchini Korea Kusini. Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Korea (KOICA)

ikiwa na jumla ya washiriki 15 ikijumuisha wadau wa filamu wanne (4), Watumishi 10 kutoka Bodi ya Filamu na mtumishi mmoja (1) kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi imeendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali ikiwemo Kituo cha Sayansi na Utamaduni cha Urusi nchini; Ubalozi wa China pamoja na Kituo cha Utamaduni wa China; Tanga Yetu kupitia mradi wake wa Global Opportunity Youth Network (GOYN) kwa kushirikiana na Jiji la Tanga. Kupitia ushirikiano huo, Bodi imewajengea uwezo wanatasnia wa Mkoa wa Tanga na mikoa ya jirani ili kuwawezesha vijana kupata fursa za ajira, kujiongezea kipato, kupata mikopo, kuanzisha biashara endelevu na kuchangia ukuaji wa uchumi wa jamii zao na nchini kwa ujumla ambapo hadi Aprili 2026 Bodi imefanikiwa kusaidia kuandaa Mpango Mkakati wa filamu (Tanga Film Strategic Plan) wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2026/27 hadi 2030/31 ya kuifanya Tanga iwe kitovu cha utengenezaji wa filamu nchini.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha tasnia ya filamu inaendelea kukua kwa kuzingatia maadili, sheria na utamaduni wa Taifa letu, Bodi ya Filamu imeendelea kusimamia maudhui ya filamu na michezo ya kuigiza ili kukidhi viwango vya ubora vya kitaifa na kimataifa kwa kuhakiki na kupanga madaraja kabla ya kurushwa kwa hadhara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 Bodi imehakiki na kupanga madaraja kwa filamu na tamthilia 206 sawa na asilimia 103 ya lengo la filamu na tamthilia 200 pamoja na

jumla ya sehemu (Episodes) 1,126 kati 1,500 sawa na asilimia 75 ya lengo ambapo kazi 124 zilikua filamu na tamthilia za ndani ya nchi na 82 zilikua filamu na tamthilia kutoka nje ya nchi.

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, hakukua na filamu wala tamthilia iliyowasilishwa Bodi ambayo ilikiuka maadili, sheria na utamaduni wa Taifa. Wizara kwa kushirikiana na Bodi imeendelea kuonya, kukemea na kudhibiti maudhui potofu kwa wanatasnia wa filamu na michezo ya kuigiza hasa yanayorushwa mitandaoni bila kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki na kupangiwa madaraja. Vikao mbalimbali vya kinidhamu vimekuwa vikifanyika kwa kushirikisha Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ili kulinda maadili, amani, umoja na mshikamo wa Taifa letu. Sambamba na hayo, Bodi imeendela kufanya maboresho ya Sheria ya Filamu na Michezo ya Kuigiza, Sura 230 kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili Sheria ziendane na mabadiliko ya teknolojia yanayokua kwa kasi katika mnyororo wa tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini.

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha mazingira ya uwekezaji katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wanatasnia juu ya urasimishaji kwa kutumia vyombo mbalimbali kama televisheni, redio na mitandao ya kijamii ili kufuata taratibu za kutambulika rasmi katika tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza kwa kujirasimisha kidijiti katika Mfumo wa *Artist Management Information System* (AMIS) ambapo

wanatasnia wanaweza kujirasimisha kokote waliko nchi bila kufika katika ofisi za Bodi. Jumla ya vitambulisho 148 vimetolewa sawa na asilimia 49 ya lengo la vitambulisho 300. Pia, vibali 103 vimetolewa sawa na asilimia 34 ya lengo la vibali 300. Kati ya vibali vilivyotolewa, vibali 56 vilitolewa kwa wazalishaji wa ndani na 47 vilitolewa kwa wazalishaji kutoka nje ya nchi.

**165.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa ujumla, utekelezaji wa majukumu haya unaonesha dhamira thabiti ya Serikali ya kuendelea kukuza tasnia ya filamu na michezo ya kuigiza nchini ili iweze kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya uchumi wa taifa, kuongeza ajira kwa vijana pamoja na kuitangaza Tanzania kimataifa kupitia sanaa na utamaduni.

### 3.2.3.4 TAASISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**166.** ***Mheshimiwa Spika*,** Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) ilianzishwa kwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Sura ya 218 (Rekebu ya mwaka 2023). Majukumu ya Ofisi ya Hakimiliki Tanzania ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya Watunzi, Waandishi, Wasanii, Wafasiri, Watayarishaji wa kurekodi sauti, Watangazaji, Waongozaji na Wachapishaji kwa kulinda haki zao; kusaidia uanzishwaji na kusimamia Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha (Collective Management Organizations - CMOs); na kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu. Aidha, Ofisi hii ina jukumu la

kutunza rejista ya kazi za wasanii na vyama vya watunzi, wasanii, wafasiri, watayarishaji wa sauti zilizorekodiwa, watangazaji na wachapishaji.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kwamba Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha zinasimamiwa ipasavyo, COSOTA imetekeleza mojawapo ya jukumu lililopangwa kwa mwaka 2025/26 ambalo ni kusimamia Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha katika madaraja ya kazi za muziki na kazi za maandishi. COSOTA imeainisha madaraja manne (4) ya wadau wa sanaa na ubunifu ambayo yanastahili kuwa na kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha. Madaraja hayo ni ya muziki, filamu, kazi za maandishi, sanaa za maonesho na ufundi. Katika kutelekeza jukumu hili COSOTA imetoa leseni kwa Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha (Collective Management Organizations - CMOs) katika madaraja mawili (2) ya muziki na kazi za maandishi. Leseni hizi zimetolewa kwa kampuni ya Society of Music Advocacy (SOMA) kwa kazi za muziki na Tanzania Reproduction Rights Society (TANRRS) kwa kazi za maandishi. Aidha, COSOTA imeratibu uanzishwaji wa CMOs katika daraja la filamu na taratibu za utoaji wa leseni ya uendeshaji zipo katika hatua ya tathmini ya maombi. Ofisi inaendelea kuhamasisha wadau kuanzisha na kusajili CMO katika madaraja ya sanaa za maonesho na sanaa za ufundi ili kuhakikisha kuwa ukusanyaji wa mirabaha unafanyika kikamilifu.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa kampuni za kukusanya na kugawa mirahaba (CMOs)

zinatekeleza majukumu yake kwa ufasaha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026, COSOTA imewajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao na kuzingatia Sheria na Kanuni; kufanya uchambuzi wa taarifa za kibenki za mirabaha iliyokusanywa na Kampuni ya daraja la Muziki ya SOMA; na kufanya mapitio ya Viwango vya tozo (tariff rates) vya Kampuni ya TANRRS kwa ajili ya utoaji leseni kwa watumiaji wa kazi za maandishi.

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Serikali inakusanya Mirabaha kikamilifu na wasanii wananufaika na kazi zao, Wizara kupitia COSOTA iliendelea kufuatilia ukusanyaji wa tozo ya hakimiliki (Copyright Levy) kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambapo jumla ya kiasi cha shilingi 522,596,890.57 kimekusanywa kwa kipindi cha mwezi Julai 2025 hadi Aprili 2026. COSOTA inaratibu mgao wa fedha zitokanazo na Tozo ya Hakimiliki ambapo jumla ya shilingi 988,656,103.92, sawa na asilimia 60 ya makusanyo yote ya shilingi 1,647,760,173.20 yaliyofanyika kuanzia Septemba 2023 hadi Juni 2025 ambazo zitagawiwa kwa wabunifu wa kazi za sanaa na uandishi. Mchanganuo wa mgao ni daraja la muziki asilimia 20, filamu asilimia 15, sanaa ya uandishi asilimia 10, sanaa za ufundi asilimia 7.5 na sanaa za maonesho asilimia 7.5.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inathamini sana mchango wa tasnia ya sanaa na Ubunifu katika kukuza pato la Taifa, pia inawathamini wabunifu wote pamoja na mchango wao katika maendeleo ya sanaa nchini.

Hivyo, COSOTA imeendelea kutekeleza mkakati wa kupambana na uharamia wa kazi za ubunifu kwa kufanya operesheni maalumu, kutoa elimu na kushughulikia malalamiko/migogoro. Jumla ya programu za elimu kwa umma nane (8) na operesheni mbili (2) zimefanyika. Tarehe 30 Januari hadi 9 Februari, 2026 COSOTA ilifanya oparesheni ya uharamia katika mkoa wa Mwanza ambapo mtuhumiwa mmoja (1) alikamatwa na jalada la uchunguzi lilifunguliwa. Aidha, kwa kushirikiana na Kampuni ya MultiChoice Tanzania pamoja na Jeshi la Polisi Tanzania, COSOTA imefanya doria mtandaoni na kukamata maharamia wawili (2) ambao walikiri makosa na kulipa faini ya shilingi 2,000,000 kwa mujibu wa Kanuni ya Hakimiliki na Hakishiriki ya Ufifilishaji wa Makosa *(Copyrights and Neighbouring Rights (Compounding of Offenses)* za mwaka 2020. Pia, ili kuhakikisha wabunifu na watu wote wanaohusika na tasnia hii wanasikilizwa na kutatuliwa kero zao ipasavyo kupitia dawati la malalamiko, COSOTA imepokea na kusikiliza jumla ya migogoro 28 ambapo 21 imesuluhishwa na saba (7) inaendelea na usuluhishi.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu jingine la COSOTA ni kukusanya na kugawa mirabaha kwenye maeneo ambayo hayana Kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha. Ili kufanikisha jukumu hili kwa ufanisi mkubwa, COSOTA ilianza mchakato wa kuandaa Kanuni za kutekeleza jukumu hili kwa madaraja ya filamu, sanaa za maonesho na sanaa za ufundi. Hadi Aprili 2026, Wizara kwa kushirikiana na COSOTA imeandaa rasimu ya Kanuni ya vielelezo vya kusikia na

kuona (*Audiovisual Regulations*) ili kuwezesha kukusanya na kugawa mirabaha kwa upande wa kazi za filamu. Aidha, Wizara kupitia COSOTA, ilifanikiwa kuandaa Kanuni ya haki ya kunufaika na mauzo endelevu (Resale rights) kwa ajili ya kusimamia kazi za sanaa za ufundi na maonesho zinapouzwa kwa mara ya pili na kuendelea.

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha usimamizi wa Hakimiliki nchini unawanufaisha wabunifu nchini, COSOTA imewasilisha mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Hakimiliki na Hashiriki Na 7 ya mwaka 1999 kupitia Sheria ya Fedha ili kuhakikisha inakidhi mabadiliko ya teknolojia pamoja na kufuata miongozo ya kimataifa ambayo Tanzania tumeridhia. Mabadiliko hayo yatahusisha kuongeza kiwango cha asilimia inayotozwa pamoja na idadi ya vifaa vinavyotumika kuzalisha, kuhifadhi, kunakili na kusambaza kazi za wabunifu. Hali hii itawezesha kuongezeka kwa makusanyo ya mirabaha yatokanayo na Tozo ya Hakimiliki na hatimaye kuwezesha ugawaji wa mirabaha kwa kiwango kikubwa na hivyo wabunifu kunufaika na kazi zao.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita ina nia thabiti ya kuhakikisha kuwa wasanii na wabunifu katika madaraja mbalimbali kote nchini wanakuwa na uelewa kuhusu masuala ya Hakimiliki. COSOTA ilitoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya hakimiliki kwa mwaka 2025/26 kwa kuzingatia mpango wa utoaji elimu ya hakimiliki na hakishiriki kwa umma wa mwaka husika. COSOTA ilitoa elimu iliyowezesha

kuanzishwa kwa kampuni za kukusanya na kugawa mirabaha, elimu kwa viongozi wa Shirikisho la Filamu ili waweze kuanzisha CMOs katika daraja la kazi zao. Aidha, elimu ilitolewa kupitia vyombo vya habari ambapo hadi Aprili 2026 jumla ya vipindi 15 vilitayarishwa na kurushwa kwa hadhara kupitia stesheni za EFM Redio, TBC Taifa, Redio One, Rick Media Online Tv, Wasafi Online Tv, Crown FM, Uhai Fm Redio, Azam TV, Furaha FM na ITV jijini Dar es Salaam. Vilevile vipindi 8 vilitayarishwa na kurushwa kupitia redio za AFM, CFM, Dodoma FM, Point FM, TBC redio jamii , Ngassa Online TV, Millard Ayo Tv na Jambo online TV jijini Dodoma.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** fauka na hayo, COSOTA ilitoa elimu ya hakimiliki Jijini Dar es Salaam na Dodoma katika matukio mbalimbali kama vile Tamasha la Samia Master Class, maadhimisho ya Maonesho ya Kimataifa ya Vitabu ambapo wageni 120 waliofika kwenye banda walipatiwa elimu. Maeneo mengine ni Mkutano Mkuu wa wadau wa sanaa za Maonesho Tanzania ambao ulifanyika TaSUBa na wadau 100 walipatiwa elimu. Aidha, wadau wa sanaa waliopatiwa elimu ya hakimiliki ni pamoja na Shirikisho la Kazi za Maandishi Dar es Salaam, Wanafunzi 200 wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo TaSUBa tarehe 5 Desemba, 2025, Kampuni ya kukusanya na kugawa mirabaha kwa kazi za Muziki ya Society of Music Advocacy (SOMA), wanafunzi 150 kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) pamoja na vijana 450 wa kikundi cha "Vijana Innovation" mwezi Februari, 2026. Aidha, tarehe 2 hadi 3 Februari 2026 COSOTA ilitoa

elimu kwa Wanafunzi 50 wa DIT, na Januari 2026 wanafunzi 100 kutoka Chuo cha Kilimo na Uvuvi (LITA), Wasanii 113 wa sanaa za Ufundi wa chama cha wasanii wachongaji (CHAWASAWATA) walipatiwa elimu ya hakimiliki tarehe 24 Januari, 2026 Dar es Salaam. Watayarishaji wa kazi za sanaa (Producers) 130 walipatiwa elimu Machi 18, 2026 katika kituo cha Urithi wa Ukombozi na Benjamini Mkapa walipatiwa elimu ya hakimiliki. Tarehe 11 Machi, 2026 elimu kuhusu Hakimiliki na namna ya kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu ilitolewa kwa Maafisa 721 wa Chuo cha Dar es Salaam Police Academy Kurasini. Pia, COSOTA imetoa elimu kwa umma kwa njia ya mitandao ya kijamii ambapo jumla ya vibango 23, na makala jongefu mbili (2) za elimu ya hakimiliki vimetolewa na kusambazwa katika mitandao ya kijamii ya Instagram, Whatsapp na Facebook. Aidha, elimu ilitolewa jijini Dodoma kwa Wahadhiri 17 na wanafunzi 18 wa Chuo cha mipango Dodoma (IRDP) walipatiwa elimu ya Hakimiliki, Maafisa Utamaduni wa jiji na mkoa wa Dodoma, Jeshi la Polisi kitengo cha Makosa ya jinai (DCI), Wamiliki wa baa na Hoteli pamoja na viongozi wa Chemba ya Taifa ya Biashara (TNCC).

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa kwenye usimamizi na ulinzi wa hakimiliki na hakishiriki**,** COSOTA ilishirikiana na Taasisi za ndani nne (4) ambazo ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika kukusanya Tozo ya Hakimiliki, Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa) kutoa elimu ya hakimiliki pamoja na kufanya usajili wa kazi za Sanaa, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika

kuweka mpango mkakati wa kupambana na uharamia wa kazi za wabunifu kidijitali, pamoja na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutekeleza mradi wa "*IP School Club*" na kutoa elimu ya Hakimiliki kwa Walimu 20 waliosajiliwa pamoja na Wanafunzi 100 katika shule tano (5) za Sekondari ambazo ni Makongo, na St. Joseph zilizopo Dar es Salaam, Tanga Technical iliyopo Tanga, Sikirali iliyopo Kilimanjaro pamoja na Kiembesamaki Zanzibar.

**176.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika ngazi ya kimataifa, COSOTA ilishirikiana na mashirika ya kimataifa matano (5) kwa lengo la kukuza ushirikiano wa kimataifa kwenye usimamizi na ulinzi wa hakimiliki na hakishiriki. Mashirika hayo ni; Shirika la Kikanda la Miliki Bumifu Afrika (African Regional Intellectual Property Organization - ARIPO); Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Waandishi na Watunzi (International Confederation of Societies of Authors and Composers - CISAC) ambapo tarehe 12 Desemba, 2025 Ofisi ilishiriki katika kikao kazi cha *Working Licensing Africa* kwa lengo la kujengewa uwezo juu ya kusimamia masuala ya utoaji leseni kwa vyombo mbalimbali vinavyorusha na kupokea matangazo. Pia, COSOTA ilishiriki kikao cha 7 na 8 cha Kamati ya Haki za Miliki Bunifu (Committee on Intellectual Property Rights) kujadili itifaki za Miliki Bunifu (IPR Protocols) ikiwemo itifaki ya hakimiliki kwenye Eneo Huru la Biashara Afrika (African Continental Free Trade Area - AfCFTA) uliofanyika tarehe 20 Julai hadi tarehe 02 Agosti, 2025 nchini Djibouti kuhakikisha masuala ya Hakimiliki na Hakishiriki yanasimamiwa na kuzingatiwa vyema.

Aidha, COSOTA ilishiriki kongamano lililofanyika Harare Zimbabwe 21 Oktoba, 2025 lilioandaliwa na Shirika la Kikanda la Miliki Bunifu Afrika (ARIPO) kuhusu namna bora ya kushirikiana kwa kuzingatia mifumo ya Sheria na Sera za kusimamia masuala ya Hakimiliki. Pia COSOTA ilishiriki Mkutano wa Kimataifa wa Hakimiliki wa mwaka 2025 (2025 International expo and China Copyright forum) ulioandaliwa kwa pamoja na "National Copyright Administration of China" (NCAC), CISAC, na Shirika na Miliki Bunifu Duniani (World Intellectual Property Organization - WIPO) tarehe 13 - 17 Oktoba, 2025 katika mji wa Qingdao - China, kwa lengo la kujadili mchango wa sekta ya ubunifu na mifumo ya Hakimiliki katika kuchochea maendeleo na mabadiliko ya kidigiti.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha kuwa Serikali ina kanzi data ya wabunifu wote nchini pamoja na kazi zao, COSOTA imeendelea kutekeleza jukumu lake la kusajili kazi za kibunifu na wabunifu ambapo jumla ya kazi 959 zilisajiliwa na pia wabunifu 316 walisajiliwa kuanzia Julai 2025 mpaka Aprili 2026. Vilevile, katika kuhakikisha kuwa kanzidata hiyo ni salama na wabunifu wanaweza kujisajili popote watakapokuwa, COSOTA imekamilisha ujenzi wa mfumo wa usajili wa kazi za ubunifu yaani Copyright Registration Management Information System (CRMIS) ambao uliwezesha kuunganishwa na mfumo wa usajili wa AMIS wa BASATA, NIDA na NaPA.

### 3.2.3.5 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania umeanzishwa kwa Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini (Trustees' Incorporation Act 2002) iliyorejelewa mwaka 2023 kupitia Sura 318 (CAP. 318 R.E. 2023) na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 Septemba, 2020. Lengo la uanzishwaji wake ni kuinua ubora wa kazi za Utamaduni na Sanaa ili zijiendeshe kibiashara, kuzalisha ajira na kuchangia pato la Taifa. Mfuko unatoa huduma za mitaji kwa wadau wa Utamaduni na Sanaa kupitia mikopo yenye masharti nafuu, huwajengea uwezo kwa kutoa mafunzo mbalimbali husuan yanayohusika na urasimishaji wa kazi zao, elimu ya fedha, masoko, uwekezaji pamoja na hifadhi ya jamii.

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Utamaduni na Sanaa unawezesha upatikanaji wa mikopo kwa wasanii kwa kushirikiana na Taasisi za Fedha ambazo ni Benki ya CRDB na NBC. Mfuko uliamua kushirikiana na Taasisi hizo katika utoaji wa huduma hii ili kutumia miundombinu ya Ofisi za matawi ya Benki yaliyoenea nchi nzima. Lengo likiwa ni kupunguza gharama za uendeshaji ambapo ili kuwafikia wasanii wengi Mfuko ungelazimika kuwa na Ofisi hadi katika ngazi ya Wilaya, kuwa na watumishi wengi na vitendea kazi vya kutosha kama vile magari, kompyuta, viti, meza, n.k. Kutumia wataalamu wa Benki walio na uzoefu katika ukaguzi wa miradi, utoaji wa mikopo, ufuatiliaji wa marejesho na usimamizi wa mikopo, kwa ujumla pamoja na kuulinda

mtaji ili ukue, uwe endelevu na hatimaye uweze kuwafikia wasanii wengi zaidi ilikuwa ni lazima Mfuko uingie makubaliano na Benki.

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mfuko imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.535 kwa miradi 229 ya Utamaduni na Sanaa. Aidha, Sekta zilizonufaika na mikopo hiyo ni Filamu (miradi 61) imewezeshwa shilingi 1,008,133,655.91, Ufundi (miradi 68) imewezeshwa shilingi 1,268,433,172.05; Maonesho (miradi 45) imewezeshwa shilingi 525,372,235.95, Muziki (miradi 44) imewezeshwa shilingi 433,060,936.09 na Lugha na Fasihi (miradi 11) imewezeshwa shilingi 300,000,000.

**181.** ***Mheshimiwa Spika***, kupitia miradi 229 iliyowezeshwa, miradi 55 inayomilikiwa na Makampuni iliwezeshwa shilingi 1,088,662,802.42, miradi 48 inayomilikiwa na vikundi iliwezeshwa shilingi 613,745,732.53, miradi 59 inayomilikiwa na Wanawake iliwezeshwa shilingi 595,322,866.26 na miradi 67 inayomilikiwa na Wanaume iliwezeshwa shilingi 1,237,268,598.79. Aidha, Miradi iliyowezeshwa imefikia Mikoa 15 ambayo ni Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Manyara, Arusha, Mwanza, Kagera, Shinyanga, Mara, Geita, Mbeya, Njombe, Kilimanjaro, Ruvuma, na Tabora. Halikadhalika, kupitia miradi iliyowezeshwa jumla ya ajira 75,537 zimezalishwa na kuwanufaisha wananchi 971,285.

**182.** ***Mheshimiwa Spika***, matokeo ya uwezeshaji wa mitaji kwa wasanii yamesaidia ununuzi wa vifaa kwa

studio 72 za Muziki na Filamu, ununuzi wa vifaa kwa vyuo kumi na moja (11) vya kati vilivyosajiliwa na Serikali katika ngazi ya Cheti, Diploma na kozi fupi kwa ajili ya kutoa elimu ya ujuzi kwa fani mbalimbali kama vile ushonaji, mapambo, ususi, upishi nk. Vyuo hivi vimezalisha wasanii 3,579, ununuzi wa majukwaa ya kisasa kumi (10) yanayotumika katika hafla mbalimbali hususani mikutano mikubwa. Aidha, uwezeshaji huo umechagiza uzalishaji wa Filamu 287 ambapo filamu 253 zimekubalika katika vituo vya Televisheni vya DSTV, Azam TV, Star Times na ZUKU na uzalishaji wa sehemu (episodes) kwa tamthilia tisa (9) zinazoendelea kurushwa katika vituo vya Televisheni vya DSTV na Azam TV. Halikadhalika, utengenezwaji wa nyimbo za audio 107 na video 85 za Muziki pamoja na kukua kwa utalii wa kiutamaduni katika Mkoa wa Arusha kupitia uwezeshaji wa mitaji kwa wasanii wa Sanaa za Ufundi katika Soko la Maasai ambalo limekuwa kichocheo na kivutio cha utalii katika Mkoa wa Arusha.

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko umewezesha upatikanaji wa mafunzo ya urasimishaji, uendelezaji wa biashara na ushauri wa kibiashara kwa wasanii kwa lengo la kuwaimarisha katika usimamizi wa shughuli zao za sanaa, kuwakutanisha wasanii ili kubadilishana mawazo na uzoefu pamoja na kuwasaidia kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa kazi zao. Mfuko kwa kushirikiana na wadau umewajengea uwezo wasanii 11,556 ambao kati yao wanawake ni 6,125 sawa na asilimia 53 na wanaume ni 5,431 sawa na asilimia 47 kutoka mikoa 11 ambayo ni Wasanii 1,140 - Dodoma, Wasanii 2,235 Dar es Salaam, Wasanii

338 - Geita, Wasanii 724 - Kagera, Wasanii 531- Mara , Wasanii 1,224 - Mwanza, Wasanii 1,178 - Mtwara, Wasanii 1,277 - Shinyanga, Wasanii 627 – Tabora, Wasanii 753 - Arusha na Wasanii 1,529 - Tanga. Aidha, mada zilizofundishwa ni umuhimu na aina za urasimishaji, elimu ya fedha, masoko, uwekezaji, usimamizi na uandishi wa miradi pamoja na hifadhi ya jamii.

**184.** ***Mheshimiwa Spika***, urasimishaji wa wasanii na kazi zao una umuhimu mkubwa katika kuimarisha utambuzi, ulinzi na usalama wa kazi za wabunifu, kujenga uaminifu kwa wadau na wawekezaji katika sekta ya sanaa, sambamba na kutambua mchango wao katika kukuza uchumi wa Taifa na kuendeleza utambulisho wa jamii. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara kupitia Mfuko imechochea urasimishaji wa kazi za sanaa kwa jumla ya wasanii 5,627 katika Mamlaka mbalimbali. Hatua hizo zilijumuisha ufunguaji wa akaunti 3,275 za benki, usajili wa wasanii 749 kupitia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), usajili wa wasanii 573 kupitia Bodi ya Filamu, usajili wa majina 103 ya biashara, usajili wa makampuni 27, upatikanaji wa namba za utambulisho wa mlipakodi (TIN) kwa wasanii 217, utoaji wa leseni mpya za biashara 89, uhuishaji wa vibali vya sanaa 481 pamoja na uhuishaji wa leseni za biashara 113.

**185.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuelimisha wasanii kuhusu umuhimu wa kuzalisha na kutoa huduma kutokana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Katika kufikia jitihada hizo, Mfuko

umewezesha wasanii 257 katika eneo la muziki, ufundi na maonesho kushiriki katika masoko ya kimataifa katika nchi 19. Hatua hii imeleta manufaa kwa wasanii kupanua wigo wa soko la bidhaa zao, kubadilishana maarifa ya biashara kwa kuboresha bidhaa na mbinu mpya za teknolojia. Vilevile, kuongeza utambulisho wa wasanii wa Tanzania katika soko la kimataifa. Aidha, nchi zilizofikiwa ni Ufaransa, Italia, Ujerumani, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi, Kenya, Uganda, Rwanda, Madagascar, Zimbabwe, Nigeria, Komoro, Uingereza, Marekani, Zambia, Kuwait, Dubai, China na Afrika Kusini.

**186.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kufuatilia thamani ya fedha za miradi ya wanufaika binafsi kubaini matokeo ya uwezeshaji kiuchumi kwa mnufaika binafsi, jamii na nchi kwa ujumla wake, Mfuko umefanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 135 iliyowezeshwa ambapo matokeo ya shughuli hiyo yalibainisha kuwa, kukamilika kwa malengo ya wanufaika kwa asilimia 89 ambao wameweza kuongeza vifaa vyenye ubora na kuzalisha kazi zenye ubora zaidi, kukamilisha programu zilizokuwa zinaendelea kama vile utengenezaji wa Filamu, Tamthilia, Muziki, Matamasha na utengenezaji wa kazi za mikono kama vile batiki, vikapu, mikoba, kununua vitambaa vya Mapambo, maua, maturubai, majukwaa n.k. Wategemezi 10,175 wamenufaika kutokana na ajira zilizozalishwa. Aidha, wategemezi wa wamiliki wa miradi hiyo na waajiriwa wao wanahusisha watoto, wenza, wakwe pamoja na ndugu na jamaa; asilimia 40 ya wanufaika wameweza kujiunga na programu za bima za afya na familia zao na hatimaye

kupunguza gharama walizokua wakitumia katika matibabu; na asilimia 61 ya waombaji wa mikopo wamepata kiwango walichoomba kutokana na kuongezeka kwa uelewa kwenye masuala ya uwekezaji katika masoko ya mitaji na hatifungani, elimu ya biashara pamoja na utunzaji wa akiba.

### 3.2.3.6 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ilianzishwa mnamo tarehe 2 Novemba, 2007 kwa tangazo Namba 220 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria ya Wakala wa Serikali namba 30 ya mwaka 1997. Mwaka 2012, TaSUBa iliteuliwa kuwa Kituo cha Jumuiya ya Afrika Mashariki chenye Ubora Uliotukuka *(Centre of Excellency)* katika ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa. Hivyo, ni kituo cha ufundishaji wa fani za utamaduni na sanaa chenye hadhi ya kimataifa.

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza adhma ya Serikali katika kuibua, kukuza, kulinda na kuendeleza vipaji vya vijana katika sekta ya sanaa kwa lengo la kuzalisha fursa za ajira na ukuaji wa uchumi wa Taifa, Serikali kupitia TaSUBa imeendela kutekeleza majukumu yake ya utoaji wa mafunzo, ushauri na utafiti katika masuala ya sanaa na utamaduni.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa afua za Serikali ya Awamu ya Sita za kuendeleza vipaji vya vijana katika kuzalisha fursa za ajira na kuongeza

mchango wa ukuaji wa uchumi wa Taifa kupitia sekta ya Sanaa na Utamaduni, Wizara kupitia TaSUBa imefanikiwa kudahili jumla ya wanafunzi 947 sawa na asilimia 118.3 ya lengo la kuwapatia mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada. Mafanikio haya ya kuongezeka kwa udahili ya wanafunzi ni moja ya matokeo ya juhudi za makusudi zinazoendelea kufanywa na Serikali inaendelea kuboresha na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya chuo kwa kuendelea kujenga madarasa na maktaba za kisasa; kujenga uzio kuzunguka majengo ya chuo; na ununuzi wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Sambamba na hayo, imeendele na mikakati ya kuanzisha na kufungua vituo vya mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya masuala ya Sanaa na Utamaduni katika mikoa mbalimbali kama Dar es Salaam, Songea na Dodoma ili kuwafikia vijana wengi wenye vipaji vya Sanaa na Utamaduni.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kutangaza na kuuza kazi za Sanaa na Utamadani ndani na nje ya nchi, TaSUBa ilikuwa na jukumu la kutangaza shughuli na mazao ya kazi za Sanaa na Utamaduni zinazozalishwa na chuo. Wizara kupitia TaSUBa imeendelea kukamilisha uanzishwaji wa redio na televisheni mtandao (Online Tv) kupitia fedha za maendeleo ambapo mpaka kufikia Aprili 2026 ukamilishaji wa uanzishaji upo kwenye hatua ya mwisho. TaSUBa imeendelea kushirikiana na wasanii maarufu wa ndani hasa wa Filamu kuwa mabalozi bora katika kukitangaza chuo na shughuli zake ambapo Taasisi iliingia

makubaliano na msanii wa filamu Bw. Salim Ahmed Issa (Gabo Zigamba) kuwa Balozi wa chuo kitaifa na kimataifa. Pia, Taasisi imeendelea kutumia vyombo vya habari vya Televisheni (*TBC, ITV, Channel Ten* na *Azam Tv*), Radio, Magazeti (*HabariLEO, Mwananchi, Uhuru na Daily News*) na akaunti za mitandao ya kijamii (Facebook, Instagram na Tiktok) kutangaza shughuli zinazofanywa na chuo na mazao yake.

**191.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza malengo ya Serikali, sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 kwa kujenga na kuboresha miundombinu ya sekta ya Sanaa na Michezo ili kuzalisha fursa nyingi za ajira kwa vijana na mchango kwa pato la Taifa. Wizara kupitia TaSUBa imeendelea kusimamia na kuratibu mradi wa ukarabati wa chuo cha Sanaa Bagamoyo kwa kupitia fedha za maendeleo ambapo, kiasi cha shilingi 750,000,000 zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kufanyika kwa shughuli mbalimbali za uboreshaji wa miundombinu ya chuo ikiwemo kukamilisha ujenzi wa uzio kwa asilimia 100; ujenzi wa darasa na maktaba ya kisasa ambao umefikia asilimi 70 na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kujifunzia na kufundishia.

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukuza na kuongeza ubora na thamani ya kazi za Sanaa na Utamaduni zinazozalishwa na wasanii wetu, TaSUBa imeendelea na taratibu za kutoa huduma ya ushauri (Consultancy) kwa vyuo, mashirikisho ya sanaa na utamaduni, vikundi vya sanaa, na taasisi mbalimbali binafsi na umma, ambapo Chuo cha Taaluma ya

Urekebishaji Tanzania (Tanzania Correction Training Academic - TCTA) kilichopo Ukonga jijini Dar es salaam kilipata ushauri wa uendeshaji wa mafunzo ya sanaa na utamaduni kwa vijana 27. Aidha, Ubalozi wa India ulipata ushauri juu ya uendeshaji wa mashindano ya uchoraji wa picha za rangi ambapo yalifanyika chuoni TaSUBa na vijana 20 walinufaika; na Taasisi ya *Ongala Music Open Forum* ilipewa ushauri juu ya uendeshaji mafunzo ya muziki wa dansi ambapo vijana 20 walinufaika. Katika kuwawezesha na kuwafikia wadau mbalimbali wa sanaa na utamaduni kupata huduma ya ushauri ili kukuza na kuongeza thamani ya kazi zao, Wizara kupitia TaSUBa kwa mwaka wa fedha 2025/26 imeshiriki katika maonesho ya kimataifa ya biashara Sabasaba tarehe 01 – 13 Julai, 2025 ambapo wadau, wasanii na vikundi mbalimbali walihudhuria kwenye banda la TaSUBa na kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wa TaSUBa.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za makusudi za Serikali ya awamu ya sita zinazoendelea kuchukuliwa katika kuongeza nafasi za ajira na ushindani katika soko la ajira hasa kwa vijana, TaSUBa imeendelea kujipambanua zaidi kwa kuwajengea uwezo vijana katika sekta ya sanaa na utamaduni kwa kuendelea kuandaa na kuhuisha mitaala mipya ya masomo. Vilevile, kwa kushirikiana na NACTVET imeendelea kukamilisha uandishi wa mitaala mitatu ya masomo ambayo ni Urithi wa Kitamaduni na Utalii (*Cultural Heritage and Tourism*), Usimamizi wa Sanaa na Masoko (*Arts Management and Marketing*) na Utendaji wa Muziki (*Music Performance)* ambapo masomo haya

yameonekana kuwa na umuhimu katika kuongeza nafasi za ajira kutokana na mahitaji ya soko la ajira.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuwawezesha wasanii na vikundi vya sanaa na utamaduni kwa kuwapa jukwaa la kutangaza na kujitangaza kitaifa na kimataifa kupitia kazi zao za sanaa na utamaduni. TaSUBa ilifanya shughuli mbalimbali za maandalizi ya Tamasha la 44 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo la tarehe 26 mpaka 29 Novemba, 2025. Maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na kuanda Mpango Kazi wa uendeshaji wa Tamasha (Festival Action plan); kuandaa na kutuma mialiko kwa wasanii na vikundi vya sanaa ndani na nje ya nchi; kutafuta wafadhili mbalimbali wa Tamasha; kuandaa na kutengeneza matangazo mbalimbali kuhusu Tamasha; na kuunda kamati mbalimbali za kusimamia shughuli za Tamasha.

**195.** ***Mheshimiwa Spika***, TaSUBa ilifanikiwa kuingia makubaliano ya mwaka mmoja na kampuni ya Vision Investiment katika kushirikiana kutafuta wafadhili ambao watasaidia kufadhili uendeshaji wa shughuli za Tamasha. Hata hivyo, Tamasha halikuweza kufanyika kutokana na kutokea kwa mabadiliko ya ratiba ya kufunguliwa kwa muhula wa masomo iliyotolewa na NACTVET ambapo tarehe ya kufunguliwa ilibadilika na kuwa tarehe 17 na 24 Novemba, 2025 hivyo kusababisha kutopata muda wa kutosha kufanya maandalizi ya shughuli mbalimbali za Tamasha ambapo pia ni sehemu ya masomo ya wanafunzi.

### 3.2.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Maendeleo ya Michezo ni nyenzo muhimu ya kuzalisha ajira, kuimarisha afya za wananchi pamoja na kuwaletea furaha Watanzania. Pia, kupitia sekta ya michezo nchi yetu inaendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali kupitia diplomasia ya michezo. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali inao wajibu wa kujenga mazingira rafiki kwa ukuaji wa sekta ya michezo. Sekta hii kwa sasa inatekeleza majukumu yake kwa kufuata Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 pamoja na Mkakati wa Maendeleo ya Michezo wa mwaka 2022. Sekta hii ni miongoni mwa mihimili inayotoa ajira na kuchangia katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Aidha, Sekta hii inasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Michezo na taasisi zilizo chini yake ambazo ni Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

#### 3.2.4.1 Idara ya Maendeleo ya Michezo

**197.** **Mheshimiwa *Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2025/26 majukumu yaliyotekelezwa ni yafuatavyo:

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu kwa ufanisi michuano ya Mpira wa Miguu Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN 2024) pamoja na kuendelea na maandalizi ya Mashindano ya AFCON 2027. Mashindano ya CHAN ni kigezo ambacho Shirikisho la Soka Afrika (CAF) hutumia kama kipimo cha nchi kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON. Mashindano hayo


yamefanyika nchini kuanzia tarehe 02 hadi 30 Agosti, 2025 ambapo nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zilikuwa wenyeji. Timu ya Taifa ya Tanzania *(Taifa Stars)* ilishiriki na kuonesha kiwango cha juu cha ushindani kwa kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali, hatua inayodhihirisha kuimarika kwa soka letu la ndani. Aidha, kutokana na ubora wa maandalizi na usimamizi wa mashindano hayo CAF ilimtunuku tuzo ya heshima Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jambo linaloendelea kuitangaza nchi yetu kimataifa kama mwenyeji mahiri wa matukio makubwa ya kimataifa ya michezo. Mafanikio haya ni matokeo ya jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita (6) inayoongozwa na mwanamichezo nambari moja (1) Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa na mapenzi makubwa na michezo hususan kuwekeza kwenye miundombinu ya michezo, kuwezesha kuijenga timu imara kupitia maandalizi bora, motisha kwa wachezaji na programu za kitaalamu kwa makocha na viongozi wa timu.




*Bw. Gerson Msigwa, Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo akiwa na Tuzo ya CAF kwa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuandaa fainali za CHAN 2024 iliyofanyika mwezi Agosti, 2025*





*Mheshimiwa Paul Christian Makonda (Mb.), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (watatu kutoka kulia) pamoja na Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Wallace Karia (wanne kutoka kulia), wakipokea bendera ya Shirikisho la mpira wa Miguu Barani Afrika (CAF), kama ishara ya kuanza kwa maandalizi ya michuano ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2027) yatakayofanyika kwa pamoja katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Tukio hilo lilifanyika tarehe 18 Januari, 2026 nchini Morocco.*





*Mheshimiwa Paul Christian Makonda (Mb.), Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo akiwa bendera ya maandalizi ya AFCON 2027 baada ya kukabidhiwa tarehe 18 Januari, 2026 nchini Morocco.*

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mashindano hayo, Serikali imeendelea na maandalizi ya Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) kwa kutekeleza kwa ufanisi majukumu mbalimbali hususan ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo, barabara, hoteli na viwanja vya mazoezi katika miji wenyeji ya Dar es Salaam, Zanzibar na Arusha. Hatua hizi ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha nchi yetu inakuwa na miundombinu ya kisasa inayokidhi viwango vya kimataifa kwa ajili ya mashindano hayo makubwa barani Afrika. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya

ukarabati wa uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umefikia asilimia 95 ya utekelezaji. Aidha, ukarabati wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi vya Gymkhana, Meja Jenerali Isamuhyo na Shule ya Sheria umekamilika na ujenzi wa viwanja vitatu (3) vingine vya mazoezi vya Farasi, Leaders Club na Gymkhana II vipo katika hatua za awali.





*Muonekano wa uwanja wa Benjamin Mkapa baada ya kufanyiwa ukarabati*

**200. *Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Jiji la Arusha, Wizara imeendelea kusimamia ujenzi wa uwanja utakaotumika katika mashindano ya AFCON 2027 wenye uwezo wa kuchukua watazamaji 32,000 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 77.5. Aidha, ujenzi wa kiwanja kimoja cha mazoezi kinachojengwa katika eneo la mradi umefikia asilimia 60. Sambamba na kiwanja hicho, Wizara imeainisha maeneo ya Mgambo, Magereza ya Kisongo na Engutoto kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vitatu (3) vya mazoezi ikiwa ni sehemu ya kukamilisha mahitaji ya miundombinu kwa ajili ya mashindano ya AFCON 2027. Utekelezaji wa miradi hii unaendelea kuonesha dhamira thabiti ya Serikali katika kuhakikisha maandalizi ya AFCON 2027 yanakamilika kwa wakati, kwa ubora unaotakiwa na kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Kufanyika kwa mashindano haya nchini kutafungua fursa mbalimbali za biashara na kuitangaza Tanzania na vivutio vyake Kimataifa pamoja na kuongeza pato la Taifa kupitia michezo.



*Ujenzi wa uwanja wa Mpira wa Miguu Arusha ukiendelea, Aprili 2026*



*Mwonekano wa uwanja wa Arusha utakapokamilika*

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mashindano ya AFCON 2027 yanafanikiwa, Serikali kupitia Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Mashindano iligawa majukumu kwa Wizara zote na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeendelea kufanya ufuatliliaji wa utekelezaji wake. Napenda kutumia fursa hii kuipongeza kamati hiyo kwa utendaji wake chini ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mradi wa uwanja, miundombinu saidizi imeendelea kujengwa ambayo ni barabara za Mateves – Bondeni yenye urefu wa kilomita 6.5 (kilomita 1.5 za njia nne na kilomita 5 za njia mbili) kutoka barabara kuu ya Arusha – Babati; barabara ya Lendita yenye urefu wa kilomita 2.75 kwa njia nne; barabara ya Essuri yenye urefu wa kilomita 2.45 kwa

njia nne, zote zikitokea barabara kuu ya Arusha bypass; na kilomita 1.5 za barabara zitakazozunguka uwanja. Aidha, ujenzi wa miundombinu mingine muhimu ikiwemo umeme, maji na mawasiliano unaendelea. Katika hatua nyingine, kwa lengo la kupata thamani halisi ya uwekezaji unaofanywa na Serikali, umetolewa mwongozo wa maendelezo ya maeneo yote yanayozunguka uwanja wa Arusha.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuridhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha tunafanikisha mashindano ya AFCON 2027, tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameridhia na kutoa kiasi cha Dola za Marekani 30,000,000, sawa na shilingi 76,157,100,000 kama ada ya uandaaji wa mashindano husika. Hii ndiyo tafsiri halisi ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kama mwanamichezo namba 1 nchini.

**203.** ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na maandalizi ya miundombinu ya AFCON 2027, Serikali imeendelea kuwekeza katika maendeleo ya miundombinu mingine ya michezo nchini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati yenye lengo la kukuza vipaji na kuboresha huduma za michezo kwa wananchi. Miradi mingine ambayo inatekelezwa ni ujenzi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 49, ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu jijini Dodoma wenye uwezo wa kuchukua watu 32,500 ambao umefikia asilimia 5, ujenzi wa Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi Jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 73.5, ujenzi wa

Kituo cha Mazoezi na Kupumzikia Wananchi jijini Dar es Salaam kilichofikia asilimia 49, ukarabati wa uwanja wa Uhuru ambao umefikia asilimia 70 na ujenzi wa miundombinu ya michezo katika shule teule saba (7) za michezo ambapo zabuni imetangazwa. Utekelezaji wa miradi hii unaonesha dhamira ya dhati ya Serikali ya kuendeleza sekta ya michezo kwa kuweka miundombinu thabiti kwa ajili ya ukuzaji wa vipaji.

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha mashindano ya AFCON 2027 yanafanikiwa, Wizara iliunda kamati tatu (3) za maandalizi. Kamati hizo ni Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi inayoundwa na Mawaziri Wote na inaongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo jukumu lake ni kusimamia maandalizi ya mashindano zikiwemo kamati zote; Kamati ya Wataalamu inayoundwa na Makatibu Wakuu na kuongozwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu. Jukumu lake likiwa ni kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Kamati ya Kitaifa, na Kamati ya Maandalizi ya Ndani - *Local Organizing Committee – (LOC)* iliyoundwa na wadau wa michezo kutoka sekta za umma, binafsi, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania na Zanzibar ambapo jukumu lake ni kutekeleza maelekezo kutoka Kamati ya Wataalamu na kutoa ushauri.

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia nchi yetu kuwa mwenyeji wa Mashindano ya AFCON 2027, Wizara imeendelea kuchukua tahadhari na hatua madhubuti za kuimarisha usalama katika michezo kwa kuratibu mkutano wa kimataifa kuhusu kupambana na ugaidi

michezoni uliofanyika tarehe 4 Machi, 2026 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwashirikisha wadau 45 kutoka Umoja wa Mataifa kupitia Kitengo cha Usalama Michezoni na Kupambana na Ugaidi (UNOCT), Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika (AUSC), Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa New York nchini Marekani, Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Jeshi la Wananchi Tanzania, Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania, Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Jeshi la Polisi Tanzania, Idara ya Uhamiaji na Taasisi nyingine za ndani ya nchi. Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kuwakutanisha wadau wa sekta ya michezo nchini na wataalamu wa masuala ya usalama michezoni kutoka Mashirika ya kimataifa ili kuweka mikakati ya pamoja, kubadilishana uzoefu, kujenga uelewa wa pamoja na kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kukabiliana na vitisho vya ugaidi wakati wa mashindano ya AFCON 2027. Kupitia mkutano huo, Tanzania imeendelea kujiandaa kikamilifu kwa kuimarisha mifumo ya usalama, kuongeza uwezo wa rasilimali watu, na kuhakikisha kuwa nchi inakuwa salama na ya kuaminika wakati wote.

**206.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ushiriki wa nchi katika majukwaa ya kimataifa na kukuza vipaji vya wanamichezo, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) na Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) imeendelea na uratibu wa ushiriki wa wachezaji wa Tanzania katika Michezo ya Jumuiya ya Madola itakayofanyika kuanzia

tarehe 23 Julai hadi 2, Agosti 2026, jijini Glasgow, nchini Scotland. Uteuzi wa wanamichezo watakaoiwakilisha nchi umekamilika, ambapo jumla ya wanamichezo 11 wamechaguliwa kushiriki katika michezo ya riadha (5), ngumi (4), judo (1) na kuogelea (1). Aidha, kambi za maandalizi kwa wanamichezo hao zinaendelea na zimepangwa kwa kuzingatia hali ya hewa pamoja na mahitaji ya mchezo husika.

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa riadha, kambi zinafanyika mkoani Arusha; mchezo wa kuogelea kambi inaendelea nchini Afrika Kusini; na mchezo wa judo mazoezi yanaendelea Ukonga, jijini Dar es Salaam. Mara ya mwisho michezo hii kufanyika ilikuwa mwaka 2022 mjini Birmingham nchini Uingereza, ambapo Tanzania ilishiriki katika michezo ya ngumi, riadha na judo ikijizolea medali tatu (3) kutoka kwa mwanariadha Felix Simbu aliyeshinda medali ya Fedha baada ya kuibuka mshindi wa pili (2) wa mbio za marathon na mabondia Yusuf Changalawe na Kassim Mbundwike walioshinda medali za shaba. Serikali kupitia Wizara inaendelea kuweka mikakati stahiki ya kuhakikisha nchi inawakilishwa na wachezaji wengi zaidi ili tuweze kuongeza uwezekano wa kupata medali nyingi zaidi.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuendelea Kupambana na Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni (*Anti-doping*) imeratibu uchukuaji wa sampuli 64 kwa wachezaji walioshiriki mashindano ya CHAN 2024 kuanzia tarehe 02 – 30 Agosti, 2025 na kuziwasilisha katika maabara kwa uchunguzi wa kitaalamu, ambapo matokeo yalibainisha kuwa sampuli

zote hazikuwa na viashiria vya matumizi ya dawa au mbinu haramu. Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu hili kwa kuchukua sampuli za wanamichezo wa ngazi za kitaifa na kimataifa wanaoshiriki katika michezo mbalimbali hapa nchini, ikiwa ni sehemu ya kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya haki, uwazi na uadilifu katika michezo. Hatua hizi zinaendelea kuimarisha taswira ya Tanzania katika medani za michezo kimataifa na kulinda afya za wanamichezo.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha tunawaongezea ujuzi wataalamu katika kupambana na dawa na mbinu haramu michezoni, Wizara imetoa mafunzo kwa watalaamu 200 na kuwawezesha wataalamu wanne (4) kuhudhuria vikao na mafunzo mbalimbali kitaifa na kimataifa ikiwemo kikao cha Wakala wa Dunia wa Kupambana na Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni (WADA) kilichofanyika Busan Korea Kusini kuanzia tarehe 1 – 5 Desemba, 2025 kikiwa na washiriki takribani 1,500 kutoka Serikalini, Mashirika ya Kikanda na Kitaifa, Maabara za *Anti-doping*, watoa huduma, watafiti na wanahabari; kikao cha Kanda ya Tano cha kupambana na mbinu haramu michezoni kilichofanyika kwa njia ya mtandao tarehe 18 Desemba, 2025 kikiwa na washiriki 10 wakiwemo kutoka UNESCO, WUSM na Zanzibar; kikao cha kitaifa cha utekelezaji wa mkataba wa kimataifa wa udhibiti wa Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni kilichofanyika mkoani Morogoro kuanzia tarehe 22 – 26 Septemba, 2025. Vilevile, Wizara imeratibu mafunzo ya kudhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu Haramu Michezoni kwa wataalamu 48 wa kinga

na tiba michezoni yaliyofanyika tarehe 27 Desemba, 2025 katika uwanja wa Benjamin Mkapa na mafunzo ya Maafisa Udhibiti watatu (3) kutoka Tanzania Bara na Zanzibar yalifanyika kwa njia ya mtandao.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Tanzania inaendelea kunufaika na fursa za diplomasia ya michezo, kwa mara ya pili Serikali imekuwa mwenyeji wa mkutano wa Pili wa Baraza la Mawaziri wa Michezo Afrika Kanda ya Nne (*AUSC Region IV*) uliofanyika tarehe 18 hadi 21 Agosti, 2025 Jijini Dar es Salaam. Jumla ya nchi tisa (9) ambazo ni Tanzania, Kameruni, Komoro, Mauritius, Shelisheli, Rwanda, Kenya, Sudan Kusini na Uganda na wadau wa sekta ya michezo kutoka Baraza la Umoja wa Afrika – *African Union Sports Council* (AUSC) walishiriki. Katika mkutano huo, Waziri mwenye dhamana ya michezo Tanzania alichaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kanda hiyo jambo linaloendelea kuimarisha nafasi na ushawishi wa Tanzania katika uongozi wa michezo barani Afrika. Aidha, Tanzania ilifanikiwa kupata hadhi ya kuwa mwenyeji wa Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Afrika Kanda ya Nne (*AUSC Region IV Secretariat)* kufuatia kusainiwa kwa Mkataba wa uenyeji hatua itakayowezesha nchi kunufaika zaidi na shughuli za michezo za kikanda, kuongeza ajira na utalii.




*Wajumbe wa Mkutano wa Pili wa Baraza la Mawaziri wa Michezo Afrika Kanda ya Nne (AUSC Region IV) wakiwa katika mkutano, uliofanyika tarehe 18 hadi 21 Agosti, 2025 Jijini Dar es Salaam.*

**211.** ***Mheshimiwa Spika***, ikiwa ni hatua ya kuibua na kuendeleza vipaji vya watoto nchini, Serikali imeendelea kuratibu Mashindano ya Michezo ya UMISSETA na UMITASHUMTA kwa kushirikiana na Vyama na Mashirikisho ya Michezo. Serikali kupitia Wizara imeratibu na kushiriki mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa kushirikiana na OWM - TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WEST). Mashindano hayo yalifanyika mkoani Iringa kuanzia tarehe 7 – 30 Juni, 2025 yakihusisha jumla ya timu 28 kutoka Tanzania Bara na Visiwani. Jumla ya michezo 10 ilishindaniwa ambayo ni: Mpira wa Miguu, Mpira wa Mikono, Mpira wa Kikapu, Netiboli, Mpira wa goli, Riadha, Sanaa za Maonesho, Usafi, Nidhamu, Tenisi na Tenisi ya Mezani. Jumla ya wanafunzi 3,194 walishiriki, wakiwemo wavulana 1,611

na wasichana 1,583 kutoka mikoa 26 ya Tanzania Bara na Visiwani pamoja na viongozi wa michezo na walimu 843. Serikali imeendelea kuwatumia wadau katika kulea vipaji vinavyopatikana kupitia mashindano hayo. Mashindano hayo yamekuwa na manufaa makubwa katika uibuaji wa vipaji ambapo Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) likiwa ni wadau muhimu miongoni mwa wadau wakubwa wa kuendeleza vipaji, wanawachukua watoto waliofanya vizuri na kuwaendeleza katika vituo vyao vya michezo vya Kigamboni jijini Dar es Salaam na Mnyanjani Tanga. Aidha kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Shule teule 56 za michezo pamoja na Akademia ya Michezo chuoni Malya kutaongeza wigo wa kuendeleza/kulea vipaji hivyo.




*Viongozi mbalimbali katika ufunguzi wa mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA yaliyofanyika Mkoani Iringa, Juni – Julai 2025*






*Wanafunzi waloshiriki katika mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA Mkoani Iringa, Juni – Julai 2025*

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na michezo iliyotajwa hapo juu, Serikali imeratibu michezo ya Shirikisho la Michezo ya Shule za Sekondari Afrika Mashariki (FEASSA) iliyofanyika Kakamega nchini Kenya ambapo jumla ya wanafunzi 4,199 walishiriki kutoka nchi sita (6) ambazo ni Burundi 37, Rwanda 261, na wanafunzi 18 kutoka Ivory Coast. Tanzania iliwakilishwa na wanafunzi 490, Kenya 1,815, Uganda 1,578. Michezo iliyoshindaniwa katika mashindano hayo ni; Kriketi, Mpira wa Goli, Mpira wa Miguu, Mpira wa Pete, Mpira wa Wavu, Mpira wa Besiboli, Mpira wa Mikono, Tenisi ya Meza, Tenisi na Riadha. Tanzania ilifanikiwa kushinda jumla ya medali 10, zikiwemo nne (4) za dhahabu, mbili (2) za fedha, na nne (4) za shaba. Katika kukuza na kuendeleza vipaji vinavyoibuliwa kupitia mashindano hayo, Serikali kupitia Wizara inashirikiana na vyama na mashirikisho ya michezo katika ufuatiliaji wa vipaji ili kuhakikisha wanamichezo wenye vipaji wanaendelezwa na kuunganishwa na timu mbalimbali pamoja na akademia za kitaifa na kimataifa.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua mchango wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuibua na kuendeleza michezo nchini, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imechukua hatua za haraka kwa kuanza majadiliano na OWM– TAMISEMI ili kuhakikisha kuwa Halmashauri zote nchini zinajenga viwanja vya michezo pia maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za michezo yanalindwa, yanatunzwa na kuendelezwa kama ilivyokusudiwa. Hatua hii inalenga kuibua vipaji, kuzuia uvamizi wa maeneo husika na kuhakikisha yanatumika

kwa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza ushiriki mpana wa sekta binafsi katika kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya michezo.

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na juhudi kubwa zinazoendelea kufanywa na Serikali katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo nchini, Serikali kupitia Wizara imepata kibali cha kuanzisha Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo nchini ujulikanao kama - *Sports Infrastructure Management Agency* (SIMA). Kuanzishwa kwa Wakala huu kutaongeza ufanisi katika utunzaji na uendeshaji wa miundombinu ya michezo iliyopo na inayoendelea kujengwa, sambamba na kutoa miongozo ya kitaalamu kuhusu ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miundombinu hiyo kwa kuzingatia viwango bora vya kitaifa na kimataifa, pia kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wadau wote wanaokusudia kuwekeza katika miundombinu ya michezo nchini. Aidha, kwa kuwa Serikali inaendelea kuwekeza rasilimali fedha kwa kiwango kikubwa katika sekta hii kwa matarajio ya kupata thamani halisi ya uwekezaji wake, Wakala huu utaweka mifumo madhubuti ya usimamizi na utunzaji wa miundombinu hiyo ili kuhakikisha ubora, uendelevu na uwekezaji wenye tija.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha sekta ya michezo nchini, Wizara imefanikiwa kuandaa na kuratibu Kikao Kazi cha 16 cha Maofisa Maendeleo ya Michezo Tanzania kilichofanyika tarehe 28 - 31 Machi, 2026 jijini Arusha ambapo jumla ya wadau 147 walishiriki. Kikao hicho

kilihusisha Maofisa Michezo kutoka ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau mbalimbali wa sekta ya michezo. Kikao hicho kilitumika kama jukwaa muhimu la kujengeana uwezo, kubadilishana uzoefu na kuimarisha uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya michezo hususani katika ngazi za Halmashauri na Mikoa. Aidha, kupitia kikao hicho, washiriki walipata mafunzo kuhusu fursa zitokanazo na mashindano ya AFCON 2027 na jinsi ya kunufaika nazo.

**216.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ustawi na afya za wanamichezo nchini, Serikali kupitia Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuratibu utoaji wa huduma za kinga na tiba michezoni ambapo kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya wanamichezo 771 walioshiriki katika michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa walipatiwa huduma hizo. Huduma hizo zinalenga kuhakikisha wanamichezo wanapata huduma stahiki za afya kabla, wakati na baada ya mashindano na hivyo kuimarisha uchezaji wao, kulinda afya zao na kuongeza ushindani kwa ngazi ya taifa na kimataifa. Mbali na huduma ya kinga na tiba michezoni, Serikali pia imeendelea kuratibu mafunzo ya tiba na kinga michezoni kwa jumla ya watoa huduma wapatao 240 na wanamichezo 120 wa michezo ya Judo, Ngumi, Riadha na kriketi.

### 3.2.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza la Michezo la Taifa (BMT) limeanzishwa chini ya Sheria ya Baraza la

Michezo la Taifa Sura ya 49. Majukumu ya BMT ni pamoja na kuendeleza, kustawisha na kudhibiti aina zote za michezo ya ridhaa na kulipwa kwa kushirikiana na Vyama/Mashirikisho ya Michezo; kuhimiza na kutoa fursa za ushirikiano miongoni mwa Vyama vya Michezo; kuidhinisha mashindano na matamasha ya Kitaifa na Kimataifa yanayoandaliwa na Mashirikisho/Vyama vya Michezo na kuamsha ari ya wananchi kupenda aina zote za michezo. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Aprili 2026 majukumu yaliyotekelezwa na Serikali kupitia BMT yanabainishwa ifuatavyo:

**218.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuendeleza ushirikiano na mataifa mbalimbali katika sekta ya michezo. BMT kwa kushirikiana na taasisi ya ushirikiano wa Kimataifa ya Japani (JICA) limeratibu awamu ya saba ya mashindano ya Riadha kwa Wanawake *"Ladies First"* ambayo yalifanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 28 - 30 Novemba, 2025. Jumla ya wanariadha wa kike 152 kutoka mikoa 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar walihudhuria katika mashindano hayo. Mashindano hayo yamekuwa na mafanikio makubwa kwa kuzalisha wanariadha wawili wa kike ambao wameliwakilisha taifa katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo michezo ya Jumuiya ya Madola, michezo ya Afrika pamoja na Marathoni za kimataifa.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT imeendelea kutekeleza mipango mbalimbali ya kuhamasisha ushiriki wa watu wenye ulemavu katika michezo. Baraza kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa

ya Temeke limeratibu tamasha la michezo kwa wanafunzi wenye ulemavu kupitia programu ya michezo kwa wote (Sports for all) ambapo jumla ya wanafunzi 2,000 walishiriki katika tamasha hilo. Vilevile, BMT kwa kushirikiana na Chama cha Mpira wa Meza kwa Watu wenye Ulemavu (Tanzania Para Table Tennis Association) waliendesha mafunzo kwa walimu 23 wa mchezo wa mpira wa meza kwa watu wenye ulemavu kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu wa michezo ya watu wenye ulemavu.

**220.** ***Mheshimiwa Spika,*** BMT kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) liliratibu mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao ulifanyika tarehe 13 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwaleta pamoja viongozi 50 wa soka barani Afrika ukiwa na lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kukuza vipaji, kuimarisha ushindani wa vilabu na timu za taifa, pamoja na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya mpira wa miguu. Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni kielelezo cha uwezo wa nchi yetu kuandaa mikutano mikubwa na umeongeza hadhi ya Tanzania katika ramani ya soka Afrika, hasa wakati Taifa linajiandaa na fainali za mashindano ya "Africa Cup of Nations 2027" (AFCON 2027). Kufanyika kwa mkutano huu nchini, umeifanya nchi yetu iendelee kuaminiwa kama kitovu cha maamuzi makubwa ya michezo barani Afrika.

**221.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kutambua na kuthamini mafanikio ya wanamichezo na

timu za Taifa kwa kutoa tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa. Baraza la Michezo la Taifa linaendelea kutoa motisha na tuzo kwa wanamichezo waliofanya vizuri kwa msimu wa nne (4) mfululizo tangu mwaka 2022 zilipoanzishwa tuzo hizi na kuwa chachu ya mafanikio katika sekta ya michezo na kwa wanamichezo kwa ujumla. Aidha, kwa msimu wa 2024/25 tuzo zinatarajia kufanyika mwezi Mei 2026 jijini Dar es salaam.

**222.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia BMT imeanza ujenzi wa Kituo cha Mafunzi ya Michezo "*Sports Training Centre*" katika mji wa Babati mkoani Manyara. Serikali inatarajia kujenga vituo vya michezo katika kanda saba (7) ambazo ni Kanda ya Kaskazini, Kusini, Mashariki, Kati, Ziwa, Magharibi pamoja na Nyanda za Juu Kusini. Kwa awamu ya kwanza Serikali inaanza ujenzi katika Kanda ya Kaskazini katika Mkoa wa Manyara. Kazi zilizofanyika ni kulipa fidia ya eneo, hati miliki ya eneo na michoro imeandaliwa. BMT lililipa fidia ya eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 54,896 kwa thamani ya Shilingi 137,240,000. Pia, Mshauri Elekezi amepatikana ambaye ni *Volumetric Architec Consultancy Ltd* na zabuni ya ujenzi imetangazwa.

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) imeendelea kuwezesha ushiriki wa wanamichezo na timu za taifa katika mashindano ya kimataifa ambapo uwezeshaji huo umeleta mafanikio makubwa katika ushiriki wa wanamichezo wetu. Serikali inampongeza mwanariadha Alphonce Felix Simbu aliyefanikiwa kushinda medali ya dhahabu

katika mashindano ya riadha ya Dunia yaliyofanyika Septemba 2025 jijini Tokyo, Japani, ikiwa ni medali ya kwanza ya dhahabu kwa Tanzania katika mashindano hayo tangu kupata uhuru, pia kwa kuibuka mshindi wa pili na kushinda medali ya fedha katika mashindano ya marathoni ya kimataifa yaliyofanyika tarehe 20 Aprili, 2026 Jijini Boston, Marekani. Pia, tunampongeza mwanariadha John Nahhay Wele aliyetwaa medali ya dhahabu katika mashindano ya nusu marathon yaliyofanyika tarehe 19 Aprili, 2026 nchini Poland. Vilevile, Serikali inazipongeza Timu ya Taifa ya mpira wa miguu "Taifa Stars" kwa kufika hatua ya 16 bora katika mashindano ya AFCON 2025 yaliyofanyika nchini Morocco na kufika hatua ya robo fainali ya mashindano ya CHAN 2024, Timu ya wanawake ya Futsal kwa kushiriki Kombe la Dunia 2025 nchini Ufilipino na kufika hatua ya makundi, "Twiga Stars" iliyotwaa ubingwa wa CECAFA Senior Women's Championship 2025 na kufuzu WAFCON 2026, pamoja na timu ya Amputee Football kwa kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati nchini Burundi. Aidha, Wizara inatoa pongezi kwa timu ya Taifa ya ngumi kwa kushinda jumla ya medali 18 (dhahabu 1, fedha 4 na shaba 13) katika mashindano ya kanda ya tatu Afrika yaliyofanyika Kenya mwaka 2025; timu ya Kriketi U19 kwa kufuzu Kombe la Dunia la U19 2026 lililofanyika Namibia na Zimbabwe; timu ya mpira wa kikapu ya Dar City iliyoshiriki mashindano ya kikapu Afrika yaliyofanyika nchini Afrika Kusini na kufanikiwa kufuzu kucheza fainali ya mashindano hayo itakayofanyika nchini Rwanda Mei 2026; bondia Ibrahim Class alipigana na kuapata mikanda miwili ya WBC na WBO;

bondia Lupakisyo Shoti alishinda mkanda wa IBO Afrika; Amani Bariki (Manichuga) alishinda mkanda wa WBC Intercontinental; Frank Shagembe alishinda mkanda wa WBO Afrika kwa uzito kg 90; Yusuph Changarawe ameshinda mkanda wa WBC Afrika; Halima Vunjabei alishinda mkanda wa PST, mafanikio hayo yanayoonesha maendeleo chanya ya michezo nchini.

**224.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia BMT kwa kushirikiana na Shirkisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) liliratibu mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) ambao ulifanyika tarehe 13 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliwaleta pamoja vigogo wa soka barani Afrika ukiwa na lengo la kujadili na kuweka mikakati ya kukuza vipaji, kuimarisha ushindani wa vilabu na timu za Taifa, pamoja na kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya mpira wa miguu. Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo ni kielelezo cha uwezo wa nchi yetu kuandaa mikutano mikubwa na umeongezea hadhi ya Tanzania  katika ramani ya soka Afrika hususan wakati mataifa yakijiandaa na fainali za AFCON 2027. Ujio wa viongozi hawa unaweka wazi kuwa nchi yetu inazidi kuaminiwa kama kitovu cha maamuzi makubwa ya michezo barani Afrika.

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali ya awamu ya sita katika sekta ya michezo umechochea ukuaji wa sekta hii na kuchachusha upatikanaji wa ajira kwa vijana wa kitanzania ndani na nje ya nchi. Wachezaji wa

kitanzania 57 wamepata ajira za kulipwa katika nchi mbalimbali, katika vilabu vya mpira wa miguu kwa wanawake na wanaume, mpira wa kikapu, mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu, mchezo wa *softball*, mchezo wa kikapu na mchezo wa wavu.



Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, *Taifa Stars*



Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu ya Wanawake, *Twiga Stars*



Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu chini ya Miaka 20, *Ngorongoro Heroes*

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, Wizara kupitia BMT ipo kwenye hatua za ujenzi wa mfumo wa kukusanya mapato, kutoa vibali vya wachezaji pamoja na usajili wa vyama, vilabu pamoja na mashirikisho ya michezo unaoitwa "*Sports Intergrated Management Information System*" (SIMIS). Mfumo huu utaongeza ufanisi katika makusanyo ya mapato ya Serikali pamoja na kurahisisha mchakato wa usajili wa vyama vya michezo. Mfumo huu unajengwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na unatarajiwa kukamilika Julai 2027 kwa gharama ya shilingi 139,476,000. Mfumo upo kwenye hatua ya upembuzi yakinifu na utarahisisha utoaji wa vibali kwa njia ya mfumo ambao utaunganishwa na taasisi zingine ambazo zinahusika

katika shughuli za michezo ili kurahisha huduma kwa wateja.

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia BMT imeidhinisha na kutoa jumla ya vibali 304 sawa na asilimia 75.71 ya lengo la kutoa vibali 350 kwa wanamichezo mbalimbali pamoja na timu za Taifa kushiriki katika mashindano mbalimbali ya Kimataifa. Baraza linaendelea na kusimamia taratibu kwa mujibu wa sheria ili vyama na mashirikisho vifuate taratibu za upatikanaji wa vibali kwa ajili ya kuendesha matukio ya michezo. Vibali vilivyotolewa vinahusisha michezo ifuatayo:

(a) Mabondia wa Ngumi za kulipwa vibali 56;
(b) Mapromota kuandaa mapambano ya ngumi za kulipwa vibali 31;
(c) Safari za Wanariadha kwenda nje ya nchi vibali 32;
(d) Kuandaa marathoni vibali 18;
(e) Wachezaji na wataalamu wa kigeni vibali 137;
(f) Matukio mengine ya michezo vibali 30; na
(g) Mabonanza vibali 23.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutoa elimu kwa umma na kusajili vyama, Akademia, Mawakala, Mashirikisho, na Vilabu vya Michezo kwa kutumia mfumo wa kidigitali, ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Aprili 2026 jumla ya vyama vya michezo 260 vimesajiliwa ambapo, vituo vya michezo ni 18, akademia 27, mawakala wa michezo 46, mashirikisho 27 na vilabu 142 vimesajiliwa sawa na asilimia 173 ya lengo la kusajili 150.

**229. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kufanya maandalizi ya timu ya Taifa ambayo itashiriki katika mashindano ya AFCON. Ushindani katika mashindano ya AFCON umeendelea kuongezeka kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na nchi mbalimbali katika maendeleo ya soka. Kwa kuzingatia kuwa Tanzania itakuwa mmoja ya wenyeji wa mashindano hayo, timu ya Taifa inatakiwa kufanya vizuri ili kulinda heshima ya nchi yetu. Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati madhubuti wa maandalizi ya timu ya taifa unaolenga kuimarisha uwezo wa wachezaji, benchi la ufundi, na mifumo ya maandalizi ya timu kwa ujumla. Mpango huo ni pamoja na kumpata kocha mwenye uwezo wa kuiongoza timu hiyo, kuandaa kambi za muda mfupi kwa ajili ya kuwapa wachezaji uzoefu, kushiriki mechi za kirafiki za kimataifa, kuimarisha mfumo wa utambuzi wa vipaji pamoja na kuongeza uungwaji mkono wa mashabiki kwa timu ya Taifa kwa kutengeneza jezi zenye ubora na mvuto zitakazovaliwa na wananchi.

**230. *Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuimarisha dhana ya utawala bora Wizara kupitia BMT imeratibu na kusimamia chaguzi za vyama na mashirikisho ya michezo, pamoja na kusimamia utawala bora kwa vyama vya michezo kwa kuratibu vikao 21 vya vyama na mashirikisho ya michezo kwa lengo la kujadili masuala ya maendeleo ya michezo ikiwa ni pamoja na kutatua changamoto zinazowakabili. Jumla ya chaguzi 12 sawa na asilimia 300 ya lengo la mwaka zimeratibiwa. Chaguzi zilizosimamiwa na Baraza ni zifuatazo:

(a) Uchaguzi Mkuu wa chama cha Waamuzi wa Ngumi za Kulipwa Tanzania (ATPBO) uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 12 Julai, 2025;
(b) Uchaguzi wa Chama cha Mbio za Pikipiki Tanzania uliofanyika jijini Dar es Salaam tarehe 8 Novemba, 2025;
(c) Uchaguzi wa Shirikisho la Taekwondo Tanzania uliofanyika jijini Arusha terehe 15 Novemba, 2025;
(d) Uchaguzi wa Shirikisho la Mpira wa Wavu Tanzania uliofanyika tarehe 21 Desemba, 2025 jijini Dodoma;
(e) Uchaguzi wa Kamati ya Paralimpiki Tanzania (TPC) uliofanyika tarehe 25 Januari, 2026 jijini Dar es Salaam;
(f) Uchaguzi wa Chama cha Michezo ya Mashua Tanzania (TCA) uliofanyika tarehe 9 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam;
(g) Uchaguzi wa Chama cha wanawake wa gofu (TLGU) uliofanyika tarehe 22 Februari, 2026 jijini Dar es Salaam;
(h) Uchaguzi wa Chama cha Netiboli Tanzania (CHANETA) uliofanyika tarehe 01 Februari, 2026 jijini Dodoma;
(i) Uchaguzi wa shirikisho la mpira wa kikapu Tanzania (TBF) uliofanyika tarehe 28 Februari, 2026 jijini Dodoma; na
(j) Uchaguzi wa Chama cha Judo Tanzania (JATA) uliofanyika tarehe 16 Januari, 2026 jijini Dar es Salaam.

### 3.2.4.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni chuo cha kati kilichosajiliwa mwaka 2010 na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa usajili namba

REG/PWF/019 na kupatiwa ithibati ya kutoa mafunzo. Chuo hiki ni taasisi muhimu ya Serikali katika kuendeleza taaluma ya michezo nchini na katika kutekeleza na kukuza sekta ya michezo ili iwe sehemu muhimu ya kukuza uchumi wa Taifa. Kupitia Chuo hiki, Serikali inalenga kuandaa wataalamu wa michezo watakaosaidia kuibua na kukuza vipaji, kuboresha usimamizi wa michezo na kuongeza mchango wa sekta hii katika ajira, afya ya jamii na maendeleo ya uchumi kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi April 2026, Wizara kupitia Chuo imetekeleza majukumu yafuatavyo:

**232.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha rasilimaliwatu katika sekta ya michezo, Serikali kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wanachuo 416, sawa na asilimia 83 ya lengo la kutoa mafunzo kwa wanachuo 500. Mafunzo hayo yametolewa katika programu mbalimbali zikiwemo Astashahada na Stashahada ya Elimu ya Viungo kwa Michezo, Stashahada ya Utawala na Uongozi katika Michezo pamoja na Stashahada ya Ufundishaji wa Michezo. Kupitia programu hizi, Serikali inaendelea kuandaa wataalamu watakaosaidia kuibua na kukuza vipaji vya wanamichezo, kuimarisha usimamizi wa mashindano na kuongeza mchango wa sekta ya michezo katika kuchochea uchumi na ajira kwa vijana.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwajengea uwezo na kuongeza ufanisi katika kusimamia na kuendeleza michezo nchini, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya

kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau mbalimbali wa michezo. Jumla ya wadau 279 wamenufaika na mafunzo, wakiwemo viongozi wa vilabu na makocha 52, watoa huduma ya kwanza na madaktari wa timu 108, waamuzi 30, mawakala wa wachezaji 11 na waandishi wa habari za michezo 20. Mafunzo hayo yametolewa katika Nyanja za Usimamizi wa Michezo (Sports Management), usimamizi wa majeraha ya michezo na uhamasishaji wa udhibiti wa matumizi ya dawa zilizokatazwa michezoni, mafunzo ya Mikataba na Ustawi wa Wachezaji (Sports Agency Contract Management and Athlete Welfare) na mafunzo ya sheria za Michezo, mikataba na masuala ya maadili (sports law, contract and ethical issues). Mafunzo haya ni sehemu ya jitihada za Serikali kulinda maslahi ya wanamichezo na kuhakikisha sekta ya michezo inasimamiwa kwa weledi na uwazi.

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kilitoa mafunzo kwa waongoza vituo vya mazoezi ya viungo *(Fitness and Gym Instructors)* 28 wa vituo 28 Nchini. Vilevile, mafunzo ya michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mikono, kikapu, wavu, goli na mchezo wa riadha yalifanyika katika Halmashauri ya Jiji la Arusha yakihusisha walimu 44 wa michezo kutoka shule za msingi na sekondari.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika dhamira ya dhati ya kuijenga Tanzania yenye vijana wenye ujuzi, ajira na mchango hai katika uchumi wa Taifa, Wizara imeendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kuwa mitaala ya mafunzo inaendana kikamilifu na kasi

ya mabadiliko ya sekta ya michezo duniani pamoja na mahitaji halisi ya soko la ajira. Kupitia Chuo husika, Serikali imefanya maboresho ya kimkakati katika mitaala ya programu za pamoja na *Sports Coaching*, katika ngazi ya tano na sita.

**236. *Mheshimiwa Spika,*** maboresho haya si ya kawaida, yamelenga kwa makusudi kabisa kuimarisha mafunzo kwa vitendo, kuongeza ubora wa ujuzi kwa wanafunzi wetu, na kuhakikisha kuwa wahitimu wanaandaliwa kuwa wataalamu mahiri, wabunifu na wenye uwezo wa kushindana katika soko la ajira la ndani na kimataifa. Hatua hii inaakisi dira ya Serikali ya kuhakikisha sekta ya michezo inakuwa chanzo cha ajira, kipato na fahari ya taifa letu. Tunajenga kizazi chenye maarifa, nidhamu na weledi kitakachoipeleka Tanzania mbele kupitia michezo.

**237. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuhakikisha mitaala ya mafunzo inaendana na mabadiliko ya sekta ya michezo Duniani na mahitaji ya soko la ajira, Wizara kupitia Chuo imefanya maboresho katika mitaala ya programu za Elimu ya Viungo kwa Michezo (Physical Education and Sports), Uongozi na Utawala wa Michezo pamoja na Ufundishaji wa Michezo (Sports Leadership and Management), katika ngazi ya tano na sita. Maboresho hayo yamelenga kwa makusudi kabisa kuimarisha mafunzo kwa vitendo, kuongeza ubora wa ujuzi kwa wanafunzi wetu, na kuhakikisha kuwa wahitimu wanaandaliwa kuwa wataalamu mahiri, wabunifu na wenye uwezo wa kushindana katika soko la ajira la ndani na kimataifa.

**238.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kupanua wigo wa programu za mafunzo ili kuendana na mwelekeo wa sasa wa maendeleo ya michezo duniani, Wizara kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kwa kushirikiana na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) imeandaa mitaala mipya mitatu (3) ambayo itaanza kufundishwa mwaka wa masomo 2026/27. Mitaala hiyo ni Mtaala wa Usimamizi wa Michezo katika Jamii, Afya na Ustawi *(Community Sports, Health and Wellness Management)*, Uandishi wa Habari za Michezo *(Sports Journalism),* Utalii wa Michezo *(Sports Tourism)* na Masoko ya Michezo na Ukarimu *(Sports Marketing and Hospitality Studies).* Programu hizi zinalenga kuongeza thamani ya sekta ya michezo katika uchumi wa Taifa kwa kufungua fursa za ajira, ubunifu na uwekezaji katika michezo.

**239.** ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kimeendelea kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika maendeleo ya michezo kwa kuanzisha ushirikiano na taasisi 4 za kimataifa. Ushirikiano huu unalenga kubadilishana utaalamu, kufanya tafiti na kuendeleza elimu ya michezo. Katika hatua hiyo, Wizara imeanzisha ushirikiano na Taasisi ya *Yoga for Wellness Tanzania/Africa* ili kuendeleza programu za michezo kwa afya na ustawi wa jamii. Vilevile, majadiliano yanaendelea na Chuo Kikuu cha North Carolina nchini Marekani yenye lengo la kuboresha eneo la habari za michezo, Chuo Kikuu cha Michezo cha Scuber nchini Japan kwa ajili ya kubadilishana utaalamu wa michezo. Hali kadhalika, majadiliano na *Norwegian School of*

*Sports Sciences* yanaendelea kwa ajili ya kupata vifaa na mafunzo yatakayosaidia kukuza Akademia za Michezo.

**240.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza ufanisi wa shughuli za michezo pamoja na kushughulikia changamoto ya uhaba wa wataalamu wa michezo katika shule za msingi, sekondari na taasisi zingine za umma, Wizara kupitia Chuo imeandaa andiko la mpango wa ushirikiano wa kitaasisi na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu ya michezo katika ngazi mbalimbali za elimu. Lengo kuu la ushirikiano huu ni kuimarisha mfumo wa utoaji wa elimu ya michezo katika ngazi zote za elimu, sambamba na kuweka mazingira wezeshi ya kitaasisi yatakayochochea ubunifu, utaalamu na ushindani. Kupitia mpango huu, Serikali inalenga kuibua, kulea na kukuza vipaji vya michezo kwa utaratibu endelevu, kuanzia ngazi ya shule hadi kufikia viwango vya juu vya kitaaluma kitaifa na kimataifa, hivyo kuchangia kikamilifu katika ajenda ya taifa ya kukuza ajira, afya na hadhi ya nchi katika medani za kimataifa.

**241.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, Serikali imekamilisha ukarabati wa madarasa matatu (3), jengo moja (1) la ofisi (utawala) pamoja na ujenzi wa jengo la hosteli la ghorofa nne (4) lenye uwezo wa kuchukua wanachuo 198. Kukamilika kwa miundombinu hii kunaongeza uwezo wa Chuo kudahili wanafunzi wengi zaidi na hivyo kuongeza idadi ya wataalamu wasio tia shaka katika tasnia ya michezo nchini. Aidha, Serikali imenunua

magari mawili (2) likiwemo basi dogo la Chuo kwa ajili ya kurahisisha safari za mafunzo kwa vitendo kwa wanachuo pamoja na gari la Mkuu wa Chuo ili kuboresha ufanisi wa shughuli za kiutendaji. Hatua hizi zimeendelea kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia Chuoni.



*Muonekano wa jengo la hosteli ya Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya lililokamilika.*

**242.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha vipaji vya michezo mbalimbali vinaibuliwa na kuendelezwa, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya Akademia ya Michezo ambao umefikia asilimia 49**.** Kupitia akademia hii, Serikali inalenga kuibua na kukuza vipaji vya vijana, kuandaa wataalamu wa michezo watakaokidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa ili kuifanya sekta ya michezo kuwa chanzo muhimu cha ajira, kipato na uchumi. Aidha, maendeleo ya akademia hii yatawezesha kuvutia mashindano na uwekezaji wa michezo kutoka ndani na nje ya nchi.

### 3.2.5 KUIMARISHA UTENDAJI WA WIZARA NA RASILIMALIWATU

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu, Serikali kupitia Wizara inaendelea kutoa huduma ya usafiri kwa viongozi na watumishi ambapo Wizara imeimarisha sehemu ya usafiri kwa kuipatia vitendea kazi vipya na vya kutosha yakiwemo magari. Jumla ya magari 23 yameendelea kutumika na kuhudumiwa. Vilevile, Wizara imeendelea kulipa stahiki za viongozi na watumishi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali iliyowekwa na Serikali. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2026, Watumishi 50 wamelipwa gharama za likizo, watumishi sita (6) wamelipwa stahiki za uhamisho na watumishi watatu (3) wamelipwa stahiki za kusafirisha mizigo baada ya utumishi wao wa umma kukoma.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za ulinzi na usafi kwa ofisi za Wizara zilizopo Mtumba Dodoma na Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam. Huduma zote zinatolewa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya Serikali. Sambamba na hilo, ili kuimarisha utaalamu na ujuzi, Wizara imeendelea kuratibu na kuwezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi ambapo jumla ya watumishi 51 wamehudhuria mafunzo hayo, kati ya hao wanaume ni 31 na wanawake ni 20. Kati yao watumishi 27 wanaendelea kupata mafunzo ya muda mrefu kwa idadi

ya wanaume 16 na wanawake 11. Aidha, watumishi 24 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi ambapo wanaume ni 15 na wanawake ni tisa (9). Mafunzo hayo ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo na kukidhi vigezo vya miundo mbalimbali ya kiutumishi.

**245.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuwapatia watumishi vitendea kazi. Watumishi wamehamia kwenye jengo jipya la wizara lenye nafasi ya kutosha na samani nzuri. Sambamba na hilo, mazingira ya kazi yameboreshwa kwa kuwapatia vifaa vya kisasa vinavyoendana na mabadiliko ya teknolojia zikiwemo kompyuta na printa. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Aprili 2026, Wizara imenunua kompyuta za mezani 55, kompyuta mpakato 30 na printa 10. Juhudi zote hizi zinalenga kuongeza ari ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kuongeza ufanisi.

**246.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa mazingira bora ya utendaji kazi pamoja na ustawi wa watumishi, ni chachu ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu. Hivyo, Wizara inaendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi na ustawi wa watumishi. Kwani kwa kufanya hivyo, watumishi watakuwa na utulivu ambao utaongeza ari katika utekelezaji wa majukumu.

## 4.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA NA HATUA ZILIZOCHUKULIWA KUKABILIANA NAZO

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana mwaka 2025/26, changamoto katika utekelezaji wa majukumu hazikosekani. Changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kama ifuatavyo:

(i) Ufinyu wa bajeti ya Wizara hususan ya Matumizi Mengineyo (OC), unaosababisha kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake ikiwemo kufanya tafiti mbalimbali kuhusu utamaduni, mila na desturi za mtanzania, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbuku;

(ii) Kasi ya maendeleo ya sayansi na teknolojia na utandawazi inayosababisha upotoshwaji wa mila, desturi na maadili hususan kwa vijana na wasanii; na

(iii) Kuwepo kwa migogoro kwenye baadhi ya vyama na vilabu vya michezo hivyo kukwamisha maendeleo ya michezo.

**248.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na changamoto hizo, Serikali imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutumia njia mbalimbali za kutatua changamoto hizo. Miongoni mwa njia ilizozitumia ni pamoja na:

(i) Kuendelea kutafuta kikamilifu vyanzo vipya vya mapato kwa kupitia upya sheria na kanuni zinazosimamia sekta zilizo chini ya mamlaka yake;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa vijana na wasanii kupitia njia mbalimbali ikiwemo semina, mikutano

na warsha. Pia, mafunzo hutolewa kwa njia ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii; na

(iii) Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa inaendelea kutoa elimu kwa wadau wa michezo kuhusu uzingativu wa sheria na taratibu kwa maendeleo ya sekta.

## 5.0 MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2026/27, Wizara na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau itatekeleza majukumu mbalimbali kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/27 - 2030/31); Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025 - 2030); Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipohutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; maelekezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Mwelekeo wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2026/27; Mpango Mkakati wa Wizara (2026/27 - 2030/31); Malengo ya Umoja wa Mataifa kuhusu Maendeleo Endelevu ya Mwaka 2030; na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### 5.1 SEKTA YA HABARI

#### 5.1.1 IDARA YA HABARI - MAELEZO

**250.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara, kupitia Idara ya Habari – MAELEZO, katika mwaka wa fedha 2026/27 itaendelea kutekeleza jukumu la kusimamia Sekta ya Habari ili kuhakikisha Watanzania wanapata taarifa sahihi na kwa wakati. Katika kutekeleza hilo, Wizara itaratibu na kuandaa mikutano ya Msemaji Mkuu wa

Serikali kwa lengo la kuelezea utekelezaji wa miradi ya kimkakati, pamoja na kukusanya, kuchakata na kusambaza habari na makala kuhusu utendaji wa Serikali. Vilevile, Wizara itaratibu na kufanya tathmini ya utoaji wa taarifa za Serikali kwa umma, kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata taarifa sahihi, kwa wakati, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, Wizara itaratibu na kuandaa mikutano ya Wizara na taasisi za Serikali na waandishi wa habari, ili kuimarisha mawasiliano kati ya Serikali na vyombo vya habari.

**251.** ***Mheshimiwa Spika***, kadhalika, Wizara itaratibu kikao kazi cha mwaka cha Maofisa Habari wa Serikali pamoja na mkutano wa mwaka wa maendeleo ya Sekta ya Habari. Pia, itaendelea na jukumu la kuchapisha leseni za magazeti na majarida, kuchapisha Jarida la *NCHI YETU*, pamoja na kusambaza picha rasmi za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere. Sambamba na hayo, Wizara itaendelea kuratibu utambuzi wa akaunti za mitandao ya kijamii ya taasisi za Serikali, pamoja na kuratibu vyombo vya habari na waandishi wa habari wa ndani na nje ya nchi katika matukio mbalimbali ya kitaifa na ziara za viongozi. Hatua hizi zinalenga kuimarisha utoaji wa taarifa sahihi na kuongeza uwazi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali.

### 5.1.2 SHIRIKA LA UTANGAZAJI TANZANIA (TBC)

**252.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2026/27, TBC imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo;

kuhakikisha upatikanaji wa maudhui ya redio (TBC Taifa, Bongo FM na TBC International), Televisheni (TBC1, TBC2, Tanzania Safari Chaneli na Televisheni ya Kiingereza), TBC mtandao, kurasa za mitandao ya Kijamii na redio za Kanda za TBC (TBC Dodoma na TBC Arusha); kuendelea kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha kwa kutangaza utekelezaji wa shughuli za kimkakati za Serikali, kurusha matangazo ya michuano ya mpira wa miguu kitaifa (NBC Premier League mechi 180) na kimataifa (AFCON mechi 64) na kushiriki kampeni za kimkakati za kuhabari zinazoendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Kampeni za mazingira (*Pika kijanja* na *Jicho la Mpita njia*) na Kampeni za utalii *(Slave Caravan*)); kurusha matangazo mubashara ya viongozi wakuu wa kitaifa na matukio yenye manufaa ya umma 500 pamoja na sherehe 15 za kitaifa; na kulipa stahiki za watumishi, upatikanaji wa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi 100 wa kada mbalimbali.

### 5.1.3 KAMPUNI YA MAGAZETI YA SERIKALI (TSN)

**253.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2026/27, TSN imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo; kuandaa na kuchapa makala maalumu za kuhabarisha umma juu ya michuano ya AFCON 2027; kuhabarisha na kuelimisha umma juu ya Mipango, miongozo, mikakati, sera na miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali; kuchapa na kusambaza nakala 1,909,752 za magazeti ya *Daily News* na HabariLEO; kukamilisha mradi wa ukarabati wa Studio ya kisasa ya kidigiti; kuandaa maudhui ya kidigitali na kusambaza kupitia chaneli ya *Dailynews Digital* na mitandao ya kijamii;

kuandaa sheria ya kuanzishwa kwa TSN; na kuwezesha stahiki na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 130 na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 18.

### 5.1.4 BODI YA ITHIBATI YA WAANDISHI WA HABARI

**254.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari itaendelea kutekeleza jukumu lake la kisheria kwa kutoa ithibati na vitambulisho 500 kwa waandishi wa habari kwa lengo la kuhakikisha kuwa waandishi wote wanatekeleza majukumu yao wakiwa na utambulisho rasmi wa kisheria na unaokidhi viwango vya taaluma na maadili; hatua hii itachangia kuongeza ufanisi katika utendaji wa sekta ya habari sambamba na kuimarisha na kuboresha ubora wa kanzidata ya waandishi wa habari nchini.

**255.** ***Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Ithibati, imejipanga kuimarisha usimamizi wa uzingatiaji wa maadili ya taaluma ya uandishi wa habari kwa mujibu wa sheria na kanuni za maadili ya taaluma. Katika kutekeleza azma hiyo, Bodi itaboresha mifumo ya kupokea, kuchakata na kushughulikia malalamiko ili kuhakikisha kuwa haki inatendeka kwa wakati, kwa uwazi na kwa kuzingatia misingi ya haki, usawa na uwajibikaji. Aidha, Bodi itaongeza matumizi ya mifumo ya kidijiti na kuimarisha ufuatiliaji wa mwenendo wa malalamiko ili kuongeza ufanisi, uwazi na imani ya wadau katika utekelezaji wa majukumu yake.

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Ithibati, itaendelea kutoa elimu na mafunzo kwa umma na waandishi wa habari nchini kama sehemu ya kuimarisha taaluma na uelewa wa majukumu ya Bodi ya Ithibati; mafunzo haya yatatekelezwa kwa mtindo endelevu katika kanda tano (5) yakilenga kuwawezesha waandishi kuendana na mabadiliko ya teknolojia, kuzingatia maadili ya taaluma, na kuongeza ubora na weledi wa kazi zao. Aidha, Bodi itaongeza na kuimarisha ushirikiano na taasisi mbalimbali zikiwemo vyuo vikuu, mamlaka za usimamizi na wadau wa sekta ya habari ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakuwa yenye tija, yanazingatia viwango vya kitaaluma, na yanakidhi mahitaji ya wakati pamoja na changamoto zinazoibuka katika mazingira ya kazi.

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Bodi ya Ithibati, imepanga kufanya maboresho ya mfumo wa ithibati na usajili kwa ajili ya kanzidata ya waandishi wa habari nchini. Maboresho hayo yanalenga kuimarisha utambuzi wa waandishi wa habari, kuboresha taratibu za usajili ili ziwe rahisi, wazi na zenye ufanisi zaidi, pamoja na kuongeza usahihi wa taarifa zinazohifadhiwa katika kanzidata hiyo kwa madhumuni ya upangaji, ufuatiliaji na usimamizi bora wa taaluma.

### 5.1.5 KAMATI YA MAUDHUI

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Kamati ya Maudhui imepanga kuendelea kutoa elimu kwa watoa huduma za maudhui na

imeandaa kitabu elekezi kuhusu Kanuni, Miongozo, Masharti ya Leseni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Vilevile, Kamati itaendelea kufuatilia uzingatiaji wa maadili ya utangazaji ili kuhakikisha watoa huduma wanatoa maudhui yanayokidhi Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo kwa kuendelea kufanya vikao vya mashauriano na watoa huduma, na wadau/taasisi nyingine za sekta ya Habari na Utangazaji. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kupitia Kamati ya Maudhui, inatekeleza mfumo wa kushauriana na watoa huduma na kuwapa fursa ya kuondoa kasoro zinazojitokeza kabla ya kuchukua hatua za kiusimamizi.

## 5.2 SEKTA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

### 5.2.1 IDARA YA MAENDELEO YA UTAMADUNI

**259.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo yaliyopangwa kutekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Utamaduni kwa mwaka 2026/27 ni kukamilisha uandishi wa Sera ya Utamaduni ya Mwaka 1997 Toleo la Mwaka 2026; kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997 katika mikoa na mamlaka za Serikali za Mitaa; kuratibu Kampeni ya kitaifa ya kukabiliana na changamoto za mmomonyoko wa maadili nchini; kuandaa Kikao Kazi cha Sekta ya Utamaduni nchini; kuratibu Tamasha la Nne la Kitaifa la Utamaduni na Matamasha mengine matano (5) ya utamaduni yanayoandaliwa na wadau; kuratibu maendeleo na matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa pamoja na kufanya tafiti za lugha, mila na desturi za

jamii za kitanzania.

### 5.2.2 BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)

**260.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni kuratibu Maadhimisho ya Siku ya Lugha ya Kiswahili Duniani katika ngazi ya kitaifa na kikanda; kufanya Kongamano la Kimataifa la Kiswahili jijini Paris, Ufaransa; kusanifisha Istilahi za michezo (AFCON), Sheria na Mseto; kuendeleza Kongoo ya Kiswahili (KOKITA); kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa kuandaa na kurusha hewani jumla ya vipindi 750 kupitia redio na televisheni; kutoa mafunzo ya kuimarisha stadi za kufundisha Kiswahili kwa wageni; na kutoa mafunzo ya msasa ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa makundi maalumu.

**261.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine ni pamoja na kuendesha mtihani wa kupima umahiri wa lugha ya Kiswahili kwa wageni; kuendesha mafunzo ya Kiswahili kwa wageni; kufanya tafiti kwa lengo la kuongeza maneno kwenye Kongoo ya Kiswahili; kuendesha mafunzo kwa wakalimani; na kutoa huduma ya tafsiri kwa nyaraka 800 na kuthibisha kazi 3,000 zinazofanywa na mawakala wa Baraza.

### 5.2.3 KITUO CHA URITHI WA UKOMBOZI WA BARA LA AFRIKA

**262.** ***Mheshimiwa Spika***, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Afrika kitafanya ufuatiliaji wa uhifadhi katika maeneo 15 ya Ukombozi; na kuanzisha vituo saba (7) vya taarifa katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Dodoma, Lindi, Pwani, Iringa na Ruvuma kwa ajili ya kukuza utalii wa ukombozi, utafiti na elimu.

## 5.3 SEKTA YA MAENDELEO YA SANAA

### 5.3.1 IDARA YA MAENDELEO YA SANAA

**263.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Sanaa ni kusimamia maandalizi na uendeshaji wa mashindano ya 74 ya kimataifa ya Miss World 2027 yanayofungamanishwa na AFCON 2027 ili kupata manufaa makubwa ya kiuchumi; kufanya tathimini ya utekelezaji wa majukumu yanayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya Idara ya Maendeleo ya Sanaa; kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Utamaduni katika mikoa 10 ya Tanzania Bara; kuandaa Mkakati wa Maendeleo wa Sekta ya Sanaa; na kuratibu matamasha 3 ya kitaifa na 3 ya kimataifa ya Sanaa ikiwemo Serengeti Music Festival; kuibua na kukuza vipaji vya Sanaa; kuratibu tafiti za mchango wa sekta ya Sanaa kwenye Pato la Taifa; kusimamia hamasa ya ushiriki wa wananchi kwenye mashindano ya AFCON 2027 kupitia shughuli za Sanaa na burudani; na kufuatilia utekelezaji wa Miradi yaTaasisi za Sanaa.

### 5.3.2 BODI YA FILAMU TANZANIA

**264.** ***Mheshimiwa*** **Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yatakayotekelezwa na Bodi ya Filamu ni kuwajengea uwezo wasanii 500 wa filamu na michezo ya kuigiza kupitia programu mbalimbali; kusimamia maudhui ya filamu kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja filamu na tamthilia 300; kusimamia maudhui ya filamu kwa kuhakiki na kupanga katika madaraja michezo sita (6) ya jukwaani; kuratibu Tamasha 1 la Tuzo za Filamu Tanzania (TAFFA) na kusimamia utekelezaji wa matamasha matano (5) yatakayoandaliwa na wadau; kusimamia utayarishaji wa filamu kwa kuchakata maombi na kutoa vibali 400 vya utayarishaji wa filamu; na kuimarisha urasimishaji wa biashara za filamu kwa kutoa leseni 450 na vitambulisho 350 vya wasanii wa filamu na Michezo ya Kuigiza.

### 5.3.3 BARAZA LA SANAA LA TAIFA (BASATA)

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, BASATA imepanga kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwamo; kukuza na kuimarisha Sekta ya Sanaa ili iendelee kutengeneza fursa za ajira na kuchangia Pato la Taifa; kusimamia uzingatiaji wa Maadili katika shughuli za Sanaa kwa kutekeleza Miongozo nane (8) iliyoandaliwa na BASATA na kuandaa miongozo mitano (5); kuimarisha uhusiano na Wadau wa Sekta ya Sanaa wa ndani wanne (4) na wawili (2) nje ya nchi; kuimarisha kanzidata ya wasanii kwa kufanya

utambuzi na usajili wa wasanii na wadau wa sanaa nchini 12,000; kuimarisha utumiaji wa mifumo ya TEHAMA katika kurahisisha utoaji na upatikanaji wa Huduma za Baraza; na kuandaa tuzo ya ubora wa kazi za sanaa.

### 5.3.4 OFISI YA HAKIMILIKI TANZANIA (COSOTA)

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa usimamizi wa Hakimiliki nchini unafanyika kwa ufanisi mkubwa Wizara kupitia COSOTA imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: kufanya mapitio ya Kanuni mbili (2) za Sheria ya hakimiliki na hakishiriki; kutoa leseni kwa Kampuni za Kukusanya na Kugawa Mirabaha (CMOs) katika madaraja manne (4) ya muziki, kazi za maandishi, kazi za vielelezo vya kusikia na kuona *(audiovisual),* sanaa za maonesho na ufundi; kufanya usimamizi, ufuatiliaji na tathmini za utendaji wa CMOs kila robo mwaka, ikijumuisha ukusanyaji na ugawaji wa mirabaha kwa wanufaika; kutoa leseni 10 kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki katika madaraja ambayo hayana CMOs; kufanya programu nne (4) za uhamasishaji na uelimishaji kwa watumiaji na wamiliki wa hakimiliki; kufanya oparesheni nne (4) za kupambana na uharamia (piracy) dhidi ya kazi za sanaa na ubunifu; na kusajili kazi 2,000 za wamiliki wa kazi za ubunifu.

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu mengine yatakayotekelezwa ni: kukusanya tozo ya hakimiliki hadi kufikia shilingi bilioni 1.4 kwa mwaka; kuratibu utatuzi mbadala wa migogoro *(Alternative Dispute*

*Resolution - ADR)* ya hakimiliki; kuimarisha uwezo na uendelevu wa kifedha wa taasisi kwa kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuboresha mapato; kuandaa na kuboresha miongozo mitatu (3) ya ndani kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya utendaji na kuboresha ufanisi; kufanya tafiti moja (1) inayohusiana na masuala ya hakimiliki kwa kushirikiana na vyuo vikuu na taasisi za utafiti; kujenga na kuimarisha mahusiano na ushirikiano na wadau wa tasnia ya sanaa na ubunifu ndani (Taasisi 5 – Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Tume ya Ushindani (FCC), Jeshi la Polisi na nje ya nchi (Mashiriki 6 - WIPO, ARIPO, CISAC, International Federation of Reproduction Rights Organization (IFRRO), International Federation of the Phonographic Industry (IFPI), African Continental Free Trade Area (AfCFTA); kuboresha mfumo wa usajili kidijiti Copyright Registration Management Information System (CRMIS); na kuanzisha Kanzidata ya Kitaifa ya Kazi za Ubunifu.

### 5.3.5 TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO (TaSUBa)

**268.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2026/27, majukumu yatakayotekelezwa ni kudahili na kusajili wanafunzi 900 wa kozi ndefu na 350 wa kozi fupi; kuandaa mitaala mitatu (3) ya masomo ya Sanaa na Utamaduni; kuandaa Tamasha la 44 la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; kutangaza shughuli na mazao yatokanayo na chuo kwa kufanya ziara kwa shule za sekondari 20 katika mikoa

ya Dar es Salaam na Pwani; na kuendesha mafunzo ya kozi fupi kwa wanachuo 100 kwenye vituo vya Dar es Salaam na Songea.

#### 5.3.6 MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** malengo ya Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kwa mwaka 2026/27 ni yafuatayo: kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20 kwa wadau wa tasnia za habari, utamaduni na sanaa; kutangaza huduma zake kwa Wadau kupitia vipindi vya Televisheni, redio, machapisho ya magazeti, machapisho katika mitandao ya kijamii pamoja na vipeperushi; kuwakutanisha wadau wa utamaduni na sanaa pamoja kwa ajili ya kujengewa uwezo na kubadilishana uzoefu na kutatua changamoto za masoko ambapo utaandaa Mkutano Mkuu wa mwaka wa tatu (3) wa wadau wa mfuko na maonesho ya kimataifa ya kazi za utamaduni na sanaa; kuchochea urasimishaji wa kazi za kiutamaduni na Sanaa 11,000 ili zijiendeshe kibiashara, zikuze uchumi na kuzalisha ajira nchini; na kushirikiana na taasisi 5 za kimataifa na taasisi 10 za kitaifa katika kutekeleza shughuli mbalimbali kama mafunzo.

### 5.4 SEKTA YA MAENDELEO YA MICHEZO

#### 5.4.1 IDARA YA MAENDELEO YA MICHEZO

**270.** ***Mheshimiwa Spika***, kuelekea mashindano ya AFCON 2027 yatakayofanyika kuanzia tarehe 19 Juni hadi 17 Julai, 2027, Wizara imejipanga kikamilifu kwa

kushirikisha wadau wote kuhakikisha mashindano haya siyo tu yanafanyika bali yanaweka historia na alama isiyofutika kwa taifa letu. Tayari tunazo Kamati mbalimbali za uratibu kitaifa na katika hili nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Kitaifa na Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ushiriki wao madhubuti.

**271.** ***Mheshimiwa Spika***, pamaoja na miundombinu iliyoelezewa hapo awali, tayari Serikali imewaunganisha pamoja wadau katika sekta za utalii na ukarimu hususan mighahawa, hoteli na huduma za malazi, huduma za usafiri na ushafirishaji (magari, treni, ndege na meli), maeneo ya starehe na burudani kwa mashabiki (fun zones), maboresho ya muonekano wa miji yetu, vivutio vya utalii (mbuga, fukwe, malikale n.k.), matibabu ya kibingwa, ulinzi na usalama, uhamiaji n.k. Mkakati mahsusi wa hamasa kuelekea AFCON 2027 umeandaliwa ambapo utazinduliwa hivi karibuni na kuhakikisha kuwa kila mtanzania anakuwa sehemu ya mashindano haya kwa lengo lengo la kunufaika na fursa za AFCON na kutangaza nchi.

**272.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na hayo yote tumeendelea kushirikiana na wadau na wanamichezo maarufu walioonekana kusaidia au kutoa mchango mkubwa kwa nchi zao na dunia katika soka. Na hapa niruhusu nimtambue mwanamichezo maarufu Didier Drogba ambaye ni mchezaji bora wa wakati wote na nahodha wa zamani wa timu ya taifa ya Ivory Coast. Pia,

amewahi kutumikia vilabu vikubwa vya mpira wa miguu duniani vya Chelsea na Galatasaray na ni mmiliki wa klabu ya Phoenix Rising ya Marekani. Uwepo wake leo ni uthibitisho tosha wa namna gani Serikali imeamua kuitumia AFCON 2027 kuitangaza taswira ya Tanzania kimataifa.

**273.** ***Mheshimiwa Spika***, majukumu mengine ni: kuratibu na kushiriki mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa ya michezo; kuratibu udhibiti wa matumizi ya dawa na mbinu haramu michezoni; kuratibu Michezo ya UMITASHUMTA, UMISSETA na FEASSA kwa kushirikiana na OWM-TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; kusimamia uendeshaji wa Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo Nchini (SIMA); kuratibu kikao kazi cha Maafisa Michezo nchini; kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma za kinga na tiba kwa wanamichezo 800 watakaoshiriki kwenye michezo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa; kuratibu Michezo ya Jumuiya ya Madola; kuandaa siku ya michezo duniani; kuandaa kongamano la wadau wa michezo; na kuratibu ushirikiano wa michezo na nchi mbalimbali.

### 5.4.2 BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27 majukumu yatakayotekelezwa ni pamoja na kuendelea kuwezesha na kuzigharamia timu 20 za taifa kushiriki mashindano mbalimbali ya Kimataifa; kuendelea kutoa mafunzo ya utaalamu wa michezo na usimamizi kwa wataalamu 500 ili kupata wataalamu wa

michezo nchini; kuendelea kusajili Vyama/Mashirikisho na vilabu vya michezo vipatavyo 200**;** kuratibu matamasha matatu (3) ya Michezo ya Wanawake; kuendelea kuhamasisha utawala bora katika vyama na mashirikisho ya michezo 45; kuratibu chaguzi 8 za vyama na mashirikisho ya michezo kuidhinisha vibali 400 vya matukio mbalimbali ya michezo; kuendelea kutoa tuzo kwa wanamichezo bora kwa michezo yote inayochezwa Tanzania; kuendelea kutoa elimu kwa umma na wadau 350 kushiriki katika michezo kupitia vyombo vya habari; kukamilisha ujenzi wa kituo cha michezo na mazoezi mkoani Manyara; na kukamilisha marekebisho ya sheria ya Baraza la Michezo la Taifa pamoja na kuboresha muundo wa Utumishi wa Baraza la Michezo la Taifa.

### 5.4.3 CHUO CHA MAENDELEO YA MICHEZO MALYA

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ni kutoa mafuzo ya muda mrefu kwa wanachuo 500 na muda mfupi kwa wadau wa michezo 700; kuongeza programu sita (6) mpya za mafunzo ya muda mrefu; kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia; kujenga mahusiano na vyuo sita (6) vya michezo vya ndani vitatu (3) na nje nchi vitatu (3); kukamilisha muundo wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ili kuwa Taasisi ya elimu ya Michezo; na kuanzisha kambi ya michezo ya vijana kwa ajili ya kumbukumbu ya kudumu ya mchango wa AFCON 2027.

### 5.4.4 UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2026/27, malengo yatakayotekelezwa ni kuhakikisha stahiki mbalimbali za Watumishi 261 na Viongozi wa Wizara zinatolewa; kutoa huduma ya usafiri kwa Viongozi na Watumishi 261 wa Wizara; kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo wa Wizara; kusimamia mpango wa utekelezaji wa majukumu ya watumishi wa Wizara; kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kuwapatia vitendea kazi Watumishi 261 wa Wizara; na kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa rasilimaliwatu.

## 5.5 MIRADI YA MAENDELEO

**277.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa Upanuzi wa usikivu wa TBC imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufunga mitambo kwenye vituo (20) vya urushaji wa matangazo ya FM ya redio ambapo ujenzi wa majengo unaendelea; ununuzi wa haki na uandaaji wa maudhui ya Michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027); kuendelea na mradi wa kuhamisha maudhui zilizopo katika maktaba za TBC kutoka mfumo wa analojia kwenda kidijiti; kununua vitendea kazi ikiwemo magari 20 kwa ajili ya shughuli za utangazaji, kompyuta mpakato 300, kamera 50, vinasa sauti 50, FLY AWAY - 2, Ndege nyuki (Drone) sita (6), Live-U 13 na quantum 15 kwa ajili ya kuimarisha chaneli za kimkakati za TBC (TBC 2, Bongo

FM, TBC mtandaoni, Tanzania Safari Chaneli na Televisheni ya Kiingereza) na redio za Kanda (TBC Arusha na TBC Dodoma) pamoja na kuongeza uwezo wa urushaji wa Matangazo Mbashara; kuendelea na Ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya TBC eneo la Vikonje jijini Dodoma.

**278.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa Ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la kiwanda cha uchapaji; ukamilishaji wa ufungaji wa Mitambo Mipya ya Kisasa ya Uchapaji; kuunganisha mifumo ya uendeshaji wa shughuli za uchapaji *(Digital Convergence);* ufungaji mtambo maalumu wa uchapaji wa kisasa wa Vitambulisho awamu II; ufungaji mitambo ya urejelezaji (recycling) kutokana na uzalishaji wa kiwanda kipya cha uchapaji; na kuimarisha ofisi za biashara kikanda.

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mradi wa Habari kwa umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kukusanya, kuchakata na kusambaza taarifa (habari) kuhusu miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali; kuandaa na kurusha vipindi (picha jongefu) vinavyoitangaza Tanzania, kuratibu na kuandaa mikutano ya Wanahabari na Mawaziri, Wakuu wa Mikoa; Taasisi na Wakurugenzi wa Halmashauri na Msemaji Mkuu wa Serikali kutangaza utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kurusha matangazo mbashara (Livestreaming) ya miradi na matukio ya Serikali; kugharamia vipindi vya televisheni vya kutangaza utekelezaji wa shughuli za Serikali na kuchapisha

nakala 10,000 za Jarida la NCHI YETU.

**280.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Ukombozi wa Afrika, Kongwa imepanga kumtafuta Mshauri Elekezi kwa ajili ya upembuzi yakinifu; kumtafuta Mkandarasi wa mradi; na kuanza ujenzi.

**281.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia mradi wa Kuimarisha BAKITA na Kukuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya usanifishaji mkubwa wa pili wa lugha ya Kiswahili; kufanya Maadhimisho ya sita (6) ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU); kuendeleza kongoo ya Taifa; kuandaa atlasi ya lugha za Tanzania; ubidhaishaji kwa kufungua vituo vya kufundisha Kiswahili kwa wageni; kutengeneza mifumo miwili ya Kiswahili (mfumo wa mauzo ya machapisho pamoja na mfumo wa tafsiri ya nyaraka); na kufanya maboresho ya darasa la kufundishia Kiswahili kwa wageni.

**282.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa), imepanga: ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia; kuanza ujenzi wa jengo moja (1) la utawala; kuendelea na ujenzi wa uzio kuzunguka hosteli za wanachuo; kuanza ujenzi wa jengo moja la hosteli za wanachuo; kufanya ufungaji na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA; kuboresha vifaa na miundombinu ya Tamasha la Kimataifa la Sanaa na Utamaduni Bagamoyo; kuendela na ujenzi wa jengo moja la kutunzia vifaa *(warehouse);* kuendelea na

ukarabati wa vifaa na miundombinu ya Taasisi; na kununua jenereta moja.

**283.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa ujenzi wa Ukumbi wa Wazi wa Sanaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya upembuzi yakinifu wa mradi; kuandaa michoro; kufanya ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa eneo la Ilala Sharif Shamba; kutafuta eneo na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Makumbusho ya Taifa ya Sanaa *(National Art Gallery)* jijini Dodoma; kuendelea na maandalizi ya Atlasi ya Vifaa vya Muziki wa Asili wa Tanzania; na kuendelea na mapitio na maboresho ya Mfumo wa AMIS pamoja na kutengeneza BASATA mobile APP.

**284.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa ujenzi wa Jumba Changamani la Filamu Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kufanya tathmini ya awali ya mradi *(preliminary assessment),* kufanya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* ili kubaini uhalisia wa kiuchumi, kiufundi na kijamii wa mradi. Mradi huu ni sehemu ya miradi iliyoombewa mkopo wa masharti nafuu kutoka benki ya EXIM ya Korea Kusini ambapo taratibu zitakapokamilika utekelezaji wake utaanza na unatarajiwa kugharimu takribani bilioni 150.

**285.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kuendelea kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wadau wa utamaduni na sanaa ambapo mikopo itakayotolewa itakuwa na thamani ya

shilingi 20,000,000,000 kwa wasanii 8,000 na ajira zinazotarajiwa kuzalishwa ni 105,000; kuwajengea uwezo wadau wa utamaduni na sanaa 15,000 katika masuala yanayohusiana na elimu ya fedha, uwekezaji, masoko, TEHAMA na hifadhi ya jamii; kuendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo ili kuwa na Mfuko endelevu; na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa wanufaika 200 wa Mfuko.

**286.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea na uboreshaji wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya ambapo imepanga: kuanza ujenzi wa maktaba, maabara ya michezo, ujenzi wa madarasa, ujenzi wa jengo la utawala na nyumba kumi (10) za watumishi; kuendelea na ukarabati wa nyumba kumi (10) za watumishi; kukarabati viwanja vya michezo saba (7) ambavyo ni Mpira wa Miguu viwili (2), Netiboli kimoja (1), Mpira wa Mikono viwili (2) na Mpira wa Kikapu viwili (2); kuimarisha mfumo wa mawasiliano; na kuendelea na ufungaji wa huduma za maji, umeme na ulinzi.

**287.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika mradi wa Akademia ya Michezo katika Chuo cha Michezo imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya akademia ya michezo ikiwemo viwanja vya mpira wa miguu vitatu (3), netiboli viwili (2), kikapu viwili (2), wavu viwili(2), mikono kimoja (1), tenisi viwili (2), jengo moja la madarasa lenye vyumba vya madarasa nane (8), bwalo moja(1), na hosteli moja (1), na kuanza ujenzi wa bwawa la kuongelea na jengo la utawala.

**288.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Michezo umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: kugharamia uendeshaji wa mashindano ya AFCON 2027 katika vituo vya Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar ikiwemo kugharamia timu ya Taifa, Kamati za uratibu za Kitaifa, uratibu wa mashindano na wajibu wa Tanzania kimkataba; kuratibu Mashindano ya Urembo ya Dunia (Miss World) kama sehemu ya matukio ya AFCON 2027; kuwezesha ushiriki wa timu na wanamichezo wa Kitanzania katika mashindano ya kimataifa; kuanza ujenzi wa ofisi ya makao makuu ya Baraza jijini Dodoma; kuanza ujenzi wa kituo cha michezo katika Mkoa wa Manyara.

**289.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo; kukamilisha maboresho ya eneo la kuchezea (pitch); kuboresha eneo la jukwaa la wageni mashuhuri (VVIP); kutoa na kuweka milango mipya katika ofisi zote zilizopo uwanjani; kuweka mfumo wa TEHAMA wa kuingia uwanjani; na kuweka milango mipya katika vyoo vya watazamaji katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Aidha, Serikali itakamilisha ukarabati wa uwanja wa uhuru kwa kufungua viti 1,446 katika eneo la jukwaa la VIP; kuendelea na upanuzi wa vyumba vya kubadilishia nguo vya wachezaji; kufunga taa mpya za Uwanja (Pitch lights); na kukamilisha marekebisho ya eneo la kuchezea (pitch). Kazi nyingine ni kukamilisha ujenzi wa viwanja vya mazoezi kwa ajili ya AFCON 2027 vya Gymkhana 2, Farasi na *Leaders Club*.

**290. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa uwanja wa Mpira wa Miguu wa Arusha Serikali imepanga: kukamilisha ujenzi wa uwanja ikiwemo ujenzi wa eneo la kuchezea (pitch); kuweka Mfumo wa kudhibiti halijoto *(Heating Ventlation and Air Conditioning - HVAC)*; na kukamilisha viwanja vya mazoezi vya AFCON 2027 katika maeneo ya Magereza ya Kisongo, Engutoto na Mgambo.

**291. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa Dodoma Serikali imepanga: kuanza ujenzi wa jengo kuu la uwanja wa michezo, ujenzi wa miundombinu saidizi itakayojumuisha huduma za maji, umeme, barabara na mtandao wa mawasiliano. Serikali itajenga viwanja viwili (2) vya mazoezi pamoja na jengo la Kituo cha Habari *(Media Centre)* katika eneo la mradi.

**292. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (*Recreational Centres*) Dodoma na Dar es Salaam Serikali imepanga: kukamilisha ujenzi wa viwanja viwili (2) vya mpira wa miguu, mpira wa mikono (1), mpira wa kikapu (1), netiboli (1) na wavu (1); kukamilisha ujenzi wa majengo ya utawala, kubadilishia nguo na eneo la burudani linalojumuisha jiko, kaunta ya vinywaji na vizimba vya kupumzikia; ujenzi wa uzio; ujenzi wa bwawa la kuogelea; ujenzi wa eneo la maegesho ya magari; na upandaji wa miti eneo la bustani.

**293. *Mheshimiwa Spika,*** katika mradi wa Ujenzi

na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika shule saba (7) maalumu za michezo kati ya 56 Serikali imepanga: kuanza ujenzi wa viwanja wa mpira wa miguu, riadha, kikapu, tenisi, mpira wa mikono, mpira wa wavu na netiboli katika shule za sekondari Nanguruwe (Mtwara), Kicheba (Tanga), Bisheshe (Kagera), New Kiomboi (Singida), Dkt. Damasi Ndumbaro (Ruvuma), Ikwiriri (Pwani) na Sekondari Dodoma (Dodoma).

**294.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mradi wa ujenzi wa Arena ya Michezo Serikali imepanga: kuandaa mahitaji ya mradi; michoro; na kumtafuta Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa Mradi. Eneo la ujenzi wa mradi limepatikana ambapo ekari 12 zimetengwa katika eneo la Tanganyika Packers Kawe jijini Dar es Salaam. Mradi huu ni sehemu ya miradi iliyoombewa mkopo wa masharti nafuu kutoka benki ya EXIM ya Korea Kusini ambapo taratibu zitakapokamilika utekelezaji wake utaanza.

**295.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika mradi wa Maendeleo ya Taasisi imepanga kutekeleza shughuli zilifuatazo; kufuatilia na kutathmini programu na miradi inayotekelezwa chini ya Wizara; kuratibu Ofisi ya Kanda ya Sekretarieti ya Baraza la Michezo la Umoja wa Afrika Kanda ya IV; kuratibu usimamizi wa vihatarishi katika miradi inayotekelezwa na Wizara; uendeshaji wa Wakala wa Usimamizi wa Miundombinu ya Michezo (SIMA); kuratibu shughuli za Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari; kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Mapato ya Wizara na taasisi zake; na

kuwajengea uwezo watumishi kuhusu uandishi wa maandiko ya miradi, maandalizi ya bajeti na masuala ya usimamizi wa vihatarishi.

## 6.0 SHUKURANI

**296.** ***Mheshimiwa Spika***, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wamechangia kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Ushirikiano na misaada yao ya kifedha, kiufundi na kitaalamu imekuwa nguzo ya mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2025/26. Wadau hao ni pamoja na nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kimataifa, taasisi za fedha, vyombo vya habari, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini.

**297.** ***Mheshimiwa Spika*****,** kwa upande wa wadau siyo rahisi kuwataja wote kwa majina, nitawataja wachache nikianza na wadau wa ndani, ambao ni Kampuni za Azam Media; Multichoice Tanzania; Airtel Tanzania; Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Benki ya NMB; Benki ya CRDB; Benki ya NBC; Tanzania National Parks (TANAPA); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro (NCA); Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA); Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF); na Makumbusho ya Taifa. Aidha, wadau wengine ni pamoja na Shirika la Bima la Taifa (NIC); Wakala wa Serikali Mtandao (eGA); Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC); Shirika la Culture and Development East Africa (CDEA); Taasisi ya Global Opportunity Youth

Network (GOYN); Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Kampuni ya Startimes; Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF); Vituo vya Redio vya Clouds Media Group, EFM; Mega FM; Wasafi; Crown Fm; Dodoma FM; Chamwino Arts Center; Vyama na Mashirikisho ya Sanaa; Mingle and Audience Agency; Jambo Group of Companies (JAMUKAYA); Kilimarathon; Sports Pesa; na 361 Degrees Africa Limited.

**298.** ***Mheshimiwa Spika,*** natambua mchango mkubwa wa Balozi zote za Tanzania katika mataifa mbalimbali; Serikali ya Mji wa Busan nchini Korea ya Kusini; Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA); Bagamoyo Friendship Society (Ujerumani); Musicians for a Better Life (Ujerumani); Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO); Wamiliki wa Kampuni za Emirates; Jamhuri ya Watu wa China; Umoja wa Ulaya; Organisation of African Carribean Pacific States (OACPS); na Kituo cha Sanaa na Utamaduni cha Alliance Francaise.

**299.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mara nyingine tena ninamshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maono yake, maelekezo na miongozo yake katika utekelezaji wa majukumu ya sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wizara hii tunakiri kuwa tunadaiwa matokeo, Mheshimiwa Rais amemaliza kazi yake. Nimhakikishie kuwa katika kipindi alichoniamini kusimamia majukumu haya sitomwangusha. Watanzania tuendelee kumwombea

kwa Mwenyezi Mungu amjalie afya njema ili aendee kutuongoza vema.

**300.** ***Mheshimiwa Spika***, pia ninamshukuru Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na ushauri katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za Sekta za Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Vile vile, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na maelekezo yake yaliyowezesha kuboresha utendaji wa Wizara na Serikali kwa ujumla.

**301.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Viongozi wa dini wanaoendelea kuliombea taifa letu usiku na mchana libaki moja, lenye mshikamano na amani. Niendelee kuwaomba wasichoke, tumlilie Mungu wetu kwa imani zetu aendelee kulifunika na kulinda Taifa la Tanzania dhidi ya maadui wa ndani na nje.

**302.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninakishukuru Chama cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kunipendekeza kuwa mgombea na hatimaye kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi kuwa Mbunge wa jimbo la Arusha Mjini. Ninaahidi kulipa imani hii kubwa kwa utumishi wenye matokeo chanya kwa taifa langu.

**303.** Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine niwashukuru wananchi wa Jimbo la Arusha mjini kwa

ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya jimbo letu. Arusha tulichelewa sana kutekeleza shughuli za msingi za maendeleo na sasa wananchi wameamua kuibadili sura ya Arusha kwa kufanya kazi. Nawashukuru sana Waheshimiwa madiwani wote wa Arusha wakiongozwa na Mheshimiwa Maximilian Iraghe, Mstahiki Meya.

**304.** ***Mheshimiwa Spika***, kufika kwangu hapa leo hii, wapo watu ambao Mwenyezi Mungu kwa kusudi lake aliwatumia katika namna moja au nyingine katika safari yangu. Namkumbuka na kumshukuru Marehemu Samwel Sitta, aliyekuwa Spika wa Bunge la Tisa kwa maelezi yake kwangu kisiasa na kunijenga nilivyo; Marehemu Reginald Mengi kwa maelezi yake kifamilia na elimu katika wakati nilioihitaji zaidi; Marehemu Bernard Membe, aliyekuwa mwalimu wangu nguli wa siasa na mikakati ndani ya Chama cha Mapinduzi; Mheshimiwa Harson Mwakyembe aliyekuwa Mbunge na Waziri pamoja na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa aliyekuwa Mbunge kwa mchango wao mkubwa katika maisha yangu ya siasa.

**305.** ***Mheshimiwa Spika***, kipekee kabisa niwashukuru Mheshimiwa Hamis M. Mwinjuma (Mb.), Naibu Waziri Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu na Ndugu Methusela Ntonda, Naibu Katibu Mkuu. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Bodi za Taasisi, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara; na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao

kwa weledi mkubwa hatua iliyopelekea mafanikio makubwa tunayoyashuhudia hivi leo.

**306.** ***Mheshimiwa Spika***, niishukuru familia yangu, hususan mke wangu kipenzi Maria Felix Massenge na watoto wetu wapendwa Keagan, Kenzel na Kenzlin. Hawa wamekuwa faraja kubwa kwangu kwanza kwa maombi yao, uvumilivu ninapokuwa katika majukumu ya kitaifa na usimamizi imara wa wajibu wao katika familia. Haya yamenipa moyo na faraja kuendelea mbele bila kuchoka wala kukata tamaa katika kulitumikia Taifa. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**307.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii inapatikana kwenye tovuti ya Wizara ambayo ni *www.michezo.go.tz.*

## 7.0 HITIMISHO

**308.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2026/27, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 1,058,000,000**. Vyanzo vya mapato hayo ni Vitambulisho vya Waandishi wa Habari, machapisho ya picha, mabango na majarida, usajili wa magazeti, ada ya mwaka ya magazeti, viingilio katika uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru, ada za upangishaji na matangazo katika eneo changamani la michezo Dar es Salaam pamoja na ada za wanachuo kutoka Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Aidha,

kwa upande wa Taasisi 12 zilizo chini ya Wizara kiasi kinachotarajiwa kukusanywa ni **shilingi 40,898,692,000**.

**309.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza majukumu ya Wizara katika mwaka 2026/27 naomba Bunge lako Tukufu liridhie na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2026/27 yenye jumla ya **Shilingi 525,327,857,000.** Kati ya bajeti hiyo **Shilingi 39,071,597,000** ni kwa ajili ya Mishahara; **Shilingi 28,065,472,000** ni Matumizi Mengineyo; na Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 458,190,778,000.**

**310.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.




Kikosi cha Timu ya Taifa ya Mpira wa Miguu (Taifa Stars) kilichofuzu hatua ya 16 Bora katika Mashindano ya Kombe la Mataifa Afrika mwaka 2025 (AFCON 2025) nchini Morocco.




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Paul Makonda akimkabidhi hundi ya shilingi Milioni 5.5 Ndg. William Morwabe, ambaye ni miongoni mwa washindi wa Kilimanjaro Marathon tarehe 22, Machi 2026, Moshi.




Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
S.L.P 25
Dodoma, Tanzania
Simu: 026 2322129
Barua pepe: km@michezo.go.tz
www.michezo.go.tz